JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI

# RIPOTI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI

## KUHUSU UKAGUZI WA TAARIFA ZA FEDHA ZA MIRADI YA MAENDELEO KWA MWAKA WA FEDHA ULIOISHIA TAREHE 30 JUNI, 2013

**Machi, 2014**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI**

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi,
Barabara ya Samora, S.L.P. 9080, Dar es Salaam.Simu ya Upepo:
'Ukaguzi' D'Salaam, Simu: 255(022)2115157/8, Tarakishi: 255(022)2117527,
Barua pepe: ocag@nao.go.tz, tovuti: www.nao.go.tz

Mh. Dkt. Jakaya M. Kikwete,
Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,
Ikulu,
S.L.P. 9120,
**Dar es Salaam.**

**Yah: Kuwasilisha Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu ukaguzi wa Taarifa za Fedha za Miradi ya Maendeleo kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2013**

Kwa mujibu wa Ibara ya 143 (4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (iliyorekebishwa 2005) na Kifungu cha 34 (1)(c) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na.11 ya mwaka 2008, ninawasilisha kwako ripoti ya tatu inayohusu miradi ya maendeleo kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2013 iliyotajwa hapo juu.

Nawasilisha.

Ludovick S. L. Utouh
**MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI**

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali,
Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi,
Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**(Ilianzishwa kwa mujibu wa Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania)**

**Madaraka na wajibu wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali** yameelezwa kwenye Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (iliyorekebishwa 2005) na kufafanuliwa zaidi katika Kifungu cha 10(1) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na.11 ya mwaka 2008.

**Dira**
Kuwa kituo cha ufanisi katika ukaguzi wa hesabu za Serikali na taasisi za umma.

**Dhamiri**
Kutoa huduma ya ukaguzi wa hesabu yenye tija ili kuimarisha uwajibikaji na thamani ya fedha katika kukusanya na kutumia rasilimali za umma.

**Katika kutoa huduma zenye ubora, ofisi hii inaongozwa na vigezo vya msingi vifuatavyo:**

- **Uadilifu**
  Sisi ni asasi adilifu inayotoa huduma kwa namna isiyo na upendeleo.
- **Ubora**
  Sisi ni wanataaluma wanaotoa huduma zenye ubora kwa kuzingatia viwango kubalifu vya ukaguzi.
- **Uaminifu**
  Tunahakikisha kuwa na kiwango cha juu cha uaminifu na kuzingatia Utawala wa Sheria.
- **Mtazamo wa watu**
  Tunatazama na kukazia zaidi katika matarajio ya wadau wetu kwa kujenga utamaduni mzuri wa kuhudumia mteja na kuwa na watumishi wataalamu na wenye motisha ya kazi.
- **Uvumbuzi:**
  Sisi ni asasi ambayo wakati wote inahamasisha utamaduni wa kupokea na kuendeleza mawazo mapya kutoka ndani na nje ya asasi.
- **Matumizi bora ya rasilimali**
  Sisi ni asasi inayothamini na kutumia rasilimali za umma ilizokabidhiwa kwa umakini mkubwa.

**Tunatimiza haya kwa kufanya yafuatayo:-**

- Kuchangia katika matumizi bora ya fedha za umma kwa kuhakikisha kwamba wakaguliwa wetu wanawajibika kutunza rasilimali walizokabidhiwa;
- Kusaidia kuimarisha ubora wa utoaji huduma kwa kuchangia ubunifu kwa matumizi bora ya rasillimali za umma;
- Kutoa ushauri wa kitaalamu kwa wadau wetu kuhusu mapungufu katika uendeshaji wa shughuli zao;
- Kuwahusisha wadau wetu katika mfumo wa ukaguzi; na
- Kuwapa wakaguzi nyenzo za kufanya kazi ambazo zitaimarisha uhuru wa ofisi ya ukaguzi.

© **Ripoti hii imekusudiwa kwa matumizi ya Mamlaka za Serikali. Hata hivyo, mara baada ya kupokelewa na Spika na kuwasilishwa Bungeni, ripoti hii huwa ni kumbukumbu ya umma na usambazaji wake hauwezi kuzuiwa.**

# YALIYOMO

**Madaraka na Wajibu wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali**...ii
Dira ..........ii
Dhamiri ..........ii
Orodha ya Majedwali ..........v
Orodha ya Michoro ..........viii
Dibaji ..........xi
Shukrani ..........xiv
Muhtasari wa Mambo Muhimu katika Ripoti ya Ukaguzi wa Taarifa za Fedha za Miradi Inayofadhiliwa na Washirika wa Maendeleo kwa Mwaka 2012/2013 ..........xvi

**SURA YA KWANZA..........1**
1.0 Utangulizi..........1
1.1 Mamlaka na Umuhimu wa Ukaguzi ..........1
1.2 Majukumu na wajibu wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Miradi ya Maendeleo ..........2
1.3 Muundo wa Kazi za Ukaguzi ..........2
1.4 Mawanda na Viwango vya Ukaguzi vinavyotumika ..........3
1.5 Sera ya Kihasibu ..........4
1.6 Kuandaa na Kuwasilisha Hesabu kwa ajili ya Ukaguzi ..........4
1.7 Mfumo wa Udhibiti wa Ndani ..........5

**SURA YA PILI ..........6**
**Misingi na Mwelekeo wa Hati za Ukaguzi**..........6
2.0 Utangulizi..........6
2.1 Aina ya Hati ya Ukaguzi ..........6
2.2 Mwelekeo wa hati za ukaguzi ..........8
2.3 Uwasilishaji na uchambuzi wa matokeo ya ukaguzi..........9

**SURA YA TATU..........50**
**Utekelezaji wa Mapendekezo katika Ripoti za ..........**
**Kaguzi za Miaka ya Nyuma..........50**
3.0 Utangulizi..........50
3.1 Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo (ASDP)..........51
3.2 Mfuko wa Maendeleo ya Afya (HBF) ..........51
3.3 Mfuko wa Maendeleo ya Jamii Tanzania (TASAF)..........51
3.4 Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji (WSDP)..........52
3.5 Miradi Mingine ..........52

**SURA YA NNE ..........53**
**Utendaji wa Kifedha** ..........53
4.0 Utangulizi..........53

4.1 Programu ya Maendeleo Katika Sekta ya Kilimo ........................ 53
4.2 Ufadhili wa Mfuko wa Maendeleo ya Afya ............................... 56
4.3 Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) ................................. 60
4.4 Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji .............................. 63
4.5 Miradi Mingine ...................................................... 66

**SURA YA TANO ........................................................ 72**
**Udhaifu Katika Usimamizi wa Fedha** ................................... 72
5.0 Utangulizi ........................................................... 72
5.1 Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo (ASDP) ...................... 72
5.2 Mfuko wa Maendeleo ya Afya ........................................... 78
5.3 Mfuko wa Maendeleo ya Jamii Tanzania (TASAF) ......................... 82
5.4 Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji (WSDP) ........................ 88
5.5 Miradi Mingine ...................................................... 89

**SURA YA SITA ......................................................... 93**
**Mapitio ya Taratibu na Mikataba ya Manunuzi ........................... 93**
6.0 Utangulizi ........................................................... 93
6.1 Programu ya Maendeleo katika Sekta ya Kilimo ......................... 93
6.2 Mfuko wa Maendeleo ya Afya ........................................... 97
6.3 Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) ................................. 102
6.4 Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji .............................. 103
6.5 Miradi Mingine ..................................................... 108

**SURA YA SABA ........................................................ 110**
**Kaguzi Maalum** ....................................................... 110
7.0 Utangulizi .......................................................... 110
7.1 Ukaguzi maalum wa Mfuko wa Maendeleo ya Afya (HBF) ................... 110
7.2 Masuala yaliyojitokeza katika ukaguzi maalum wa miradi inayofadhiliwa na Shirika la Maendeleo la Denmark "PFM" na "SWMP" ........................................... 116

**SURA YA NANE ........................................................ 120**
**Hitimisho Na Mapendekezo ............................................. 120**
8.0 Utangulizi .......................................................... 120
8.1 Hitimisho la Jumla .................................................. 120
8.2 Mambo muhimu ya kuzingatia kutokana na ukaguzi maalum ..... 122
8.3 Mapendekezo ya Jumla ................................................ 122
**Viambatanisho** ....................................................... 126

## Orodha ya Majedwali


Jedwali 1: Mchanganuo wa hati za ukaguzi zilizotolewa .......................... xvii
Jedwali 2: Mwelekeo wa hati za Ukaguzi wa miradi ................................ xvii
Jedwali 3: Mchanganuo wa fedha za Miradi .............................................. xix
Jedwali 4: Mchanganuo wa hati za maoni ya ukaguzi.................................... 8
Jedwali 5: Mwelekeo wa hati za Ukaguzi wa miradi .................................... 8
Jedwali 6: Halmashauri zilizopata hati zinazoridhisha................................. 10
Jedwali 7: Halmashauri zilizopata hati yenye shaka.................................... 12
Jedwali 8: Halmashauri iliyopata hati isiyoridhisha .................................... 16
Jedwali 9: Halmashauri iliyopata hati isiyoridhisha .................................... 17
Jedwali 10: Halmashauri ambazo hazikupata Fedha za Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo ................................................... 18
Jedwali 11: Halmashauri zilizopata hati inayoridhisha ............................... 19
Jedwali 12: Halmashauri zilizopata hati zenye shaka.................................. 21
Jedwali 13: Halmashauri zilizopata hati isiyoridhisha................................. 29
Jedwali 14: Halmashauri iliyopata hati mbaya ............................................ 30
Jedwali 15: Halmashauri ambazo hazikupata fedha .................................... 30
Jedwali 16: Halmashauri zilizopata hati inayoridhisha ............................... 32
Jedwali 17: Halmashauri zilizopata hati inayotia shaka .............................. 33
Jedwali 18: Halmashauri zilizopata hati mbaya........................................... 36
Jedwali 19: Halmashauri ambazo hazikukaguliwa kwa mwaka wa fedha 2012/2013......................................................................... 37
Jedwali 20: Watekelezaji wa programu ya maendeleo ya sekta ya maji waliopata hati zinazoridhisha .................................................. 38
Jedwali 21: Watekelezaji waliopata hati yenye shaka ................................. 40
Jedwali 22: Watekelezaji wa programu ya maendeleo ya sekta ya maji waliopata hati isiyoridhisha...................................................... 42
Jedwali 23: Mtekelezaji wa programu ya maendeleo ya sekta ya maji aliyepata hati mbaya................................................................ 43
Jedwali 24: Halmashauri ambazo hazikupewa fedha za programu ya maendeleo ya sekta ya maji...................................................... 44
Jedwali 25: Hati inayoridhishana isiyokuwa na mambo ya msisitizo .......... 44
Jedwali 26: Miradi Mitatu (3) iliyopata hati yenye shaka ........................... 49
Jedwali 27: Mchanganuo wa utekelezaji wa mapendekezo katika ripoti za kaguzi za miaka ya nyuma ....................................................... 50
Jedwali 28: Akaunti Kuu ya Mradi.............................................................. 54
Jedwali 29: Vyanzo vya fedha Programu ya Kilimo ................................... 55
Jedwali 30: Mchanganuo wa fedha za TAMISEMI ..................................... 56
Jedwali 31: Vyanzo vya Fedha vya Mfuko wa Maendeleo ya Afya ............ 57

Jedwali 32: Mapokezi na Uhamishaji wa fedha kwenda kwa Wadau wa afya ........ 57
Jedwali 33: Vyanzo vya Fedha kwa Mfuko wa Maendeleo ya Afya – Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii ........ 59
Jedwali 34: Vyanzo vya fedha kwa mfuko wa Maendeleo ya Afya TAMISEMI ........ 60
Jedwali 35: Vyanzo vya Fedha Mfuko wa Maendeleo ........ 60
Jedwali 36: Vyanzo vya Fedha na Matumizi ........ 61
Jedwali 37: Fedha zilizopelekwa Mamlaka za Serikali za Mitaa ........ 62
Jedwali 38: Mpango wa Uhawilishaji Fedha kwa Kaya Masikini ........ 62
Jedwali 39: Utendaji Kifedha katika Akaunti Kuu ya Mradi Hazina ........ 63
Jedwali 40: Chanzo cha Fedha za Mradi wa Maji 2012/13 ........ 64
Jedwali 41:Mchango Kutoka kwa Washirika wa Maendeleo ........ 65
Jedwali 42: Utendaji wa Kifedha – Mamlaka za Serikali za Mitaa ........ 66
Jedwali 43: Utendaji wa Kifedha - Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii ........ 66
Jedwali 44: Mapato na Matumizi - Hazina ........ 67
Jedwali 45: Mapato na Matumizi - Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii ........ 67
Jedwali 46: Mapato na Matumizi - Akaunti ya Fedha za Kigeni Benki Kuu ........ 68
Jedwali 47: Mapato na Matumizi Programu ya Kitaifa ya Kudhibiti Ukimwi ........ 68
Jedwali 48: Mapato na Matumizi - Ufuatiliaji na Tathmini ........ 69
Jedwali 49: Mapato na Matumizi - Uimarishaji Mfumo wa Afya ........ 69
Jedwali 50: Mapato na Matumizi Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ........ 69
Jedwali 51: Mapato na Matumizi Tume ya Kudhiditi Ukimwi ........ 70
Jedwali 52: Mapato na Matumizi Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Afya-Mwanza ........ 71
Jedwali 53: Mapato na matumizi - Kitengo cha Uchunguzi wa Magonjwa . 71
Jedwali 54: Malipo yenye Nyaraka Pungufu ........ 72
Jedwali 55: Hati za malipo zisizokaguliwa ........ 74
Jedwali 56: Matumizi yaliyofanywa kwa kutumia vifungu visivyohusika .. 74
Jedwali 57: Matumizi yaliyofanywa nje ya Bajeti iliyodhinishwa ........ 76
Jedwali 58: Malipo yasiyokubalika ........ 76
Jedwali 59: Malipo yaliyofanyika bila kibali ........ 77
Jedwali 60: Kukosekana kwa taarifa za robo mwaka za mkaguzi wa ndani ........ 79
Jedwali 61: Masurufu yasiyorejeshwa ........ 79
Jedwali 62: Hati za malipo zilizokosekana ........ 81
Jedwali 63: Malipo yasiyokubalika ya kodi ya ongezeko la thamani ........ 82
Jedwali 64: Miradi iliyopelekewa fedha lakini haijafanyika ........ 83
Jedwali 65: Miradi iliyokamilika lakini haijaaza kutumika ........ 83

Jedwali 66: Miradi ambayo haijakamilika .................................................. 84
Jedwali 67: Fedha zilizohamishwa lakini hazijapokelewa ........................... 86
Jedwali 68: Matumizi yaliyolipiwa kwenye vifungu visivyohusika ............ 86
Jedwali 69: Malipo yenye hati pungufu ...................................................... 87
Jedwali 70: Hati za Malipo zilizokosekana ................................................ 87
Jedwali 71: Masurufu yasiyorejeshwa ......................................................... 88
Jedwali 72: Matumizi yenye nyaraka pungufu ............................................ 90
Jedwali 73: Matumizi yasiyokubalika ......................................................... 91
Jedwali 74: Manunuzi yaliyofanywa bila idhini ya Bodi za Zabuni ......... 93
Jedwali 75: Ununuzi wa mali toka kwa wauzaji binafsi bila kibali cha Bodi ya Zabuni ....................................................................... 94
Jedwali 76: Manunuzi yaliyofanywa bila kushindanisha Wazabuni ............ 94
Jedwali 77: Mali na vifaa ambavyo havikuingizwa kwenye daftari ............ 95
Jedwali 78 : Mali na Vifaa Vilivyonunuliwa lakini Havikupokelewa .......... 96
Jedwali 79: Mafuta yaliyotumika bila kuonyeshwa katika leja za magari ... 96
Jedwali 80: Manunuzi ya bidhaa na huduma bila idhini ya Bodi za Zabuni ............................................................................ 97
Jedwali 81: Ununuzi wa mali toka kwa wauzaji binafsi bila kibali cha Bodi za Zabuni ...................................................................... 98
Jedwali 82: Manunuzi ya vifaa na bidhaa yaliyofanywa bila kushindanisha wazabuni ........................................................... 99
Jedwali 83: Manunuzi ya mali na vifaa bila kuingizwa kwenye daftari ..... 100
Jedwali 84: Mali na Vifaa Vilivyonunuliwa lakini havijapokelewa ........... 101
Jedwali 85: Manunuzi ya huduma na vifaa yaliyofanywa kwa fedha taslimu ........................................................................ 102
Jedwali 86:Jedwali 86: Manunuzi yaliyofanywa bila ushindanishi wa bei 103
Jedwali 87: Vifaa ambavyo havikuingizwa kwenye leja ............................ 103
Jedwali 88: Vifaa ambavyo havijaingizwa kwenye vitabu ......................... 104
Jedwali 89:Jedwali: Manunuzi kutoka kwa wasambazaji wasioidhinishwa ......................................................................... 105
Jedwali 90: Manunuzi yasiyokuwepo kwenye mpango wa manunuzi wa mwaka ........................................................................................ 106
Jedwali 91: Zabuni zilizotolewa bila kutangazwa ..................................... 106
Jedwali 92: Miradi kamilifu isiyokuwa na tija ........................................... 106
Jedwali 93: Mikataba iliyotolewa bila kibali cha Bodi za Zabuni .............. 107
Jedwali 94:Vifaa visivyo ingizwa kwenye leja ........................................... 108
Jedwali 95: Tozo ya riba kwa kuchelewesha malipo ya wakandarasi ........ 109

## Orodha ya Michoro

Mchoro 1: Mchango Kutoka kwa Washirika wa Maendeleo .................. 65

## Vifupisho

| | |
|---|---|
| **ADF** | Mfuko Wa Maendeleo Afrika |
| **AfDB** | Bank ya Maendeleo ya Afrika |
| **AFS&C** | Kilimo Chakula na Ushirika |
| **ASDP** | Mradi wa Maendeleo ya Sekta ya Kilimo |
| **ASDS** | Mkakati wa Maendeleo ya Sekta ya Kilimo |
| **ASLMS** | Wizara zinazojihusisha katika sekta ya Kilimo |
| **CAATs** | Mbinu za ukaguzi zinazotekelezwa kwa kutumia Tekinolojia ya Komputa |
| **CAG** | Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali |
| **CC** | Halmashauri ya Mji |
| **CCHP** | Mpango wa Afya |
| **DADPs** | Mipango ya Maendeleo ya Kilimo katika Wilaya |
| **PPA** | Sheria ya Ununuzi wa Umma Na. 21 ya mwaka 2004 |
| **PPRA** | Mamlaka ya kusimamia Ununuzi wa umma |
| **RWBO** | Shirika la Maji Bonde la Rufiji |
| **DANIDA** | Shirika la kimataifa la Maendeleo la Denmark |
| **DIT** | Chuo cha Technologia cha Dar es Salaam |
| **EU** | Jumuia ya Umoja wa Ulaya |
| **HBF** | Mfuko wa Uchangiaji Sekta ya Afya |
| **IA** | Shirirka la Msaada la Nchi ya Ireland |
| **IDA** | Shirika la kimataifa la Maendeleo |
| **IFAD** | Mfuko wa kimataifa kwa Maedeleo ya Kilimo |
| **IPSAS** | Viwango vya kimataifa vya ukaguzi katika sekta ya umma |
| **ISA** | Viwango vya kimataifa vya ukaguzi |
| **ISSAIs** | Viwango vya kimataifa vya ukaguzi vya Ofisi za ukaguzi wa Umma |
| **JICA** | Shirika la Maendeleo la nchi ya Japan |
| **LGAs** | Mamlaka za Serikali za Mitaa |
| **MDAs** | Wizara, Idara na Wakala |
| **MKUKUTA** | Mpango wa Kupunguza na Kuondoa Umaskini Tanzania |
| **MoU** | Mkataba wa Makubaliano |
| **MoW** | Wizara ya Maji |
| **MSD** | Bohari Kuu ya dawa |
| **MTEF** | Mwongozo wa Matumizi |
| **NAO** | Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi |
| **NBAA** | Bodi ya Taifa ya Wahasibu na wakaguzi wa hesabu |

| | |
|---|---|
| **NVF** | Mfuko waTaifa wa Fedha kwa ajili ya Vijiji |
| **PFGAs** | Vikundi shirikishi vya wakulima |
| **PFMRP** | Mradi wa maboresho ya usimamizi wa fedha za umma |
| **PFR** | Kanuni za fedha za umma |
| **PMG** | Mlipaji Mkuu wa Serikali |
| **Sect.** | Kifungu |
| **SIDA** | Shirika la kimataifa la Maendeleo la Sweden |
| **SNAO** | Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ya Sweden |
| **TASAF** | Mfuko wa Maendeleo ya jamii Tanzania |
| **TMU** | Kitengo cha Uongozi wa Mfuko wa Maendeleo Jamii |
| **TPRS** | Mkakati wa Kupunguza Umaskini Tanzania |
| **TRA** | Mamlaka ya Mapato Tanzania |
| **URT** | Jamhuri ya Muugano waTanzania |
| **USD** | Dola ya Kimarekani |
| **VFC** | Mratibu wa Fedha wa Kijiji |
| **WSDP** | Programu ya maendeleo ya sekta ya maji |

## Dibaji

Ripoti hii ni majumuisho ya matokeo ya kaguzi za miradi inayofadhiliwa na wahisani na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Miradi ipo katika makundi mawili ambayo ni miradi mikubwa minne na mingineyo kama inavyoonekana hapa chini:

- Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF)
- Mradi wa Maendeleo wa Sekta ya Kilimo (ASDP)
- Mradi wa Maendeleo wa Sekta ya Maji (WSDP)
- Mfuko wa Sekta ya Afya (HBF)

Pamoja na kaguzi za miradi ambayo washirika wa maendeleo wanachangia kwa pamoja (Basket Funds), pia nilikagua miradi mingine ambayo ni ya makubaliano kati ya Serikali na wahisani wengine.

Ripoti hii ya Ukaguzi inawasilishwa kwa Mheshimiwa Rais kwa mujibu wa Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 (ilivyorekebishwa 2005) na Kifungu 34(1) & (2) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na.11 ya mwaka 2008.

Kwa mujibu wa Ibara 143(2) (c) Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anatakiwa angalau mara moja kila mwaka kufanya ukaguzi na kutoa taarifa ya ukaguzi kwa Hesabu za Serikali ya Jamhuri ya Muungano, hesabu zinazosimamiwa na watumishi wote wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano, hesabu za Mahakama zote za Jamhuri ya Muungano na hesabu zinazosimamiwa na Katibu wa Bunge.

Ibara ya 143(4) inamtaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuwasilisha kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ripoti yoyote anayotayarisha kuhusu hesabu za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (2) cha Katiba. Mara baada ya kupokea taarifa hiyo Rais atawaagiza watu wanaohusika wawasilishe taarifa hiyo kwenye kikao cha kwanza cha Bunge kitakachofanyika baada

ya Rais kupokea taarifa hiyo na itabidi iwasilishwe katika kikao hicho kabla ya kupita siku saba tangu siku ile kilipoanza kikao hicho cha Bunge.

Kutungwa kwa Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na.11 ya mwaka 2008 kumeimarisha uhuru wa Ofisi yangu katika kutimiza jukumu lake Kikatiba. Haya ni matokeo ya jitihada za Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Bunge letu tukufu.

Uhuru wa kiutendaji wa ofisi yangu utawezesha kusimamia rasilimali za ofisi zilizopo zikijumuisha rasilimali watu na fedha ambazo zitawezesha ofisi yangu kutimiza majukumu yake bila kuingiliwa na mtu au mamlaka yoyote.

Sheria imeongeza mawanda ya ukaguzi wetu kwa kunipa madaraka ya kufanya kaguzi zingine zaidi ya ukaguzi wa kawaida wa taarifa za fedha ambazo ni ukaguzi wa ufanisi, utambuzi, mazingira na kaguzi maalum. Ni matumaini yangu kwamba, kwa kuanzishwa kwa Sheria mpya ya Ukaguzi wa Umma, Ofisi yangu imeweza kuimarisha udhibiti wa fedha na kuisaidia Serikali kuimarisha uwajibikaji. Kwa hiyo, Sheria inaniwezesha kuwa huru na kulihakikishia Bunge masuala yanayohusu uwajibikaji, uwazi na matumizi bora ya rasilimali hasa kuona kwamba rasilimali hizo zimetumika vizuri kwa kuzingatia uchumi, ufanisi na kama ilivyotarajiwa na kupitishwa na Bunge.

Ni vyema kutambua kuwa wakati Ofisi yangu inatoa taarifa kuhusu ukiukwaji wa sheria, taratibu na kanuni mbalimbali na udhaifu katika mifumo ya udhibiti wa ndani kwenye taasisi za umma na hasa miradi ya maendeleo, wajibu wa kuhakikisha kuwepo kwa mifumo thabiti ya udhibiti wa ndani ni jukumu la Maafisa Masuuli.

Matarajio ya Bunge na Umma ni kuona kwamba Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wanawahakikishia utoaji wa taarifa za fedha na usimamizi wa rasilimali katika miradi ya maendeleo zina ufanisi na ubora katika usimamizi wa mipango iliyowekwa. Kwa njia ya ukaguzi, ofisi inachangia katika kutoa mapendekezo yatakayoboresha utendaji katika sekta ya

Umma. Kwa msingi huu, Serikali Kuu, Ofisi yangu na washirika wa maendeleo wana mchango mkubwa wa kutoa kwa Bunge katika kujenga imani kwa umma katika usimamizi wa rasilimali za Umma. Ingawa majukumu yanatofautiana, matarajio ya usimamizi bora wa rasilimali yanafanana.

Ili kukidhi matarajio ya wabunge na yale ya umma kwa mapana zaidi, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi imeendelea kufanya uchambuzi wa njia bora zaidi za kufanya ukaguzi na kuongeza wigo wa masuala yanayokaguliwa na hivyo kuimarisha utendaji wa uwajibikaji katika sekta ya umma inayopokea fedha toka kwa washirika wa maendeleo. Aidha, tunahakikisha ukaguzi wetu unalenga na kuyapa kipaumbele maeneo muhimu ili kuchangia katika usimamizi wa fedha katika sekta ya umma. Kwa kuwa kazi ya ukaguzi ni chachu katika usimamizi wa fedha, tunaendelea kujadiliana na wadau kuhusu masuala yanayoibuka na maendeleo na kuona athari katika sekta ya umma, hasa katika utoaji wa taarifa za usimamizi wa fedha na masuala ya utawala bora.

Natarajia kuwa Bunge, Washirika wa Maendeleo na Umma kwa ujumla utaona taarifa hii kuwa ni muhimu katika kuiwajibisha Serikali kwa jukumu lake la usimamizi na kutoa huduma bora zaidi kwa fedha zinazotolewa na washirika wa maendeleo na utoaji wa huduma bora kwa Watanzania.

Hivyo, nitafurahi kupata taarifa ya jinsi gani nitaweza kuboresha taarifa yangu hii kwa siku zijazo.



Ludovick S. L. Utouh
**MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI**

---

Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi,
**Dar es Salaam,**

**Machi, 2014**

# SHUKRANI

Napenda kutoa shukrani za dhati kwa wote walioniwezesha kutekeleza majukumu yangu ya kikatiba.

Natoa shukrani za dhati kwa wadau wetu ambao ni Mlipaji Mkuu wa Serikali, Hazina, Maafisa Masuuli wote wa Wizara, Idara na Wakala wa Serikali (MDAs) na Mamlaka za Serikali za Mitaa (LGAs) wanaosimamia miradi inayofadhiliwa na Wahisani kwa kutoa ushirikiano na kutoa taarifa muhimu zinazohitajika sana katika utayarishaji wa ripoti hii.

Aidha, natoa shukrani zangu za dhati kwa wafadhili hasa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ya Sweden, Serikali ya Sweden kupitia Shirika la Kimataifa la Misaada ya Maendeleo la Sida, Ofisi ya Ukaguzi ya Ujerumani, Serikali ya Ujerumani kupitia Shirika la Kimataifa la Misaada ya Maendeleo la GIZ, Benki ya Dunia kupitia Mradi wa Kusimamia na Kuboresha Sekta ya Fedha za Umma (PFMRP) na wote wenye mapenzi mema ambao wamechangia kwa kiasi kikubwa kuboresha Ofisi yangu. Mchango wao umekuwa na manufaa makubwa katika kuendeleza na kukuza rasilimali watu, nyenzo za kazi (magari), mifumo ya teknolojia ya mawasiliano na vitendea kazi. Bado tunahitaji msaada zaidi katika kuboresha ukaguzi katika sekta ya umma ambao ungeweza kuharakishwa kama tungepata wafadhili wenye nia ya kutoa fedha za ujenzi wa chuo cha mafunzo ya ukaguzi kinachotarajiwa kujengwa Gezaulole-Kigamboni.

Aidha, nawashukuru watumishi wote wa umma popote pale walipo hapa Tanzania wawe ni wa Serikali Kuu au Serikali za Mitaa bila ya kuwasahau walipa kodi ambao ndio walengwa wa ripoti hii. Michango yao imekuwa msaada mkubwa katika ujenzi wa Taifa ambao hauwezi kupuuzwa hata kidogo.

Ninapenda kutambua utaalamu na kujituma kwa watumishi wa Ofisi yangu katika kufikia malengo ya kazi yaliyowekwa ingawa walitimiza hayo katika mazingira magumu yakiwemo ukosefu wa fedha, vitendea kazi, mishahara midogo na kufanya kazi kwenye maeneo yasiyofikika kirahisi.

Napenda kutoa shukrani zangu kwa wafanyakazi wote wa Ofisi yangu kwa kuniwezesha kutimiza majukumu yangu kikatiba. Ninawajibika kutoa shukrani zangu za pekee kwa familia yangu na familia za wafanyakazi wa Ofisi yangu kwa kutuvumilia kwa kutokuwa nao kwa muda mrefu wakati tukikamilisha majukumu haya ya kikatiba.

Mwisho, natoa shukrani zangu kwa Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali kwa kuniwezesha kutoa ripoti kwa wakati.

Naomba Mungu awabariki wote wakati tukitimiza wajibu wetu katika uwajibikaji na utawala bora kwa kutumia vyema rasilimali za umma.

## MUHTASARI WA MAMBO MUHIMU KATIKA RIPOTI YA UKAGUZI WA TAARIFA ZA FEDHA ZA MIRADI INAYOFADHILIWA NA WASHIRIKA WA MAENDELEO KWA MWAKA 2012/2013

Ripoti hii ya miradi inayofadhiliwa na washirika wa mendeleo imegawanyika katika maeneo yafuatayo:

A. Utangulizi
B. Hati za ukaguzi zilizotolewa
C. Utekelezaji wa mapendekezo katika ripoti za kaguzi za miaka ya nyuma.
D. Uwasilishaji na uchambuzi wa matokeo ya ukaguzi pamoja na utendaji wa miradi mikubwa na miradi mingine
E. Mapungufu katika usimamizi wa fedha na rasilimali watu
F. Mapungufu katika mchakato wa manunuzi
G. Matokeo ya ukaguzi maalum
H. Hitimisho na mapendekezo

### A: Utangulizi

Sehemu hii inaeleza kwa muhtasari matokeo ya ukaguzi wa taarifa za fedha katika miradi inayofadhiliwa na washirika wa maendeleo kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2013. Mawanda ya ukaguzi katika miradi inayofadhiliwa na wahisani yanajumuisha Mradi wa Maendeleo ya Sekta ya Maji (WSDP), Mradi wa Maendeleo ya Sekta ya Kilimo (ASDP), Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), Mfuko wa Uchangiaji wa Sekta ya Afya (HBF) na miradi mingine.

Muhtasari wa mambo muhimu yaliyotokana na ukaguzi yameonyeshwa katika taarifa ya jumla aidha taarifa kamili zilipelekwa kwa uongozi wa kila mkaguliwa anayesimamia utekelezaji wa mradi na wadau wengine wanaohusika na miradi.

## B: Hati za Ukaguzi Zilizotolewa

Matokeo ya ukaguzi wa miradi inayofadhiliwa na wahisani kwa mwaka wa fedha wa 2012/13 ni kama yanavyoonekana katika jedwali namba 1 hapa chini:-

**Jedwali 1: Mchanganuo wa hati za ukaguzi zilizotolewa**

| Mradi | Hati zinazoridhisha | % | Hati zenye Shaka | % | Hati zisizoridhisha | % | Hati mbaya | % | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| TASAF | 95 | 86.4 | 13 | 11.8 | - | 0 | 2 | 1.8 | 110 |
| ASDP | 111 | 83.5 | 20 | 15.0 | 1 | 0.7 | 1 | 0.8 | 133 |
| WSDP | 119 | 88.8 | 11 | 8.2 | 3 | 2.2 | 1 | 0.7 | 134 |
| HBF | 103 | 78.0 | 26 | 19.7 | 2 | 1.5 | 1 | 0.8 | 132 |
| **Jumla ndogo** | **428** | | **70** | | **6** | | **5** | | **509** |
| Miradi Mingine | 99 | 97.1 | 3 | 2.9 | 0 | | 0 | | 102 |
| **Jumla Kuu** | **527** | **86.3** | **73** | **11.9** | **6** | **1.0** | **5** | **0.8** | **611** |

Kwa ujumla kati ya miradi 611 iliyokaguliwa, asilimia 86.3 ilipata hati zinazoridhisha, asilimia 11.9 ilipata hati yenye shaka asilimia 1 hati zisizoridhisha na asilimia 0.8 ilipata hati mbaya.

Mwelekeo wa maoni ya ukaguzi wa miradi na hati zilizotolewa kwa kipindi cha miaka mitatu ni kama ulivyoonyeshwa katika jedwali namba 2 hapa chini:

**Jedwali 2: Mwenendo wa hati za Ukaguzi wa miradi**

| Hati | 2012/13 | % | 2011/12 | % | 2010/11 | % |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Hati zinazoridhisha | 527 | 86.3 | 497 | 80.8 | 484 | 83.4 |
| Hati zenye Shaka | 73 | 11.9 | 117 | 19 | 92 | 16 |
| Hati zisizoridhisha | 6 | 1 | 1 | 0.2 | 2 | 0.3 |
| Hati mbaya | 5 | 0.8 | 0 | 0 | 2 | 0.3 |
| Jumla | 611 | 100 | 615 | 100 | 580 | 100 |

Idadi ya hati zinazoridhisha imepungua kwa asilimia 2.6 kutoka mwaka 2010/11 hadi 2011/12 na kuongezeka kwa asilimia 5.5 kutoka mwaka 2011/12 hadi 2012/13.

Idadi ya hati zenye shaka imeongezeka kwa asilimia 3 kutoka mwaka 2010/11 hadi 2011/12 na kupungua kwa asilimia 7.1 kutoka mwaka 2011/12 hadi 2012/13.

Idadi ya hati zisizoridhisha imepungua kwa asilimia 0.1 kutoka mwaka 2010/11 hadi 2011/12 na kuongezeka kwa asilimia 0.8 kutoka mwaka 2011/12 hadi 2012/13.

Idadi ya hati mbaya imepungua kwa asilimia 0.3 kutoka mwaka 2010/11 hadi 2011/12 na kuongezeka kwa asilimia 0.8 kutoka mwaka 2011/12 hadi 2012/13.

**C: Utekelezaji wa mapendekezo katika ripoti za kaguzi za miaka ya nyuma**

Sehemu hii inatoa kwa ufupi taarifa ya utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa katika ripoti za kaguzi za miaka ya nyuma kwa maafisa masuuli pamoja na mchanganuo wa fedha, na hoja za Ukaguzi zilizohojiwa mwaka 2012/13.

Hoja za Ukaguzi wa miaka ya nyuma ambazo mapendekezo yaliyotolewa hayajatekelezwa kwa mwaka 2010/11 ni masuala yenye thamani ya Sh.106,707,796,940; mwaka wa 2011/12 ni Sh.20,289,040,011 na mwaka 2012/13 ni Sh.129,329,551,647.

**D: Utendaji wa Miradi Mikubwa na Miradi Mingine**

Sura hii inaonyesha kwa ufupi taarifa ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ikiainisha vyanzo vya fedha, taarifa za matumizi na salio lililobaki bila ya kutumiwa kwa kila mradi hadi kufikia mwisho wa mwaka wa fedha.

Ukaguzi ulifanya tathmini endapo fedha za miradi zimetumika kwa ajili ya malengo yaliyokusudiwa na kutambua mchango wake katika kukuza uchumi na maendeleo ya wananchi. Hii ilijumuisha changamoto zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wa shughuli za miradi na endapo ufanisi katika matumizi ya fedha umefikiwa.

Mchanganuo wa taarifa za fedha za miradi ni kama ulivyoonyeshwa katika jedwali Na.3 hapa chini:

## Jedwali 3: Mchanganuo wa fedha za Miradi

| Mradi | Salio Anzia | Fedha zilizopokelewa | Jumla ya Fedha | Matumizi | Salio Ishia |
|---|---|---|---|---|---|
| | (Sh.) | (Sh.) | (Sh.) | (Sh.) | (Sh.) |
| TASAF | 6,121,150,154 | 23,044,105,997 | 29,165,256,151 | 26,233,530,165 | 2,931,725,987 |
| ASDP | 33,606,929,981 | 22,450,635,301 | 56,057,565,282 | 41,278,807,664 | 14,778,757,618 |
| WSDP | 223,068,169,733 | 404,142,527,760 | 627,210,697,493 | 348,887,313,110 | 278,323,384,383 |
| HBF | 12,802,980,024 | 167,072,333,709 | 179,875,313,733 | 145,960,038,904 | 33,915,274,829 |
| **Jumla** | **275,599,229,892** | **616,709,602,767** | **892,308,832,658** | **562,359,689,844** | **329,949,142,816** |

## E: Mapungufu katika Usimamizi wa Fedha na Rasilimali Watu

Sura hii imekusudia kutoa taarifa zinazohusiana na mapungufu yaliyoonekana katika usimamizi wa fedha na rasilimali watu. Hata hivyo, kasoro zinazotokana na usimamizi wa fedha usioridhisha zimekuwa zikiongezeka kwani katika mwaka wa fedha 2010/11 mapungufu yalikuwa na thamani ya Sh.3,784,613,760, mwaka 2011/12 ni Sh.5,036,540,269 na mwaka 2012/13 ni Sh.18,775,777,298 na USD 3,391,816.

Kadhalika, tatizo la upungufu wa watumishi katika utekelezaji wa shughuli za miradi limekuwa ni kubwa katika Serikali za Mitaa kwani kwa mwaka wa fedha 2011/12 kulikuwa na upungufu wa watumishi 14,663 na mwaka 2012/13 upungufu ni watumishi 20,215.

## F: Mapungufu katika Mchakato wa Manunuzi

Katika barua zilizowasilishwa kwa kila Afisa Masuuli, nilitoa taarifa kwamba, miradi karibu yote mikubwa haikufuata kikamilifu Sheria ya Manunuzi ya Umma Na. 21 ya 2004 na kanuni zake za mwaka 2005.

Mashaka yangu ni kiwango cha watendaji kuelewa Sheria ya Manunuzi ya Umma na Kanuni zake. Tatizo hili bado lipo kama ilivyoonekana katika ukaguzi wa mwaka 2012/13 ambapo kulikuwa na Sh.32,323,051,169 na USD 114,806, ukilinganisha na Sh.1,375,404,672 na Sh.39,461,168,319 kwa miaka ya 2010/11 na 2011/12.

## G: Matokeo ya Ukaguzi Maalum

Matokeo ya Ukaguzi maalum ulibainisha mapungufu mbalimbali katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kasoro zilizoonekana ni kama zilivyoonyeshwa hapa chini:

**(i) Mfuko wa Afya**

Ukaguzi Maalum wa Mfuko wa Afya ulijumuisha halmashauri kumi na nne (14) ambazo zilichaguliwa kwa kuzingatia taarifa zilizoandaliwa kwa mujibu wa Mpango Kabambe wa Afya wa Halmashauri (CCHP) kwa mwaka 2011/12. Kati ya halmashauri hizo, 4 zilichaguliwa kutoka katika halmashauri zilizofanya vizuri, 6 kutoka katika halmashauri ambazo hazikufanya vizuri na 4 zilichaguliwa na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii. Orodha ya halmashauri hizi imeonyeshwa katika Sura ya Saba ya ripoti hii na mapungufu yaliyoonekana ni kama yalivyoonyeshwa hapa chini:

- Kanuni elekezi iliyotumika katika kukokotoa mgawanyo wa fedha zinazokwenda halmashauri haikufanyiwa mapitio ambayo yanahusiana na mabadiliko ya idadi ya watu, vifo chini ya miaka mitano (5), takwimu za umasikini na mwelekeo wa masuala ya afya katika wilaya.
- Kumekuwa na ucheleweshwaji wa fedha zinazopelekwa katika halmashauri kutoka Hazina. Ucheleweshwaji huo unakadiriwa kuchukua takriban siku 4 hadi 44.
- Baadhi ya washirika wa miradi ya maendeleo hawakutekeleza ahadi zao za utoaji fedha kama ilivyoafikiwa katika mkataba wa makubaliano ya mwaka 2010/11.
- Jukumu la kusimamia utekelezwaji wa miradi halikutekelezwa ipasavyo na kamati za afya za mikoa na (RHMT) na Ofisi ya Waziri Mkuu – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI). TAMISEMI imeshindwa kuzisimamia vizuri ofisi za makatibu tawala wa mikoa na serikali za mitaa katika kutathmini utekelezwaji wa mpango kabambe wa afya na ufuatiliaji wa mapendekezo ya ukaguzi yaliyotolewa kwa mfuko wa afya. Aidha, vikao vya mwaka vinavyowahusisha waganga wakuu wa mikoa na wilaya ili kupanga mikakati madhubuti ya utekelezaji na kutoa dira katika mchakato wa kuboresha sekta ya afya havikufanyika.

(ii) **Miradi inayofadhiliwa na Shirika la Kimataifa la Maendeleo Denmark – (PFM na SWMP)**

(a) **Mradi shirikishi wa Usimamizi wa Misitu (PFM)**

Ukaguzi maalum katika Mradi Shirikishi wa Usimamizi wa Misitu ulihusisha halmashauri kumi na moja (11), Ofisi za Katibu Tawala mbili-Mkoa wa Lindi na Iringa, Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania (TAFORI) na Wizara ya Maliasili na Utalii kitengo cha Misitu na Ufugaji Nyuki. Muhtasari wa dosari zilizoonekana ni kama ilivyoonyeshwa hapa chini:

- Kinyume na kanuni Na. 68(5) ya Sheria ya Manunuzi ya Umma ya 2004, halmashauri mbili zilinunua bidhaa, vifaa na huduma za gharama ya Sh.19,242,500 kutoka kwa wazabuni wasioorodheshwa na kupitishwa na Wakala wa Manunuzi wa Umma (GPSA) wala Bodi ya Zabuni za Halmashauri husika.

- Bidhaa zenye thamani ya Sh.13,355,534 zilinunuliwa na Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa na Ofisi ya Katibu Tawala - Mkoa wa Iringa bila kushindanisha wazabuni kinyume na Kanuni Na.68(4) ya Sheria ya Manunuzi ya Umma, 2004.

- Kiasi cha Sh.36,454,000 kilihamishwa kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Chunya kwenda katika akaunti ya mavuno (Mapogoro Akaunti namba 6076600076), hata hivyo, menejimenti haikuwasilisha kwa ajili ya Ukaguzi nyaraka na vielelezo vinanyohusiana na uhamishaji wa fedha hizo kinyume na kifungu Na. 5.7 cha Mwongozo wa Fedha na Kanuni namba 138 ya Sheria ya fedha ya mwaka 2001 (ilivyorekebishwa 2004).

- Kiasi cha Sh.48,070,000 kilitumika katika matumizi ambayo hayahusiani na malengo ya miradi. Halmashauri mbili (2) pamoja na Ofisi ya Katibu Tawala - Mkoa wa Iringa zilibainika kutumia fedha hizi kwa malengo yasiyokusudiwa.

b) **Mradi Endelevu wa Eneo Oevu – (SWMP)**
Ukaguzi maalum ulifanyika katika halmashauri tisa (9), Ofisi ya Katibu Tawala - Mkoa wa Iringa na Ofisi ya Waziri Mkuu – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa mwaka 2012/13 na mapungufu yafuatayo yalionekana:

- Malipo ya Sh.23,929,950 yalilipwa na halmashauri tano (5) bila ya nyaraka za kutosha kinyume na Kanuni Na.138 ya Sheria ya Fedha 2001(ilivyorekebishwa 2004).

- Taarifa za matumizi za Halmashauri ya Wilaya ya Iringa na Ofisi ya Katibu Tawala - Mkoa wa Iringa hazikuainisha vifungu vilivyotumika vikionyesha bajeti ya kila kifungu cha mradi.

- Halmashauri tano (5) zilitumia Sh.15,301,600 zaidi ya kiasi kilichoidhinishwa katika bajeti ya mradi kinyume na Agizo Na.23(1) la Memoranda ya Fedha Serikali za Mitaa, 2009.

## H: Hitimisho na Mapendekezo

Mwisho, mamlaka niliyopewa kwa mujibu wa kifungu cha 10 cha Sheria ya Ukaguzi Na.11 ya mwaka 2008, nimetoa mapendekezo kadhaa kwenye Sura ya Nane (8) ya ripoti hii, ambayo kama yatatekelezwa, ninaamini yatachangia katika kuboresha usimamizi wa miradi ya maendeleo inayofadhiliwa na wahisani nchini.

### Hitimisho

- Maafisa masuuli hawatoi umuhimu wa kutosha kusimamia na kushughulikia miradi na hasa mapendekezo na masuala yaliyohojiwa na wakaguzi. Hii inatokana na ushahidi kwamba, bado kuna masuala na mapendekezo yasiyojibiwa ya Sh.129,329,551,647 katika mwaka 2012/13 ikilinganishwa na Sh.20,289,040,011 kwa mwaka 2011/12 na Sh.106,707,796,940 kwa mwaka 2010/11.
- Kumekuwa na tatizo kubwa la kutofuata matakwa ya vipengele vilivyoainishwa katika mkataba wa makubaliano ya utekelezaji wa miradi inayofadhiliwa na wahisani ambavyo vinasisitiza juu ya umuhimu wa kutii na kuzifuata

sheria na taratibu za fedha na manunuzi za Tanzania. Kwa ukaguzi wa mwaka huu kasoro zimebainika katika masuala ya manunuzi yenye thamani ya Sh.32,031,551,169 na USD 114,806; na kasoro zimeonekana katika usimamizi wa fedha zenye thamani ya Sh.18,775,777,298 na USD 3,391,816.

- Kumekuwa na ucheleweshwaji wa utoaji wa fedha kutoka kwa washirika wa maendeleo na Hazina kwenda kwa watekelezaji wa miradi. Hii imechangia kukwamisha juhudi za utekelezaji wa miradi na kusababisha kuwepo kwa bakaa kubwa za fedha ambazo hazikutumika hadi kufika mwisho wa mwaka. Kwa mwaka 2012/13 kulikuwa bakaa ya kiasi cha Sh.346,284,115,450 na USD 45,950,595, ukilinganisha na miaka ya nyuma ambapo kwa mwaka 2010/11 bakaa ilikuwa ni Sh.221,997,432,753 na USD 51,356,184 wakati mwaka 2011/12 bakaa ilikuwa ni Sh.299,852,509,319 na USD 213,520,573. Kwa mwelekeo huu sehemu kubwa ya miradi haitekelezwi katika mwaka ambao bajeti imepitishwa.

- Tatizo la upungufu wa watumishi bado limekuwa ni kikwazo katika mchakato wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo na hivyo linahitaji ufumbuzi wa kina unaotakiwa kufanywa na menejimenti za halmashauri. Katika mwaka 2012/13, upungufu wa watumishi ulikuwa ni 20,215 dhidi ya watumishi 41,043 waliotakiwa ukilinganisha na mwaka 2011/12 ambao kulikuwa na upungufu wa watumishi 14,663 dhidi ya idadi halisi ya watumishi waliokuwa wanahitajika ambao ni 73,087.

**Mapendekezo**

- Maafisa masuuli ambao ni wahusika katika usimamizi wa miradi inayofadhiliwa na washirika wa maendeleo waongeze juhudi katika kusimamia na kutekeleza mapendekezo ya ukaguzi yaliyotolewa miaka iliyopita ili kuepuka kujirudia kwa mapungufu na matatizo yaliyokwisha kuhojiwa na mapendekezo kutolewa.

- Maafisa masuuli wanatakiwa kuzingatia udhibiti wa bajeti juu ya matumizi ili kuhakikisha kuwa rasilimali zinatumika

katika ubora, ufanisi, kiuchumi na uwazi na matumizi yote yana kumbukumbu za kutosha ili kusaidia kutoa taarifa sahihi.

Lazima kuwe na udhibiti sahihi na ukaguzi wa awali wa matumizi ili kuzuia, kutambua, kuripoti na kukabiliana na malipo yasiyoidhinishwa, yasiyokuwa na nyaraka, yenye nyaraka pungufu na matumizi yasiyostahili.

- Washirika wa maendeleo, Wizara ya Fedha – (Hazina) na TAMISEMI wanatakiwa kuhakikisha kuwa fedha zilizotengwa na kuidhinishwa katika bajeti za miradi ya maendeleo zinapelekwa kwa wakati kwa ajili ya kusaidia utekelezaji wa shughuli zilizopangwa. Ucheleweshaji wa kupeleka fedha kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za miradi unakwamisha juhudi za kuyafikia malengo yaliyowekwa na hivyo kusababisha gharama kupanda kunakotokana na tatizo la ongezeko la bei.

- Rasilimali watu ni moja kati ya rasilimali muhimu katika taasisi, hivyo Maafisa Masuuli wanatakiwa kutoa vipaumbele katika kuhakikisha kuwa idadi ya watumishi wenye sifa wanapatikana kwa lengo la kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa shughuli za miradi ya maendeleo. Tunashauri Serikali za Mitaa zikisaidiana na TAMISEMI kuhakikisha kuna mpango endelevu wa kuboresha mahitaji ya watumishi utakaotoa nafasi za ajira zilizo wazi katika halmashauri, kwa lengo la kuongeza ufanisi wa utekelezaji wa miradi na hatimaye kutoa huduma stahiki kwa wananchi.

- Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii ikishirikiana na TAMISEMI ihakikishe kwamba ugawaji wa fedha, usambazaji wa dawa na vifaa vya afya unazingatia mahitaji halisi kuepuka kugawa zaidi au pungufu ya mahitaji ya wilaya. Hii italeta usawa na kuepukana na tatizo la kuwepo na dawa na vifaa visivyohitajika kwenye wilaya.

- Serikali Kuu ihakikishe inaongeza fedha za huduma za afya ilingane na majukumu ya halmashauri katika kutekeleza

Sera ya Taifa ya Afya ya Misamaha na Uchangiaji wa gharama.

- Menejimenti za halmashauri zihakikishe fedha zilizochanganywa katika akaunti moja zinatolewa mchanganuo kuonyesha mapato, matumizi na bakaa kwa kila mradi. Taarifa zihifadhiwe kwa kila mradi peke yake.

## SURA YA KWANZA

### 1.0 Utangulizi

Ripoti hii inatolewa kwa mara ya tatu kufuatia ukaguzi wa hesabu na nyaraka nyingine za miradi inayofadhiliwa na washirika wa maendeleo kwa mujibu wa Ibara ya 143(4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 (iliyorekebishwa 2005) kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2013.

Mwaka 2011/12 nilitoa tarifa yangu ya pili ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo kwa kutoa hoja na ripoti za ukaguzi kwa Maafisa Masuuli. Hivyo masuala ya miaka ya nyuma yasiyoshughulikiwa yanayohusu taarifa za ukaguzi nilizotoa kwa kila Afisa Masuuli anayehusika na miradi.

### 1.1 Mamlaka na Umuhimu wa Ukaguzi

Kutokana na Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ninapaswa kukagua kumbukumbu za taarifa zote za hesabu za fedha katika ofisi zote za Umma, Mahakama na Mamlaka zote za Serikali ya Jmhuri ya Muungano wa Tanzania ikiwamo miradi ya maendeleo na kutoa taarifa kwa Mheshimiwa Rais ambaye atahakikisha zinawasilishwa mbele ya Bunge.

Katika kutimiza wajibu huu, kutokana na Kifungu Na.10 cha Sheria Na. 11 ya Ukaguzi wa Umma ya mwaka 2008, ninatakiwa kujiridhisha kwamba:-

- Tahadhari inachukuliwa ili kuhakikisha kwamba fedha za miradi ya maendeleo zinakusanywa na kutunzwa kwa mujibu wa sheria na miongozo iliyowekwa.

- Fedha zote zinazotolewa kwa ajili ya miradi ya maendeleo zinatumiwa kulingana na malengo yaliyokusudiwa na mamlaka husika na kwa mujibu wa sheria na kanuni za fedha na ugavi.

Aidha, kutokana na kifungu kilichotajwa hapo juu ninawajibika kumtanabaisha Rais na Bunge juu ya uwepo wa matumizi mabaya ya fedha na mali za Umma.

## 1.2 Majukumu na wajibu wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Miradi ya Maendeleo

Wajibu wangu kama Mkaguzi Mkuu ni kutoa hati ya ukaguzi kuhusu hesabu za fedha zilizoandaliwa na maafisa masuuli. Nilifanya ukaguzi kulingana na viwango vya kimataifa vinavyosimamia ukaguzi katika taasisi za umma za Ukaguzi (ISSAIs) mkataba wa makubaliano na taratibu nyingine nilizoona zinafaa.

Zaidi ya hayo, imebainishwa chini ya Kifungu Na. 10(1) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na.11 ya mwaka 2008, inanitaka nijiridhishe kuwa taarifa za hesabu zimeandaliwa kwa misingi ya viwango vya kihasibu, na tahadhari za kutosha zimechukuliwa kulinda ukusanyaji wa mapato, stakabadhi, uhifadhi na utunzaji wa mali ya umma; ni wajibu kuona kuwa sheria, maelekezo na maagizo yanafuatwa katika matumizi ya umma na kwamba yameidhinishwa ipasavyo.

Kifungu 44(2) cha Sheria ya Manunuzi ya Umma Na.21 ya 2004 na Kanuni Na. 31 ya Manunuzi ya Umma (bidhaa, ujenzi, huduma zisizo za ushauri na uuzaji wa mali ya umma kwa zabuni) ya mwaka 2005, inanitaka nitoe katika ripoti yangu tathmini kama hesabu nilizokagua zinakidhi matakwa ya sheria na kanuni zake au la.

## 1.3 Muundo wa Kazi za Ukaguzi

Ripoti hii inatoa kwa muhtasari matokeo ya mwisho ya zoezi la ukaguzi ambalo lilifanywa na ofisi yangu nchini kote katika mwaka huu. Ili ofisi yangu iweze kushughulikia kikamilifu kazi hii kubwa ya kukagua miradi ya maendeleo, kuna ofisi katika wizara na mikoa yote Tanzania Bara ili kurahisisha utendaji.

**Majukumu na Maslahi ya Watumishi**

Ningependa kutambua juhudi za Serikali katika kuboresha hali za wafanyakazi katika Ofisi yangu ijapokuwa juhudi zaidi zinatakiwa kuboresha maslahi hayo yaendane na mazingira

halisi ya kazi inayofanywa. Muundo mpya wa Ofisi yangu ambao umepitishwa na Mh. Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Pia, nimewasilisha mapendekezo ya mishahara katika Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma kwa watumishi wa Ofisi yangu. Suala ya muundo na mishahara ni muhimu sana katika kuongeza uhuru wa wakaguzi mbali na kuongeza tija na ufanisi kwenye kazi zao.

Ili kuendelea na mwelekeo wa sasa, kazi za ukaguzi hazijajikita katika ukaguzi wa fedha na kufuata sheria tu. Kwa sasa ofisi yangu imepanua mawanda ya ukaguzi kwa kiasi kikubwa. Nia ya ofisi ni kupanua ofisi za ukaguzi hadi ngazi ya wilaya ambako fedha nyingi za maendeleo zinaelekezwa na Serikali na Wafadhili. Juhudi hizi zitahitaji Serikali kuridhia maombi ya mapendekezo ya marekebisho ya mishahara pamoja na kutenga bajeti kwa ajili ya upanuzi wa mawanda ya ukaguzi unaokusudiwa. Kuwepo kwa ofisi yangu katika ngazi ya wilaya kutaenda sawa na sera ya serikali ya maendeleo kwa wananchi ambapo fedha nyingi za maendeleo zinaelekezwa huko.

Kwa mwelekeo huu, kazi ya ukaguzi kwa sasa siyo ile ya kuangalia masuala ya fedha na utii wa sheria. Hivyo wakaguzi wanatakiwa kuwa na utaalamu kwenye masuala ya ukaguzi wa ufanisi, kiuchunguzi, mazingira, mikataba, jinsia, utawala, ukaguzi wa viashiria, mifumo ya kielektroniki/kitekinolojia na kwa sasa ukaguzi wa mafuta na gesi ili kuweza kufanya kazi zao kwa ufasaha katika kila nyanja. Ofisi yangu inajenga uwezo wa wakaguzi katika maeneo haya kwa kuzingatia uvumbuzi wa akiba ya gesi na uwezekano wa ugunduzi wa mafuta na umuhimu wake katika uchumi.

## 1.4 Mawanda na Viwango vya Ukaguzi vinavyotumika

### 1.4.1 Mawanda ya Ukaguzi

Mawanda ya ukaguzi yanahusisha maeneo hatarishi na matumizi sahihi yaliyoidhinishwa kutathmini utekelezaji wa miradi na kutembelea kujionea hali halisi.
Ukaguzi unafanyika ili kujiridhisha kwamba kulikuwepo na uzingatiaji wa kanuni zilizopo, kuongeza ufanisi na kupunguza gharama za uendeshaji.

Wakati wa ukaguzi kasoro zilizojitokeza zinawasilishwa kwa afisa masuuli anayehusika na utekelezaji wa mradi kupitia kikao cha kumaliza ukaguzi.

Maafisa masuuli wanapewa fursa ya kujibu hoja na kutekeleza mapendekezo na maoni ya ukaguzi; baada ya hapo masuala ambayo hayakupata ufumbuzi yanajumuishwa kwenye ripoti ya mwisho.

### 1.4.2 Viwango vya Ukaguzi Vinavyotumika

Nimefanya ukaguzi kwa kuzingatia viwango vya kimataifa vya taasisi za ukaguzi (ISSAIs) zinazotolewa na Taasisi ya Kimataifa inayojumuisha Asasi kuu za Ukaguzi wa Hesabu (INTOSAI) na taratibu nyingine nilizoona zinafaa kutokana na mazingira husika.

Viwango hivi vinanitaka kuandaa na kutekeleza ukaguzi wangu kwa nia ya kupata uhakika kwamba taarifa za hesabu zimetengenezwa kwa makini na ufanisi mkubwa.

## 1.5 Sera ya Kihasibu

Taarifa za fedha za miradi ya maendeleo hutayarishwa kulingana na mkataba wa makubaliano, kwa kuzingatia mifumo ya usimamizi wa fedha za umma nchini.

Kwa mujibu wa Kanuni Na. 53 ya Sheria ya Fedha 2001 (iliyorekebishwa 2004), Serikali imeweka taratibu za kihasibu ili kuhakikisha kwamba rasilimali zinazoidhinishwa na Bunge zinatumika kwa usahihi. Kwa mujibu wa Sheria ya Fedha Na.6 ya mwaka 2001 (iliyorekebishwa 2004), Maafisa Masuuli wanapaswa kuhakikisha kwamba mapato yote ya Umma yanaingizwa kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali. Pia malipo kutoka kwenye Mfuko huo yataidhinishwa kwa Sheria ya Bunge ya Matumizi kwa mwaka husika.

## 1.6 Kuandaa na Kuwasilisha Hesabu kwa ajili ya Ukaguzi

### 1.6.1 Wajibu wa Kisheria wa Wizara, Idara, Wakala na Sekretarieti za Mikoa

Maafisa Masuuli ni wasimamizi wa rasilimali za umma kwenye maeneo yao ya kazi kulingana na matakwa ya Kifungu Na.25(4) cha Sheria ya Fedha Na. 6 ya mwaka 2001

(iliyorekebishwa 2004). Katika kulinda rasilimali zilizo chini yao, suala la kuweka mifumo madhubuti na udhibiti wa ndani ni la umuhimu mkubwa. Ni wajibu wa uongozi wa wizara, idara na wakala kuhakikisha kwamba kumbukumbu za kihasibu za miradi zinatunzwa vizuri na kutoa uhakika wa taarifa za fedha, kulinda na kuhifadhi mali zote.

### 1.6.2 Majukumu ya Mamlaka za Serikali za Mitaa katika kuandaa taarifa za fedha

Pale ambapo halmashauri inapokea fedha kutoka kwa washirika wa maendeleo, jukumu la kutayarisha taarifa za fedha, linakuwa la menejimenti ya halmashauri kama ilivyofafanuliwa katika Agizo Na. 31(1) Memoranda ya Fedha za Serikali za Mitaa ya mwaka 2009 na mkataba wa makubaliano kati ya Serikali na Washirika wa Maendeleo.

Agizo Na.11 - 14 la LAFM, 2009 inaelekeza halmashauri kuweka mfumo wa udhibiti wa ndani wa rasilimali za serikali ikiwa ni pamoja na fedha za miradi ya maendeleo.

## 1.7 Mfumo wa Udhibiti wa Ndani

Mfumo wa udhibiti wa ndani ni utaratibu wa kuhakikisha malengo ya taasisi yanafikiwa kwa ufanisi na kutoa taarifa za fedha za kuaminika kwa kufuata sheria, kanuni na sera. Mfumo wa udhibiti wa ndani una jukumu kubwa katika kuzuia na kugundua ubadhirifu, matumizi mabaya na kulinda rasilimali za umma.

Kuweka na kusimamia mfumo thabiti wa udhibiti wa ndani ni jukumu la uongozi wa taasisi husika.

## SURA YA PILI

## MISINGI NA MWELEKEO WA HATI ZA UKAGUZI

### 2.0 Utangulizi

Lengo kuu la kufanya kaguzi mbalimbali ni kutoa maoni huru ya kitaalamu kama taarifa za fedha au tathmini zinaonyesha hali halisi ya mkaguliwa. Hati hizi hutolewa ili kumwezesha mtumiaji wa taarifa za fedha au tathmini kama hakikisho ili aweze kufikia maamuzi kutokana na matokeo ya ukaguzi uliofanywa.

Ushauri wa mkaguzi ni chombo muhimu wakati wa kutumia taarifa za fedha. Inakusudia kulishauri Bunge na watumiaji wengine wa taarifa za Wizara, Idara na Wakala kama taarifa za fedha zimetayarishwa kwa kuzingatia viwango vinavyokabilika vya kimataifa vya kuandaa taarifa za fedha katika sekta ya Umma na kwa namna inavyotakiwa chini ya Kifungu cha 25 (4) cha Sheria ya Fedha ya mwaka 2001 (ilivyorekebishwa 2004).

Ni muhimu kutambua kwamba hati ya ukaguzi inayotolewa kwa taarifa za fedha siyo hakikisho la moja kwa moja kwamba hali ya kifedha ya taasisi ni nzuri na sahihi kabisa kuweza kutegemewa katika kufanyia maamuzi. Hati ya ukaguzi ni maoni tu kwamba taarifa iliyowasilishwa ni sahihi na haina makosa makubwa ambapo maamuzi mengine huachiwa mtumiaji wa taarifa kuamua.

### 2.1 Aina ya Hati ya Ukaguzi

Kuna aina nne (4) za hati za ukaguzi, kila moja ikieleza mazingira tofauti anayokutana nayo mkaguzi. Hati hizo ni kama ifuatavyo:-

**(i) Hati inayoridhisha**

Aina hii ya hati hutolewa wakati taarifa za fedha zilizowasilishwa zinakuwa hazina makosa mengi na zimezingatia matakwa ya viwango vya uhasibu vilivyochaguliwa na kwa mujibu wa Sheria na Kanuni. Wakati mwingine hati hii huchukuliwa na wengi kama “hati safi”.

Katika mazingira fulani, hati ya ukaguzi inayoridhisha huweza kurekebishwa kwa kuongeza aya yenye masuala ya msisitizo. Kuongezwa kwa aya ya masuala ya msisitizo hakuathiri hati ya ukaguzi iliyotolewa. Madhumuni makubwa ya kuongeza masuala ya msisitizo ni kutoa uelewa zaidi kwa hali iliyotokea wakati wa ukaguzi licha ya kutolewa kwa hati ya ukaguzi inayoridhisha.

**(ii) Hati yenye Shaka**

Hali na mazingira yanayosababisha kutolewa kwa hati yenye shaka, huwa katika hali moja au zote zilizoorodheshwa hapa chini:

- Kunapokuwa na mashaka juu ya jambo fulani husababisha mkaguzi ashindwe kutoa maoni juu ya ukaguzi.
- Pale ambapo mkaguzi anapotoa maoni yanayotofautiana na hali halisi ya taarifa ya fedha zilizotolewa (kutokubaliana na taratibu kubalifu za utunzaji na uzingatiaji wa sheria na kanuni).

**(iii) Hati Isiyoridhisha**

Hati isiyoridhisha hutolewa inapogundulika kuwa taarifa za fedha kwa kiasi kikubwa si sahihi zinapoangaliwa katika ujumla wake; hazikuandaliwa kwa kuzingatia viwango vya Kimataifa vya Uhasibu, na kueleza kuwa taarifa zilizopo siyo sahihi na haziaminiki katika kupima matokeo ya uendeshaji.

Maelezo ya hati isiyoridhisha huwa wazi ambapo hueleza kwamba taarifa za fedha hazikuzingatia viwango vya Kimataifa vya Uhasibu.

**(iv) Hati Mbaya**

Hati mbaya inaweza kusababishwa na kukosekana kwa uhuru au ufinyu mkubwa wa mawanda ya ukaguzi ama kwa makusudi au la, mkaguliwa kukataa kutoa ushahidi na taarifa katika maeneo muhimu kwenye taarifa za fedha na panapokuwa na mashaka makubwa katika uendeshaji wa shughuli za mkaguliwa.

## 2.2 Mwelekeo wa hati za ukaguzi

(i) Jedwali namba 4 linaonyesha mwelekeo wa hati za ukaguzi zilizotolewa kwa miradi ya maendeleo kwa mwaka wa fedha 2012/2013.

**Jedwali 4: Mchanganuo wa hati za maoni ya ukaguzi zilizotolewa kwa kipindi cha 2012/13**

| Mradi | Hati zinazoridhisha | % | Hati zenye Shaka | % | Hati zisizoridhisha | % | Hati mbaya | % | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| TASAF | 95 | 86.4 | 13 | 11.8 | - | 0 | 2 | 1.8 | 110 |
| ASDP | 111 | 83.5 | 20 | 15 | 1 | 0.7 | 1 | 0.8 | 133 |
| WSDP | 119 | 88.8 | 11 | 8.2 | 3 | 2.2 | 1 | 0.7 | 134 |
| HBF | 103 | 78 | 26 | 19.7 | 2 | 1.5 | 1 | 0.8 | 132 |
| **Jumla ndogo** | **428** | | **70** | | **6** | | **5** | | **509** |
| Miradi Mingine | 99 | 97.1 | 3 | 2.9 | 0 | | 0 | | 102 |
| **Jumla Kuu** | **527** | **86.3** | **73** | **11.9** | **6** | **1** | **5** | **0.8** | **611** |

(ii) Mwelekeo wa hati za ukaguzi wa miradi zilizotolewa kwa kipindi cha miaka mitatu ni kama ulivyoonyeshwa katika jedwali namba 5 hapa chini:

**Jedwali 5: Mwelekeo wa hati za Ukaguzi wa miradi**

| Hati | 2012/13 | % | 2011/12 | % | 2010/11 | % |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Hati zinazoridhisha | 527 | 86.3 | 497 | 80.8 | 484 | 83.4 |
| Hati zenye shaka | 73 | 11.9 | 117 | 19 | 92 | 16 |
| Hati zisizoridhisha | 6 | 1 | 1 | 0.2 | 2 | 0.3 |
| Hati mbaya | 5 | 0.8 | 0 | 0 | 2 | 0.3 |
| **Jumla** | **611** | **100** | **615** | **100** | **580** | **100** |

Idadi ya hati zinazoridhisha imepungua kwa asilimia 2.6 kutoka mwaka 2010/11 hadi 2011/12 na kuongezeka kwa asilimia 5.5 kutoka mwaka 2011/12 hadi 2012/13.

Idadi ya hati zenye shaka imeongezeka kwa asilimia 3 kutoka mwaka 2010/11 hadi 2011/12 na kupungua kwa asilimia 7.1 kutoka mwaka 2011/12 hadi 2012/13.

Idadi ya hati zisizoridhisha imepungua kwa asilimia 0.1 kutoka mwaka 2010/11 hadi 2011/12 na kuongezeka kwa asilimia 0.8 kutoka mwaka 2011/12 hadi 2012/13.

Idadi ya hati mbaya imepungua kwa asilimia 0.3 kutoka mwaka 2010/11 hadi 2011/12 na kuongezeka kwa asilimia 0.8 kutoka mwaka 2011/12 hadi 2012/13.

## 2.3 Uwasilishaji na uchambuzi wa matokeo ya ukaguzi

Sehemu hii inatoa uchambuzi wa masuala yaliyosababisha kutoa hati aina fulani kwa hesabu za fedha za Washirika wa Maendeleo. Uchambuzi unalenga kuelezea misingi iliyotumika kufikia maamuzi ya kutoa aina moja au nyingine ya hati za ukaguzi.

Jumla ya miradi mia moja na sita (106) ilikaguliwa ikijumuisha watekelezaji (ikijumuisha halmashauri) wa miradi mikubwa minne (4) ya washirika wa miradi ya maendeleo kwa mwaka 2012/13 walikaguliwa pamoja na miradi mingine ya mfadhili mmoja mmoja mia moja na mbili (102). Hivyo basi ripoti mia sita na kumi na moja (611) za miradi zilitolewa kwa mwaka wa fedha 2012/13.

### 2.3.1 Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo

Serikali ya Tanzania ilianzisha mkakati wa maendeleo ya sekta ya kilimo (ASDS) ili kufikia malengo yenye mafanikio katika sekta ya kilimo. Programu ya maendeleo katika sekta ya kilimo (ASDP) ambayo ilianzishwa kwa pamoja na Wizara zinazoongoza sekta ya kilimo (ASLMs) inatoa mwongozo na mkakati wa kufanikisha utekelezaji wa maendeleo ya sekta ya kilimo (SDS). Shughuli za maendeleo katika ngazi za Wilaya hutekelezwa na mamlaka za Serikali za Mitaa (LGAs), kwa mujibu wa mpango wa maendeleo ya kilimo katika ngazi ya Wilaya (DADPs).

Serikali ya Tanzania na washirika wa maendeleo wanafanya kazi kwa pamoja ili kuhakikisha kunakuwepo na maendeleo katika sekta ya kilimo. Washirika wa maendeleo wafuatao wamewezesha kuchangia na kusaidia mfuko wa maendeleo wa sekta ya kilimo: Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Denmak (DANIDA), Shirika la Ushirikiano wa Kimataifa la Japan (JICA), Muungano wa Ulaya (EU), Shirika la Msaada la Kimataifa la Ireland (IA), Mfuko wa Maendeleo ya Kilimo (IFAD) na Shirika

la Maendeleo la Kimataifa (IDA). Matokeo ya ukaguzi yalikuwa kama ifuatavyo:-

**(a) Hati inayoridhisha**

Jumla ya Halmashauri 111 kati ya 133 zilizokaguliwa zilipata hati zinazoridhisha kama ilivyoonyeshwa katika jedwali Na.6 hapo chini:

**Jedwali 6: Halmashauri zilizopata hati zinazoridhisha**

| Na. | Halmashauri | Na. | Halmashauri |
|---|---|---|---|
| 1 | Wilaya ya Bukombe | 56 | Wilaya ya Kilosa |
| 2 | Wilaya ya Chato | 57 | Wilaya ya Morogoro |
| 3 | Wilaya ya Geita | 58 | Manispaa ya Morogoro |
| 4 | Wilaya ya Biharamulo | 59 | Wilaya ya Mvomero |
| 5 | Wilaya ya Bukoba | 60 | Wilaya ya Ulanga |
| 6 | Manispaa ya Bukoba | 61 | Wilaya ya Masasi |
| 7 | Wilaya ya Karagwe | 62 | Wilaya ya Mtwara |
| 8 | Wilaya ya Misenyi | 63 | Manispaa ya Mtwara/ Mikindani |
| 9 | Wilaya ya Muleba | 64 | Wilaya ya Nanyumbu |
| 10 | Wilaya ya Ngara | 65 | Wilaya ya Newala |
| 11 | Wilaya ya Bunda | 66 | Wilaya ya Tandahimba |
| 12 | Halmashauri ya Wilaya ya Musoma | 67 | Wilaya ya Bagamoyo |
| 13 | Manispaa ya Musoma | 68 | Wilaya ya Kibaha |
| 14 | Wilaya ya Serengeti | 69 | Mji Kibaha |
| 15 | Wilaya ya Tarime | 70 | Wilaya ya Kisarawe |
| 16 | Wilaya ya Magu | 71 | Wilaya ya Mafia |
| 17 | Wilaya ya Misungwi | 72 | Wilaya ya Mkuranga |
| 18 | Wilaya ya Sengerema | 73 | Wilaya ya Rufiji |
| 19 | Wilaya ya Kahama | 74 | Wilaya ya Iringa |
| 20 | Wilaya ya Kishapu | 75 | Manispaa ya Iringa |
| 21 | Wilaya ya Shinyanga | 76 | Wilaya ya Mufindi |
| 22 | Manispaa ya Shinyanga | 77 | Wilaya ya Kilolo |
| 23 | Wilaya ya Maswa | 78 | Wilaya ya Njombe |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 24 | Wilaya ya Meatu | 79 | Mji ya Njombe |
| 25 | Jiji La Arusha | 80 | Wilaya ya Makete |
| 26 | Wilaya ya Arusha | 81 | Wilaya ya Ludewa |
| 27 | Wilaya ya Longido | 82 | Mji Makambako |
| 28 | Wilaya ya Monduli | 83 | Wilaya ya Chunya |
| 29 | Wilaya ya Ngorongoro | 84 | Wilaya ya Mbarali |
| 30 | Wilaya ya Hai | 85 | Wilaya ya Mbeya |
| 31 | Wilaya ya Moshi | 86 | Jiji la Mbeya |
| 32 | Wilaya ya Mwanga | 87 | Wilaya ya Rungwe |
| 33 | Wilaya ya Rombo | 88 | Wilaya ya Mbinga |
| 34 | Wilaya ya Same | 89 | Wilaya ya Songea |
| 35 | Wilaya ya Siha | 90 | Manispaa ya Songea |
| 36 | Wilaya ya Moshi | 91 | Wilaya ya Tunduru |
| 37 | Wilaya ya Babati | 92 | Wilaya ya Namtumbo |
| 38 | Mji Babati | 93 | Wilaya ya Nkasi |
| 39 | Wilaya ya Mbulu | 94 | Mji Mpanda |
| 40 | Wilaya ya Simanjiro | 95 | Wilaya ya Bahi |
| 41 | Wilaya ya Hanang' | 96 | Wilaya ya Chamwino |
| 42 | Wilaya ya Handeni | 97 | Wilaya ya Dodoma |
| 43 | Mji Korogwe | 98 | Wilaya ya Kongwa |
| 44 | Wilaya ya Lushoto | 99 | Wilaya ya Mpwapwa |
| 45 | Wilaya ya Mkinga | 100 | Wilaya ya Kasulu |
| 46 | Wilaya ya Muheza | 101 | Wilaya ya Kibondo |
| 47 | Jiji la Tanga | 102 | Wilaya ya Kigoma |
| 48 | Manispaa ya Ilala | 103 | Manispaa ya Kigoma/Ujiji |
| 49 | Manispaa ya Kinondoni | 104 | Wilaya ya Iramba |
| 50 | Manispaa ya Temeke | 105 | Wilaya ya Manyoni |
| 51 | Wilaya ya Kilwa | 106 | Wilaya ya Singida |
| 52 | Wilaya ya Lindi | 107 | Manispaa ya Singida |
| 53 | Manispaa ya Lindi | 108 | Wilaya ya Igunga |
| 54 | Wilaya ya Ruangwa | 109 | Wilaya ya Nzega |
| 55 | Wilaya ya Kilombero | 110 | Wilaya ya Tabora |
| | | 111 | Manispaa ya Tabora |

**(b) Halmashauri zilizopata hati zenye shaka**

Halmashauri ishirini (20) ikiwa ni asilimia 15% kati ya 133 zilizokaguliwa zilipata hati zenye shaka. Sababu ya kupata hati hizo zimeelezwa kwenye Jedwali Na.7 hapa chini:

**Jedwali 7: Halmashauri zilizopata hati yenye shaka**

| Na. | Halmashauri |
|---|---|
| 1 | **Wilaya ya Rorya** |
| | • Kiasi cha Sh.46,606,158.24 kililipwa kwa ajili ya kugharamia shughuli mbalimbali bila ya kuwa na nyaraka za kutosha zinazohusiana na ripoti za utekelezaji pamoja na taarifa nyingine.<br>• Hati za malipo zenye thamani ya Sh.16,701,200 zililipwa kwa kutumia vifungu visivyohusika kinyume na Agizo Na.23 (1) la LAFM, 2009.<br>• Kiasi cha Sh.11,740,000 kilitumika katika shughuli ambazo hazikuwepo katika Mpango kazi wa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo. |
| 2 | **Wilaya ya Kwimba** |
| | • Hati za malipo ya Sh.15,990,000 zilikuwa na nyaraka pungufu.<br>• Kiasi cha Sh.381,756,002 ambacho kimeonyeshwa katika Taarifa ya Mtitiriko wa fedha kama fedha zilizohamishwa kwenda vijijini kwa ajili ya shughuli za Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo hazikuwa na nyaraka kama vile hati za malipo pamoja na risiti za kukiri mapokezi zinazoonyesha namna fedha hizo zilivyohamishwa. |
| 3 | **Jiji la Mwanza** |
| | • Kiasi cha Sh.117,687,708 kilihamishwa kwenda katika vikundi mbalimbali vya kijamii kwa ajili ya kutekeleza shughuli za Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo. Hata hivyo, kiasi hiki hakikuonyeshwa katika taarifa za fedha kwa mwaka unaoishia tarehe 30 Juni, 2013. |
| 4 | **Wilaya ya Ukerewe** |
| | • Kiasi cha Sh.175,721,796 kilichopokelewa kutoka Wizara ya Fedha hakikuonyeshwa katika taarifa ya Mtiririko wa |

| | |
|---|---|
| | fedha. |
| **5** | **Wilaya ya Bariadi** |
| | • Hati za malipo yenye thamani ya Sh.485,803,736 hazikuwasilishwa kwa ajili ya Ukaguzi. |
| **6** | **Wilaya ya Kiteto** |
| | • Matumizi ya mafuta lita 1,442 yenye thamani ya Sh.4,162,400 hayakuingizwa kwenye vitabu vya magari.<br>• Hati za malipo ya Sh.13,958,000 yalikuwa na nyaraka pungufu kinyume na Agizo Na. 8(2)(c) la LAFM, 2009. |
| **7** | **Wilaya ya Kilindi** |
| | • Taarifa ya fedha za Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo kwa mwaka wa fedha 2011/12 inaonyesha kiasi cha Sh.70,961,416 kama bakaa mwisho wa mwaka wakati Halmashauri imeonyesha bakaa ya mwisho wa mwaka ya Sh. 40,222,671 katika vitabu vyake. Hivyo kusababisha tofauti ya Sh.30,738,745. |
| **8** | **Wilaya ya Korogwe** |
| | • Kiasi cha Sh.14,477,000 ambacho ni fedha za ruzuku kwa ajili ya matumizi ya kawaida kilionyeshwa pungufu katika taarifa ya fedha. |
| **9** | **Wilaya ya Pangani** |
| | • Kiasi cha Sh.26,294,696 kilichotokana na uchakavu wa Mali, Mitambo na Vifaa hakikuonyeshwa katika taarifa ya Utendaji wa fedha.<br>• Madeni ya Sh.23,843,831 katika Taarifa ya Mtiririko wa fedha hayakuonyeshwa katika fedha zinazotokana na shughuli za kawaida. |
| **10** | **Wilaya ya Meru** |
| | • Mali, Mitambo na Vifaa vilionyeshwa kwenye taarifa za hesabu kwa zaidi ya Sh.62,013,521; hii ilifanya uchakavu uliokokotolewa kuwa zaidi kwa Sh.4,667,685.<br>• Hati za malipo ya Sh. 2,470,000 hazikuwasilishwa kwa ajili ya ukaguzi na kusababisha kutoweza kuthibitishwa kwa uhalali wa malipo yaliyofanyika. |

| | |
|---|---|
| 11 | **Wilaya ya Karatu** |
| | • Majengo, Mitambo na Vifaa vilionyeshwa kuwa na thamani zaidi kwa kiasi cha Sh.132,500,000.<br>• Taarifa ya Mtiririko wa fedha imeonyesha fedha ambazo siyo sahihi kama ifuatavyo:<br><br>(a) Upungufu wa vifaa umeonyeshwa ni sifuri wakati Taarifa ya Mizania ya hesabu ilionyesha upungufu wa vifaa ni Sh.37,000,000.<br><br>(b) Upungufu wa madai umeonyeshwa ni Sh.60,382,590.80 wakati katika Taarifa ya Mizania ya hesabu hakukuwa na taarifa ya madai yaliyoonyeshwa katika hesabu za mwaka wa fedha 2011/12 kwa ajili ya ulinganifu. |
| 12 | **Wilaya ya Liwale** |
| | • Hati za malipo yenye thamani ya Sh.16,070,000 hazikuwasilishwa kwa ajili ya ukaguzi.<br>• Malipo ya Sh.7,215,000 yalilipwa kwa kutumia vifungu visivyohusika. |
| 13 | **Wilaya ya Nachingwea** |
| | • Malipo ya Sh.27,850,300 kwa ajili ya ujenzi wa jengo la maonyesho ya Nanenane Ngongo na ununuzi wa pikipiki yalifanywa bila ya kuwepo katika bajeti.<br>• Hati za malipo ya Sh.81,236,506 hazikuwasilishwa kwa ajili ya ukaguzi na hivyo uhalali wa matumizi yaliyofanyika haukuweza kuthibitishwa.<br>• Malipo ya Sh.196,800,655 yalilipwa kwa kutumia vifungu visivyohusika. |
| 14 | **Wilaya ya Mpanda** |
| | • Kiasi cha Sh.21,500,000 ambacho kilikuwa ni sehemu ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya ujenzi wa ghala katika kijiji cha Ikulwe kilitolewa benki kinyume na taratibu na kutumiwa kibadhilifu. |
| 15 | **Wilaya ya Sikonge** |

| | |
|---|---|
| | • Kulikuwa na upungufu wa Sh.20,088,853 wa mtaji wa fedha za maendeleo katika taarifa.<br>• Kiasi cha Sh.78,574,667 kilionyeshwa kama matumizi ya vifaa vya ofisi lakini kidokezo Na.18 kinachoelezea zaidi matumizi ya vifaa vya ofisi kimeonyesha matumizi ni Sh.7,918,900 na hivyo kusababisha utofauti wa Sh.70,655,767<br>• Malipo ya Sh.150,260,651 yalibainika kulipwa kwa kutumia vifungu visivyohusika. |
| **16** | **Wilaya ya Urambo** |
| | • Madai ya Sh.204,035,360 hayakuonyeshwa katika Taarifa ya Mizania ya hesabu. |
| **17** | **Wilaya ya Kondoa** |
| | • Kiasi cha Sh.14,590,000 kililipwa kwa ajili ya madeni ya mwaka wa fedha uliopita ambayo hayakuonyeshwa katika taarifa za fedha.<br>• Malipo ya Sh.32,360,401 yalilipwa kwa shughuli mbalimbali za kilimo bila kuwa na nyaraka za kutosha. |
| **18** | **Wilaya ya Ileje** |
| | • Kiasi cha Sh.23,351,983 kilitumika zaidi ya fedha zilizokuwepo kwa ajili ya shughuli za Programu ya Maendeleo katika Sekta ya Kilimo.<br>• Matumizi ya Sh.5,000,000 yalilipwa kwa kutumia vifungu visivyohusika bila ya kibali kutoka kwa kamati ya fedha.<br>• Halmashauri ilinunua lita 670 za mafuta yenye thamani ya Sh.1,675,000, nyaraka zinazothibitisha matumizi ya mafuta hayo hazikutolewa kwa ajili ya ukaguzi. |
| **19** | **Wilaya ya Kyela** |
| | • Nyaraka za mikataba ya zabuni inayohusu mradi wa kilimo cha umwagiliaji Ngana wenye thamani ya Sh.66,827,500 hazikuwasilishwa kwa ajili ya ukaguzi.<br>• Kiasi cha Sh.5,200,000 zilitumika kwa ajili ya ununuzi wa mafuta ambayo hayakuingizwa katika leja ya mafuta. |
| **20** | **Wilaya ya Sumbawanga** |
| | • Hati za malipo ya Sh.1,480,000 hazikuwasilishwa kwa |

| | |
|---|---|
| | ajili ya ukaguzi kinyume na Agizo Na.34(1) la LAFM, 2009.<br><br>• Malipo ya Sh.3,747,500 yalikuwa na nyaraka pungufu.<br>• Malipo ya Sh.18,340,000 yalilipwa bila ya kuwa na taarifa ya utekelezaji.<br>• Kiasi cha Sh.6,647,713 kilitumika kugharamia matumizi ambayo hayakuwepo katika bajeti ya Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo ya mwaka 2012/13. |

**(c) Hati isiyoridhisha**

Halmashauri moja (1) ambayo ni sawa na asilimia 0.75% ya halmashauri 133 zilizokaguliwa ilipata hati isiyoridhisha kama ilivyoonyeshwa kwenye jedwali Na.8 hapa chini:

**Jedwali 8: Halmashauri iliyopata hati isiyoridhisha**

| | **Halmashauri** |
|---|---|
| 1 | **Manispaa ya Sumbawanga** |
| | • Malipo ya Sh.24,618,298 yalikuwa na nyaraka pungufu kinyume na Agizo Na. 8 (2)(c) la LAFM, 2009.<br><br>• Kiasi cha Sh.374,039,819.29 kilionyeshwa katika Taarifa ya Mizania ya hesabu kama thamani ya Majengo, Mitambo na Vifaa kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2013. Hata hivyo, kidokezo Na.27 kinachohusiana na taarifa za Majengo, Mitambo na Vifaa kimeonyesha thamani ni Sh.423,959,819.29 na hivyo kusababisha utofauti wa Sh.49,920,000 usio na maelezo.<br><br>• Kiasi cha Sh.378,039,819 ambacho ni fedha za ruzuku kwa ajili ya shughuli za maendeleo hakikuwa na viambatanisho vya kuonyesha mchanganuo.<br><br>• Kiasi cha Sh.1,011,500 ambacho ni madai yanayotokana na masurufu hakikuonyeshwa katika Taarifa ya Mizania ya hesabu.<br><br>• Kiasi cha Sh.33,654,734 ambacho ni fedha zilizotumika kwa ajili ya shughuli za maendeleo kwa mwaka wa fedha |

| | |
|---|---|
| | 2012/13 kilikosa maelezo.<br><br>• Manunuzi ya Sh.128,639,000 ambayo ni Mali, Mitambo na Vifaa yameonyeshwa katika Taarifa ya Mtiririko wa fedha kwa mwaka 2012/13. Hata hivyo, kiasi hiki kilipaswa kufanana na thamani ya ongezeko la mali katika kidokezo Na.27 ambacho kimeonyesha Sh.135,271,000 hivyo kusababisha tofauti ya Sh. 6,632,000. |

**(d) Hati Mbaya**

Halmashauri moja (1) ambayo ni sawa na asilimia 0.75% kati ya Halmashauri 133 zilizokaguliwa ilipata hati mbaya kama ilivyoonyeshwa kwenye Jedwali Na.9 hapa chini:

**Jedwali 9: Halmashauri iliyopata hati isiyoridhisha**

| **1** | **Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi** |
|---|---|
| | • Kiasi cha Sh.106,889,500 kililipwa bila ya kufanyiwa ukaguzi wa awali.<br>• Kiasi cha Sh.71,176,000 kilitumika katika shughuli ambazo hazihusiani na Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo.<br>• Kiasi cha Sh.30,000,000 kilitumika katika matumizi ambayo hayakuainishwa katika mpango wa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo. |

**(e) Halmashauri ambazo hazikupata Fedha za Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo**

Kati ya halmashauri 140, halmashauri saba (7) ambazo ni sawa na asilimia tano (5%) hazikupata fedha za Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo kutokana na nyingi kuwa mpya na nyinginekutokuwa na shughuli za kilimo kama Jiji la Dar es Salaam. Jedwali Na.10 hapa chini linaonyesha Halmashauri hizo:

**Jedwali 10: Halmashauri ambazo hazikupata Fedha za Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo**

| Na. | Halmashauri | Sababu |
|---|---|---|
| 1 | Mji Geita | Mpya |
| 2 | Manispaa ya Ilemela | Mpya |
| 3 | Mji Kahama | Mpya |
| 4 | Mji Bariadi | Mpya |
| 5 | Jiji la Dar es Salaam | Hakuna shughuli za kilimo |
| 6 | Wilaya ya Busokeli | Mpya |
| 7 | Mji Masasi | Mpya |

### 2.3.2 Mfuko wa Maendeleo ya Afya

**Utangulizi**

Serikali ya Tanzania imeendeleza mchakato wa kurekebisha sekta ya afya ili kuboresha utoaji wa huduma ya afya. Ili kuboresha utaratibu na utekelezaji wa huduma za afya katika sekta ya afya, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii na Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa kushirikiana na washirika wa maendeleo wameandaa mbinu mbalimbali za kuendeleza vitendea kazi na vifaa katika kutoa huduma za afya kupitia mpangilio wa mfuko wa maendeleo ya huduma ya afya.

Kama sehemu ya programu ya maboresho ya maendeleo ya sekta ya afya na ili kukuza, kuratibu, kupanga na kutekeleza huduma ya afya ndani ya sekta ya afya, serikali ya Tanzania imeaamua kuwa na mtazamo mpana wa utoaji wa huduma za afya kwa kutafuta rasilimali ndani na nje. Kwa mantiki hiyo serikali na washirika wa maendeleo kama vile Ubalozi wa Uholanzi, DANIDA, Shirika la Misaada la Ireland, SDC, Ushirikiano wa Tanzania na Ujerumani (GIZ), KfW, UNFPA na Benki ya Dunia waliingia makubaliano ya mtazamo mpana wa kisekta kuunda mfuko wa pamoja katika maeneo yaliyoainishwa na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii katika mpango kazi wa mwaka.

Mwaka 1999, Serikali ya Tanzania na Wafadhili wa Maendeleo walisaini makubaliano ya pamoja ya kutekeleza mihadi katika

sekta ya afya kwa mtazamo mpana wa kisekta ili kufikia ukuaji endelevu wa sekta ya afya kwa wananchi.

Madhumuni ya kuweka pamoja misaada ya fedha ni kusaidia juhudi za maendeleo ya sekta ya afya Tanzania. Uchangiaji wa wadau wa maendeleo umeongeza bajeti ya afya ya mwaka kutoka Dola za Marekani USD1.25 hadi Dola za Marekani USD1.80 kwa kila mtanzania kama ruzuku ya mfuko wa maendeleo ya afya. Matokeo ya ukaguzi kwa Mfuko wa Afya ni kama ilivyo hapa chini:

**(a) Halmashauri zilizopata hati inayoridhisha**

Halmashauri mia moja na tatu (103) zilipata hati inayoridhisha sawa na asilimia 78 ya halmashauri mia moja na thelathini na mbili zilizokaguliwa kama inavyoonyeshwa kwenye Jedwali Na.11 hapo chini:

**Jedwali 11: Halmashauri zilizopata hati inayoridhisha**

| Na. | Halmashauri | Na. | Halmashauri |
|---|---|---|---|
| 1 | Wilaya ya Biharamulo | 53 | Wilaya ya Newala |
| 2 | Wilaya ya Muleba | 54 | Wilaya ya Masasi |
| 3 | Manispaa ya Bukoba | 55 | Wilaya ya Kisarawe |
| 4 | Wilaya ya Missenyi | 56 | Wilaya ya Kibaha |
| 5 | Wilaya ya Ngara | 57 | Wilaya ya Mafia |
| 6 | Wilaya ya Kwimba | 58 | Wilaya ya Rufiji |
| 7 | Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi | 59 | Wilaya ya Bagamoyo |
| 8 | Wilaya ya Ukerewe | 60 | Mji wa Kibaha |
| 9 | Wilaya ya Magu | 61 | Manispaa ya Ilala |
| 10 | Manispaa ya Musoma | 62 | Manispaa ya Kinondoni |
| 11 | Wilaya ya Tarime | 63 | Manispaa ya Temeke |
| 12 | Wilaya ya Kahama | 64 | Wilaya ya Iringa |
| 13 | Wilaya ya Kishapu | 65 | Manispaa ya Iringa |
| 14 | Manispaa ya Shinyanga | 66 | Wilaya ya Mufindi |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 15 | Wilaya ya Shinyanga | 67 | Wilaya ya Kilolo |
| 16 | Wilaya ya Meatu | 68 | Wilaya ya Sumbawanga |
| 17 | Wilaya ya Arusha | 69 | Wilaya ya Nkasi |
| 18 | Jiji la Arusha | 70 | Wilaya ya Chunya |
| 19 | Wilaya ya Longido | 71 | Wilaya ya Ileje |
| 20 | Wilaya ya Moshi | 72 | Wilaya ya Mbarali |
| 21 | Manispaa ya Moshi | 73 | Wilaya ya Mbeya |
| 22 | Wilaya ya Same | 74 | Jiji la Mbeya |
| 23 | Wilaya ya Mwanga | 75 | Wilaya ya Rungwe |
| 24 | Wilaya ya Siha | 76 | Wilaya ya Mbinga |
| 25 | Wilaya ya Hai | 77 | Manispaa ya Songea |
| 26 | Wilaya ya Rombo | 78 | Wilaya ya Songea |
| 27 | Wilaya ya Muheza | 79 | Wilaya ya Tunduru |
| 28 | Jiji la Tanga | 80 | Wilaya ya Bahi |
| 29 | Wilaya ya Mkinga | 81 | Wilaya ya Chamwino |
| 30 | Wilaya ya Kilindi | 82 | Manispaa ya Dodoma |
| 31 | Wilaya ya Lushoto | 83 | Wilaya ya Kondoa |
| 32 | Mji wa Korogwe | 84 | Wilaya ya Kongwa |
| 33 | Wilaya ya Babati | 85 | Wilaya ya Mpwapwa |
| 34 | Wilaya ya Mbulu | 86 | Wilaya ya Kasulu |
| 35 | Wilaya ya Simanjiro | 87 | Wilaya ya Kibondo |
| 36 | Wilaya ya Hanang’ | 88 | Wilaya ya Kigoma |
| 37 | Wilaya ya Kilwa | 89 | Manispaa ya Kigoma/Ujiji |
| 38 | Manispaa ya Lindi | 90 | Wilaya ya Iramba |
| 39 | Wilaya ya Nachingwea | 91 | Wilaya ya Manyoni |
| 40 | Wilaya ya Lindi | 92 | Wilaya ya Singida |
| 41 | Wilaya ya Liwale | 93 | Manispaa ya Singida |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 42 | Wilaya ya Ruangwa | 94 | Wilaya ya Nzega |
| 43 | Wilaya ya Kilombero | 95 | Wilaya ya Sikonge |
| 44 | Wilaya ya Morogoro | 96 | Wilaya ya Tabora |
| 45 | Wilaya ya Mvomero | 97 | Manispaa ya Tabora |
| 46 | Wilaya ya Kilosa | 98 | Wilaya ya Urambo |
| 47 | Manispaa ya Morogoro | 99 | Wilaya ya Njombe |
| 48 | Wilaya ya Ulanga | 100 | Mji wa Njombe |
| 49 | Wilaya ya Mtwara | 101 | Wilaya ya Makete |
| 50 | Wilaya ya Nanyumbu | 102 | Wilaya ya Ludewa |
| 51 | Wilaya ya Tandahimba | 103 | Mji wa Mpanda |
| 52 | Manispaa ya Mtwara | | |

**(b) Halmashauri zilizopata hati zenye shaka**

Kati ya halmashauri 132 zilizokaguliwa, halmashauri ishirini na sita (26) sawa na asilimia 19.7% zilipata hati zenye shaka. Orodha ya halmashauri hizo na sababu za kupata hati hizo ni kama inavyoonekana kwenye Jedwali Na. 12 hapa chini:

**Jedwali 12: Halmashauri zilizopata hati zenye shaka**

| | **Halmashauri** |
|---|---|
| **1.** | **Wilaya ya Karagwe** |
| | • Kiasi cha Sh.11,386,000 kililipwa nje ya bajeti ya Mfuko wa Maendeleo wa Afya kinyume na Agizo 23(1) la Memoranda ya Fedha za Serikali za Mitaa ya mwaka, (2009). |
| **2.** | **Wilaya ya Sengerema** |
| | • Kiasi kilichotumika ambacho ni fedha za ruzuku kwa ajili ya matumizi ya kawaida kilionyeshwa zaidi kwa Sh.19,056,569 kwenye taarifa za fedha. Kiasi sahihi kilichopaswa kuonyeshwa kama matumizi ya mwaka unaoishia 30 Juni 2013 ni Sh.1,013,835,431 na siyo Sh.1,032,892,000 kama ilivyoonyeshwa kwenye taarifa.<br>• Halmashauri ilionyesha kwenye taarifa za fedha kiasi cha Sh.219,749,000 kama bakaa ya ruzuku ya miradi |

| | |
|---|---|
| | ya maendeleo mwishoni mwa mwaka badala ya Sh.357,450,161 hivyo kupelekea upungufu wa Sh.137,701,161.<br>• Halmashauri ililipa kiasi cha Sh.34,205,000 kutoka kwenye kasma isiyosahihi kinyume na Agizo 23(1) la LAFM, 2009.<br>• Halmashauri ilinunua dawa na vifaa tiba Bohari Kuu ya Dawa vyenye thamani ya Sh.106,852,100 ambapo hadi wakati wa ukaguzi huu, dawa na vifaa hivyo vilikuwa havijapokelewa. |
| 3. | **Wilaya ya Bunda** |
| | • Malipo ya Sh.4,580,000 yaliyolipwa na Halmashauri hayakuwa na nyaraka za kutosha kinyume na Agizo 8(2) (c) la LAFM, (2009). |
| 4. | **Wilaya ya Musoma** |
| | • Kulikuwa na malipo ya Sh.15,326,250 ambayo hayakuwa na nyaraka za kutosha kinyume na Agizo 8(2) (c) la LAFM, 2009.<br>• Kukosekana kwa hati za malipo zenye thamani ya Sh.77,114,000<br>• Malipo yenye thamani ya Sh.1,260,000 yalilipwa kutoka kwenye kasma isiyo sahihi kinyume na Agizo 23(1) la LAFM, 2009 |
| 5. | **Wilaya ya Rorya** |
| | • Malipo ya Sh.28,146,745 hayakuwa na nyaraka za kutosha kinyume na Agizo 8(2) (c) la LAFM, (2009) |
| 6. | **Wilaya ya Serengeti** |
| | • Malipo ya Sh.27,479,208 hayakuwa na viambatanisho vya kutosha kinyume na Agizo 8(2) (c) la LAFM, (2009) |
| 7. | **Wilaya ya Maswa** |
| | • Halmashauri ililipa kiasi cha Sh.57,981,200 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa mbalimbali, hata hivyo vifaa hivyo havikuingizwa kwenye leja ya kupokelea vifaa kinyume na Agizo 59(1) la LAFM, 2009.<br>• Kiasi cha Sh.93,248,716 kilicholipwa kwa wafanyakazi wa halmashauri, taasisi na makampuni mbalimbali hakikuwa na nyaraka za kutosha kinyume na Agizo |

| | |
|---|---|
| | 8(2) (c) la LAFM, (2009).<br>• Hati za malipo zenye thamani ya Sh.15,327,500 zilikosekana wakati wa ukaguzi kinyume na Agizo 104(1) ya LAFM, 2009. |
| **8.** | **Wilaya ya Meru** |
| | • Taarifa za Hesabu za Mfuko wa Maendeleo ya Afya zilijumuisha kiasi cha Sh.228,809,539 ambazo ni fedha za EGPAF na hivyo kufanya mapato na matumizi kuzidi kwa Sh.228,809,539<br>• Mali, mitambo na vifaa mbalimbali zilionyeshwa pungufu kwa Sh.4,100,000 kutokana na kuonyeshwa kimakosa manunuzi ya komputa kwa kiasi cha Sh.2,885,700 badala ya Sh.6,985,700.<br>• Vifaa vyenye thamani ya Sh.113,853,189 zilizoonyeshwa kwenye taarifa ya mizania hazikuwa na vidokezo vya maelezo na majedwali ili kuthibitisha uwepo na uhalali wake<br>• Taarifa ya mtiririko halisi wa fedha haukuonyesha fedha zilizopokelewa kwa ajili ya miradi ya maendeleo kwa mwaka husika pamoja na fedha zilizotumika kwa ajili ya ununuzi wa mali, mitambo na vifaa mbalimbali kwa kiasi cha Sh.29,591,461<br>• Malipo ya Sh.7,149,114 yalifanywa bila kuwa na nyaraka za uthibitisho wa uhalali wa malipo hayo kinyume na Agizo 8(2) (c) la Memoranda ya Fedha za Serikali za Mitaa ya mwaka, (2009)<br>• Halmashauri ililipa kiasi cha Sh.15,749,825 kwa M/S Kitwai Engineering Ltd ikiwa ni matumizi yasiyo na tija kwa ajili ya matengenezo makubwa ya gari la kubebea wagonjwa lililopata ajali ambalo lilikuwa halina bima (ambulance) lenye namba za usajili za serikali za mitaa (SM 5080) |
| **9.** | **Wilaya ya Monduli** |
| | • Hati ya malipo yenye thamani ya Sh.3,732,500 iliyolipwa kwa Mkurugenzi Mtendaji ilikosekana wakati wa ukaguzi. Kukosekana kwa hati hiyo ya malipo, kunafanya uhalali wa matumizi yaliyofanywa kutoweza kuthibitika. |

| | |
|---|---|
| | • Hati za malipo zenye thamani ya Sh.12,133,500 hazikuwa na viambatanisho vya kutosha ili kuthibitisha uhalali wake kinyume na Agizo 8(2) (c) la Memoranda ya Fedha za Serikali za Mitaa ya mwaka, (2009) |
| **10.** | **Wilaya ya Karatu** |
| | • Kinyume na Agizo 8(2) (c) la LAFM, (2009), hati za malipo zenye thamani ya Sh.21,208,000 zilikosa nyaraka za kutosha ili kuthibitisha uhalali wa malipo hayo. |
| **11.** | **Wilaya ya Ngorongoro** |
| | • Kiasi cha Sh.614,220,950 kilionyeshwa kwenye taarifa ya utendaji wa fedha kama matumizi ya kawaida yaliyolipwa kwa kutumia fedha za ruzuku. Hata hivyo kiasi cha Sh.500,253,250 kiliainishwa kama matumizi ya kawaida kwa mwaka husika. Hivyo matumizi ya kawaida ya fedha za ruzuku yalionyeshwa zaidi kwenye taarifa za fedha kwa Sh.113,967,70<br>• Ongezeko la wadai wa halmashauri kwa kiasi cha Sh.6,822,000 halikuonyeshwa kwenye taarifa ya mtiririko halisi wa fedha kinyume na viwango vya kimataifa ya kihasibu katika sekta ya Umma<br>• Kiasi cha Sh.515,445,804 kilionyeshwa kimakosa kwenye taarifa ya mtiririko halisi wa fedha kwenye kipengele cha fedha zilizotumika kwa mwaka husika kwa ajili ya miradi ya maendeleo.<br>• Fedha za ruzuku kiasi cha Sh.451,902,246 kwa ajili ya matumizi ya kawaida zilizopokelewa kwa mwaka husika zilionyeshwa kama fedha zilizotumika kwenye miradi ya maendeleo katika taarifa ya mtiririko halisi wa fedha kinyume na viwango vya kimataifa vya kihasibu katika sekta ya umma.<br>• Malipo mbalimbali ya Sh.24,530,125 yaliyolipwa hayakuwa na nyaraka za kutosha kinyume na Agizo 8(2) (c) la LAFM, 2009. |
| **12.** | **Wilaya ya Pangani** |
| | • Malipo yenye thamani ya Sh.1,029,000 hayakuwa na nyaraka za kutosha kinyume na Agizo 8(2) (c) la LAFM, 2009. Hivyo uhalali wa malipo hayo haukuweza |

| | |
|---|---|
| | kuthibitishwa. |
| **13.** | **Wilaya ya Korogwe** |
| | • Mwishoni mwa mwaka halmashauri ilikuwa na lita 11,601 za mafuta ya dizeli yenye thamani ya Sh.24,130,080 ambayo hayakuonyeshwa kwenye taarifa ya mizania kinyume na viwango vya kimataifa vya kihasibu katika sekta ya Umma.<br>• Kulikuwa na kiasi cha Sh.4,065,800 kilicholipwa Bohari Kuu ya Dawa kabla ya kupokea dawa na vifaa vya hospitali, hata hivyo kiasi hicho hakikuonyeshwa kwenye taarifa ya mizania kama malipo kabla ya kupokea huduma kinyume na viwango vya kimataifa vya kihasibu katika sekta ya umma. |
| **14.** | **Wilaya ya Handeni** |
| | • Kiasi cha Sh.474,143,215 ambacho ni matumizi ya kawaida kilionyeshwa kwenye taarifa ya mtiririko halisi wa fedha kama matumizi yote yaliyofanywa kwa kutumia fedha za ruzuku. Hata hivyo kulingana na viwango vya kimataifa vya kihasibu katika sekta ya umma, matumizi yote yaliofanywa kwa kutumia fedha za ruzuku hayapaswi kuonyeshwa kwenye taarifa ya mtiririko.<br>• Kiasi cha Sh.217,402,385 ambacho ni mabadiliko ya ruzuku ya matumizi ya kawaida ambayo haikutumika hakikuonyeshwa kwenye taarifa ya mtiririko halisi wa fedha. Hii imetokana na tofauti kati ya kiasi cha ruzuku ya matumizi ya kawaida ambayo haikutumika mwanzoni mwa mwaka Sh.301,358,857 na mwishoni mwa mwaka Sh.518,761,242.<br>• Kiasi cha Sh.691,545,600 kilionyeshwa kwenye taarifa ya mtiririko halisi wa fedha kama ruzuku ya miradi ya maendeleo kilichopokelewa kwa mwaka husika. Hata hivyo kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2012/13 Halmashauri haikupokea ruzuku ya miradi ya maendeleo kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za Mfuko wa Maendeleo wa Afya, shughuli za Mfuko huu |

| | |
|---|---|
| | zilihusu matumizi ya kawaida tu. Hivyo kiasi cha Sh.691,545,600 kisingeonyeshwa kwenye taarifa ya mtiririko halisi wa fedha.<br>• Malipo ya Sh.5,059,500 hayakuwa na viambatanisho vya kutosha kinyume na Agizo 8(2) (c) la LAFM, 2009. |
| **15.** | **Mji wa Babati** |
| | • Malipo ya Sh.16,692,707.24 hayakuwa na viambatanisho vya kutosha kinyume na Agizo 8(2) (c) la Memoranda ya Fedha za Serikali za Mitaa ya mwaka, (2009)<br>• Kiasi cha Sh.110,162,925 ikiwa ni fedha za Mfuko wa Maendeleo ya afya zilitumika kwenye shughuli zisizokusudiwa. |
| **16.** | **Wilaya ya Kiteto** |
| | • Malipo yaliyofanywa ya Sh.6,618,980 hayakuwa na nyaraka za kutosha kinyume na Agizo 8(2) (c) la LAFM, 2009. |
| **17.** | **Wilaya ya Mkuranga** |
| | • Halmashauri ilinunua gesi yenye thamani ya Sh.11,900,000 kwa ajili ya kutekeleza shughuli za chanjo, hata hivyo hati za kupokelea gesi pamoja na daftari ya kupokelea mali havikuwasilishwa ili kuthibitisha uhalali wa matumizi hayo.<br>• Halmashauri ililipa kiasi cha Sh.16,204,450 kutoka kwenye mfuko wa maendeleo ya afya kwa ajili ya ununuzi wa dawa na vifaa vya hospitali kutoka kwa wazabuni mbalimbali bila uthibitisho wa kukosekana katika Bohari Kuu ya Dawa.<br>• Halmashauri ililipa kiasi cha Sh.13,148,000 kwa ajili ya matengenezo ya magari kwenye karakana binafsi bila kukaguliwa na kuidhinishwa na Wakala wa Huduma za Umeme na Mitambo kabla na baada ya matengenezo kinyume na Kanuni Na. 59(1-3) ya Sheria ya Manunuzi ya Umma, 2005.<br>• Halmashauri ilinunua dawa na vifaa tiba vyenye thamani ya Sh.113,273,000 bila kuingizwa kwenye leja ya kupokelea vifaa na hati ya kutolea vifaa hivyo haikuwasilishwa kwa ajili ya ukaguzi kinyume na Agizo |

| | |
|---|---|
| | Na.59(1)(2) la LAFM, 2009. |
| **18.** | **Wilaya ya Kyela** |
| | • Kiasi cha Sh.203,229,290 ambacho ni salio ishia kilichoonyeshwa kwenye taarifa ya mizania kinatofautiana na kiasi cha Sh.111,717,296 cha ruzuku ya miradi ya maendelelo ambayo haikutumika kwa Sh.91,511,994.<br><br>• Taarifa za Hesabu hazikuonyesha vidokezo vya maelezo pamoja na sera za kihasibu zilizotumika katika kuandaa taarifa za hesabu za mwaka husika. |
| **19.** | **Wilaya ya Namtumbo** |
| | • Hati za malipo zenye thamani ya Sh.24,881,000 hazikuwasilishwa wakati wa ukaguzi kinyume na kifungu 45(5) cha Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa namba 9 ya mwaka 1982 iliyorekibishwa mwaka 2000 na Agizo 104 la LAFM, 2009. |
| **20.** | **Wilaya ya Igunda** |
| | • Taarifa ya mabadiliko ya mali za kudumu ilikuwa pungufu kwa Sh.43,061,000 ikiwa ni zidio (surplus) ambalo halikuweza kuthibitika.<br>• Kiasi chote cha Sh.861,315,000 kilichopokelewa kwa mwaka husika kilionyeshwa kama ruzuku ya miradi ya maendeleo kwenye taarifa ya mtiririko halisi wa fedha ikiwa ni fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo, wakati kiasi cha Sh.5,627,000 kilionyeshwa kwenye mtiririko halisi wa fedha kama ununuzi wa mali, mitambo na vifaa mbalimbali hivyo kupelekea utofauti wa Sh.855,688,000.<br>• Kiasi cha Sh.267,646,000 kilionyeshwa kwenye taarifa za fedha mwishoni mwa mwaka kama bakaa ya fedha taslim badala ya Sh.1,140,601,000 na hivyo kufanya utofauti wa Sh.872,955,000. |
| **21** | **Wilaya ya Bukombe** |
| | • Hati za malipo zenye thamani ya Sh.35,373,972 zilikosekana wakati wa ukaguzi kinyume na Agizo Na.34(1) la LAFM, 2009. |

| | |
|---|---|
| **22.** | **Wilaya ya Chato** |
| | • Kiasi cha Sh.11,060,000 kilicholipwa kwa wafanyakazi wa halmashauri kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali hakikuwa na mchanganuo wa malipo uliosainiwa na walipwaji. |
| **23.** | **Wilaya ya Geita** |
| | • Kulikuwa na malipo ya Sh.70,629,168 ambayo yalikosa viambatanisho vya kutosha kama vile stakabadhi za kukiri mapokezi, hati za madai na hati za kupokelea bidhaa/vifaa kinyume na Agizo 8(2) (c) la LAFM, 2009. |
| **24.** | **Wilaya ya Bukoba** |
| | • Halmashauri ililipa kiasi cha Sh.10,247,100 kwa kazi ambazo hazikuwa kwenye bajeti iliyoidhinishwa ya Mfuko wa Maendeleo ya Afya kama ilivyoainishwa kwenye mwongozo kabambe wa afya (Comprehensive Council Health Planning Guideline). |
| **25.** | **Wilaya ya Bariadi** |
| | • Jumla ya kiasi cha Sh.120,870,000 kililipwa na halmashauri ikiwa ni posho kwa ajili ya masaa ya ziada, Sh.23,620,000 na posho ya kujikimu Sh.97,250,000, bila kuambatanisha fomu maalum ya maombi ambayo ingeonyesha aina ya kazi na tarehe ya utekelezaji, hivyo uhalali wa malipo hayo haukuweza kuthibitika. |
| **26.** | **Jiji la Mwanza** |
| | • Kiasi cha Sh.22,192,740 kililipwa kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali; hata hivyo hakukuwa na taarifa ya utekelezaji wa kazi na viambatanisho vingine muhimu kinyume na Agizo (8)(2) (c) na 104 la Memoranda ya Fedha za Serikali za Mitaa za Mwaka, 2009. |

**(d) Halmashauri zilizopata hati isiyoridhisha**

Kati ya halmashauri mia moja thelethini na mbili (132) zilizokaguliwa, Halmashauri mbili (2) zilipata hati isiyoridhisha sawa na asilimia 0.76% kama inavyoonekana kwenye Jedwali Na.13 hapo chini:

**Jedwali 13: Halmashauri zilizopata hati isiyoridhisha**

| Na. | Halmashauri |
|---|---|
| 1 | **Wilaya ya Sumbawanga** |
| | • Kiasi kilichotumika kwa mwaka wa fedha 2012/13 cha Sh.355,846,400 kilichotokana na fedha za ruzuku ya matumizi ya kawaida kilichoonyeshwa kwenye taarifa ya utendaji wa kifedha kinatofautina na kiasi cha Sh.238,229,719 kilichoonyeshwa kwenye kidokezo Na.11 na hivyo kupelekea ziada ya Sh.117,616,681.<br>• Taarifa ya mizania ya tarehe 30 Juni, 2013 inaonyesha kulikuwa na ongezeko la fedha za ruzuku zilizobaki kwa ajili ya matumizi ya kawaida kwa Sh.23,474,240 kutoka mwaka 2011/12 hadi Sh.141,090,920.71 kwa mwaka 2012/13, hata hivyo ongezeko hili halikuonyeshwa kwenye taarifa ya mtiririko halisi wa fedha kwa mwaka unaoishia tarehe 30 Juni, 2013.<br>• Taarifa ya mizania ya tarehe 30 Juni, 2013 inaonyesha ongezeko la mali kutoka Sh. 0 kwa mwaka wa fedha 2011/12 hadi Sh.6,365,600 kwa mwaka wa fedha 2012/13, ongezeko hili lingepaswa kuonyeshwa kwenye taarifa ya mtiririko halisi wa fedha, hata hivyo ongezeko hili halikuonyeshwa kwenye taarifa hiyo inayoishia tarehe 30 Juni, 2013. |
| 2 | **Wilaya ya Mpanda** |
| | • Bakaa ya fedha taslim ilionyeshwa pungufu kwa Sh.121,111,109.48, hii ina maana kuwa taarifa za hesabu hazionyeshi uhalisia. |

**(d) Halmashauri iliyopata hati mbaya**

Halmashauri moja (1) ilipata hati mbaya sawa na asilimia 0.76 kati ya halmashauri mia moja thelathini na mbili ambazo zilikaguliwa kama inavyoonekana kwenye jedwali Na.14 hapo chini.

**Jedwali 14: Halmashauri iliyopata hati mbaya**

| 1 | Wilaya ya Mbozi |
|---|---|
| | Halmashauri haikuandaa taarifa za hesabu zinazohusu Mfuko wa Maendeleo ya Afya kwa mwaka unaoishia tarehe 30, Juni 2013 na kuziwasilisha kwa ajili ya ukaguzi, kinyume na makubaliano yaliyofikiwa kati ya washirika wa maendeleo na serikali na kwa mujibu wa misingi inayotumika katika uandaaji wa taarifa hizo |

**(e) Halmashauri ambazo hazikupata fedha**

Halmashauri nane (8) zilizoorodheshwa kwenye jedwali Na.15 hapo chini hazikuingizwa kwenye taarifa ya utekelezaji na utendaji wa kifedha wa mradi ya Afya kwa sababu hazikupata fedha kwa kipindi cha mwaka 2012/13.

**Jedwali 15: Halmashauri ambazo hazikupata fedha**

| Na. | Halmashauri | Na. | Halmashauri |
|---|---|---|---|
| 1 | Manispaa ya Ilemela | 5 | Mji wa Masasi |
| 2 | Mji wa Geita | 6 | Jiji la Dar-Es-Salaam |
| 3 | Mji wa Kahama | 7 | Wilaya ya Busokeli |
| 4 | Mji wa Bariadi | 8 | Mji wa Makambako |

### 2.3.3 Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF)

Awamu ya pili ya Mfuko wa Maendeleo ya Jamii ilianzishwa tarehe 19/1/2003 baada ya kusainiwa kwa makubaliano kati ya Serikali ya Jamhuri ya Tanzania na Benki ya Dunia kupitia Shirikisho la Kimataifa la Maendeleo (IDA).

#### 2.3.3.1 Malengo ya Mradi

Awamu ya pili ya Mfuko wa Jamii (TASAF II) ilianzishwa kuwezesha jamii kupata fursa ya kuchangia kuboresha maisha ili kufikia malengo ya milenia katika mkakati wa kupunguza umaskini. TASAF II pia inalenga:

(i) Kusaidia uundwaji wa vikudi vya hiari vya kuweka na kukopa fedha.

(ii) Kutoa huduma kwa jamii ambayo itachangia upatikanaji wa huduma za msingi na hifadhi ya

mazingira unaofuata Mpango wa Maendeleo ya Milenia.

(iii) Kutoa nafasi za ajira kwa wasiojiweza, chakula kwa maskini na kuongeza kipato chao, ujuzi na nafasi za kazi kwa maafisa fedha wa vijiji.

(iv) Kutoa msaada kwa yatima, wasiojiweza, wazee na walioathirika wa virusi vya ukimwi waweze kujimudu kiuchumi.

### 2.3.3.2 Usimamizi wa Miradi

**(i) Kitaifa**

Awamu ya pili ya Mfuko wa Jamii (TASAF II) katika ngazi ya Taifa unasimamiwa na kitengo cha Usimamizi cha Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TMU) kinachoongozwa na Mkurugenzi Mtendaji. Kitengo hiki huratibu na kutekeleza shughuli za kila siku za Mfuko wa Jamii (TASAF II). Mkurugenzi Mtendaji huwajibika kwa Kamati ya Uongozi (NSC) kwa maswala yote ya utawala na fedha yanayohusu shughuli za Mfuko wa Jamii.

**(ii) Ngazi ya Halmashauri**

Katika ngazi ya Wilaya, Wakurugenzi Watendaji wa Wilaya (DED)/ Wakurugenzi watendaji wa Manispaa (MD) wakiwa ni watendaji wa Wilaya/Manispaa kwa uongozi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa, husaidia uendeshaji wa awamu ya pili ya Mfuko wa Jamii kwa kuwaongoza Waratibu wa fedha wa vijiji (VFC). Waratibu wa fedha wa vijiji huteuliwa na Baraza la Wilaya kutoka miongoni mwa watu wenye sifa katika Halmashauri/Manispaa kwa mujibu wa hadidu za rejea zitolewazo na Kitengo cha Uongozi cha TASAF. Waratibu wa fedha wa vijiji huratibu shughuli za awamu ya pili ya Mfuko wa Jamii katika ngazi ya wilaya kwa kuhamasisha na kuwezesha jamii katika maswala yanayohusu utekelezaji wa miradi midogo ya jamii. Mratibu wa fedha wa Kijiji anawajibika kwa kitengo cha Uongozi cha TASAF kwa niaba ya Mkurugenzi wa Halmashauri.

Kwa mujibu wa mwongozo wa kazi wa TASAF malengo ya kufanya ukaguzi ni kumwezesha Mdhibiti na Mkaguzi

Mkuu kutoa maoni huru juu ya taarifa za fedha za TASAF zilizoandaliwa kwa mwaka husika.

Ifuatayo ni orodha ya Halmashauri zilizokaguliwa katika mwaka wa fedha 2012/2013, aina ya hati za ukaguzi zilizotolewa pamoja na sababu za kutolewa kwa hati hizo.

**(a) Halmashauri zilizopata Hati Inayoridhisha**

Kati ya halmashauri mia na kumi (110) zilizokaguliwa ni halmashauri tisini na tano (95) sawa na asilimia 86.4 zilipata hati inayoridhisha kama zilivyoorodheshwa kwenye Jedwali Na.16 hapa chini:

**Jedwali 16: Halmashauri zilizopata hati inayoridhisha**

| Na. | Halmashauri | Na. | Halmashauri |
|---|---|---|---|
| 1 | Wilaya ya Geita | 46 | Wilaya ya Kondoa |
| 2 | Wilaya ya Bukoba | 47 | Wilaya ya Mpwapwa |
| 3 | Wilaya ya Biharamulo | 48 | Wilaya ya Iramba |
| 4 | Wilaya ya Misenyi | 49 | Wilaya ya Singida |
| 5 | Wilaya ya Muleba | 50 | Wilaya ya Kilolo |
| 6 | Wilaya ya Maswa | 51 | Wilaya ya Iringa |
| 7 | Wilaya ya Meatu | 52 | Wilaya ya Makete |
| 8 | Wilaya ya Bunda | 53 | Manispaa ya Iringa |
| 9 | Wilaya ya Musoma | 54 | Wilaya ya Mbeya |
| 10 | Wilaya ya Magu | 55 | Wilaya ya Mbarali |
| 11 | Wilaya ya Sengerema | 56 | Wilaya ya Rungwe |
| 12 | Wilaya ya Ukerewe | 57 | Wilaya ya Njombe |
| 13 | Wilaya ya Kishapu | 58 | Wilaya ya Ludewa |
| 14 | Manispaa ya Shinyanga | 59 | Wilaya ya Mbinga |
| 15 | Wilaya ya Shinyanga | 60 | Wilaya ya Songea |
| 16 | Wilaya ya Ngorongoro | 61 | Wilaya ya Mpanda |
| 17 | Wilaya ya Hai | 62 | Wilaya ya Kigoma |
| 18 | Wilaya ya Moshi | 63 | Wilaya ya Sikonge |
| 19 | Manispaa ya Moshi | 64 | Wilaya ya Tabora |
| 20 | Wilaya ya Rombo | 65 | Manispaa yaTabora |
| 21 | Wilaya ya Same | 66 | Wilaya ya Urambo |
| 22 | Wilaya ya Siha | 67 | Wilaya ya Igunga |
| 23 | Wilay ya Babati | 68 | Wilaya ya Monduli |
| 24 | Mji ya Babati | 69 | Wilaya ya Kibondo |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 25 | Wilaya ya Hanang | 70 | Manispaa ya Kigoma |
| 26 | Wilaya ya Kiteto | 71 | Wilaya ya Bahi |
| 27 | Wilaya ya Simanjiro | 72 | Wilaya ya Tunduru |
| 28 | Wilaya ya Handeni | 73 | Manispaa ya Songea |
| 29 | Mji ya Korogwe | 74 | Wilaya ya Ileje |
| 30 | Wilaya ya Lushoto | 75 | Wilaya ya Mufindi |
| 31 | Wilaya ya Mkinga | 76 | Wilaya ya Rufiji |
| 32 | Wilaya ya Muheza | 77 | Wilaya ya Mkuranga |
| 33 | Jiji la Tanga | 78 | Wilaya ya Mafia |
| 34 | Wilaya ya Liwale | 79 | Wilaya ya Kisarawe |
| 35 | Wilaya ya Kilwa | 80 | Mji ya Kibaha |
| 36 | Wilaya ya Lindi | 81 | Wilaya ya Kibaha |
| 37 | Manispaa ya Lindi | 82 | Wilaya ya Bagamoyo |
| 38 | Wilaya ya Nachingwea | 83 | Wilaya ya Tandahimba |
| 39 | Wilaya ya Ruangwa | 84 | Wilaya ya Newala |
| 40 | Wilaya ya Kilombero | 85 | Wilaya ya Nanyumbu |
| 41 | Wilaya ya Kilosa | 86 | Manispaa ya Mtwara Mikindani |
| 42 | Wilaya ya Morogoro | 87 | Wilaya ya Mtwara |
| 43 | Manispaa ya Morogoro | 88 | Wilaya ya Masasi |
| 44 | Wilaya ya Mvomero | 89 | Wilaya ya Ulanga |
| 45 | Wilaya ya Mwanga | | |

### (b) Halmashauri zilizopata hati inayotia shaka

Kati ya Halmashauri 104 zilizokaguliwa Halmashauri 13 sawa na asilimia 12.5 zilipata hati zinazotia shaka kama inavyoorodheshwa kwenye Jedwali Na.17 hapa chini:-

**Jedwali 17: Halmashauri zilizopata hati inayotia shaka**

| Na. | Halmashauri |
|---|---|
| **1** | **Wilaya ya Rorya** |
| | • Matumizi yenye thamani ya Sh.20,040,000 yalilipiwa kwenye vifungu visivyostahili kinyume na Agizo Namba 23(1) la Memoranda ya Fedha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa mwaka 2009. |

| | |
|---|---|
| **2** | **Wilaya ya Misungwi** |
| | • Matumizi ya kawaida yalikuwa pungufu kwa Sh.23,131,729 katika taarifa ya utendaji wa kifedha ikilinganishwa na mwaka uliopita. Bakaa ya misaada kwa matumizi ya kawaida kwa mwaka wa fedha 2011/12 ni Sh.27,436,710 ikilinganishwa nakiasi cha Sh.4,304,981 kilicho onyeshwa kwennye taarifa za mwaka wa fedha 2012/13.<br>• Kiasi cha Sh.10,102,463 kilionyeshwa kama ruzuku kwa mwaka huu lakini katika uhalisia halmashauri haijapokea fedha yoyote kwa mwaka wa fedha 2012/13, kwa ajili ya shughuli za TASAF.<br>• Bakaa ya fedha kutoka taasisi zingine wakati wa kufunga mwaka wa fedha 2011/12 ilikuwa ni Sh.343,695,153 lakini bakaa anzia kwa mwaka wa fedha 2012/13 ni Sh.366,826,882 hii imesababisha ongezeko katika hamisho toka taasisi zingine kwa kiasi cha Sh.23,131,729. |
| **3** | **Jiji la Mwanza** |
| | • Maelezo ya taarifa za fedha kwa mwaka 2012/13 yalionyesha kuwa Sh.351,395,763 ni ongezeko la mali, kati ya hizo Sh.330,012,460 ni kwa ajili ya majengo na Sh.21,383,303 kwa ajili ya kazi zinazoendelea. Hata hivyo hakuna vielelezo vya ushahidi wa mali ya nyongeza ya Sh.351,395,763. Hii imesababisha ugumu katika kutambua gharama ya kila aina ya mali, na uhalali wa umiliki wa mali hizo. |
| **4** | **Wilaya ya Karatu** |
| | • Hati za malipo ya Sh.2,070,000 hazikuwa na viambatanisho vinavyoonyesha uhalali wa malipo hayo, kinyume na Agizo namba 8(2)(c) la LAFM, 2009. |
| **5** | **Wilaya ya Longido** |
| | • Hati za malipo ya Sh.234,955,721 hazikuwa na viambatanisho vinavyoonyesha uhalali wa malipo hayo, kinyume na Agizo Na. 8(2)(c) la LAFM, 2009. |

| | |
|---|---|
| **6** | **Wilaya ya Mbulu** |
| | • Halmashauri imepokea Sh.116,260,074 kwa ajili ya shughuli za TASAF. Hata hivyo halmashauri imeonyesha fedha hizi kama ruzuku kwa ajili ya matumizi ya kawaida katika rejea namba 1, kwa upande mwingine kiasi hicho hicho kimeonyeshwa kama fedha zilizopokelewa kwa ajili ya matumizi ya maendeleo, hii imesababisha zidisho katika jumla ya fedha zilizo pokelewa. |
| **7** | **Wilaya ya Kilindi** |
| | • Halmashauri imekokotoa kiwango cha uchakavu zaidi kwa Sh.11,166,257.84 kutokana na kutumia viwango tofauti na vile vilivyoainishwa katika halmashauri na imesababisha taarifa ya utendaji kutokuwa sahihi.<br>• Upungufu katika mapato ya ruzuku kwa kiasi cha Sh.6,048,765. |
| **8** | **Wilaya ya Korogwe** |
| | • Hakukuwa na viambatanisho vya mali, mitambo na vifaa ya kiasi cha Sh.714,024,724 kinyume na Kifungu Na. 31(6)(b) cha LAFM, 2009. |
| **9** | **Wilaya ya Pangani** |
| | • Limbikizo la bakaa lilizidi kuliko ilivyotakiwa kutokana na kukosewa kuchukuliwa kwa bakaa la mwaka uliotangulia kwa kiasi cha Sh.29,181,578. |
| **10** | **Wilaya ya Namtumbo** |
| | • Taarifa ya fedha ya mizania inaonyesha kuwa mali za kudumu kiasi cha Sh.22,906,906 hazikuwa na maelezo ya rejea kinyume na mwongozo wa viwango vya kihasibu vya kimataifa katika sekta ya Umma. |
| **11** | **Manispaa ya Arusha** |
| | • Malipo ya Sh.23,966,000 hayakuwa na nyaraka za malipo pamoja na viambatanishi, hivyo uhalali wa malipo hayo haukuweza kuthibitishwa. |

| | |
|---|---|
| 12 | **Wilaya ya Arusha** |
| | • Malipo ya kiasi cha Sh.34,628,349 hayakuwa na viambatanishi kinyume na Agizo Na. 8(2)(c) la LAFM, 2009. |
| 13 | **Wilaya ya Meru** |
| | • Halmashauri ilipokea fedha kiasi cha Sh.20,636,250 ila fedha hizo hazijaorodheshwa kwenye daftari la taarifa ya fedha kinyume na kifungu namba 3.2 Mwongozo wa Kihasibu wa Serikali za Mitaa.<br>• Katika kipindi cha mwaka wa fedha halmashauri ilitoa fedha kiasi cha Sh.32,613,968.92 kwa utendaji wa shughuli za TASAF, mpaka wakati wa ukaguzi hakukuwa na taarifa za mrejesho wa utendaji wa shughuli hizo. Hii inatia mashaka huenda fedha hizi zimetumika kwa matumizi yasiyokusudiwa. |

**(c) Halmashauri zilizopata hati mbaya**

Halmashauri mbili sawa na asilimia 2 kati ya Halmashauri 110 zilizokaguliwa zilipata hati mbaya kama inavyoonekana kwenye Jedwali Na.18 hapa chini:

**Jedwali 18: Halmashauri zilizopata hati mbaya**

| | **Halmashauri** |
|---|---|
| 1 | **Manispaa ya Singida** |
| | • Taarifa za fedha za mwaka wa fedha 2012/13 hazikuwasilishwa kwa ajili ya ukaguzi. |
| 2 | **Wilaya ya Bariadi** |
| | • Halmashauri haikuandaa taarifa za fedha. |

**(d) Halmashauri ambazo hazikupata fedha**

Halmashauri 30 kati ya Halmashauri 140 hazikupokea fedha kutokana na sababu zifuatazo:

- Mradi wa TASAF II ulimalizika 2011/12, ni halmashauri zile zilizokuwa na bakaa tu ndizo zilizoendelea na utekelezaji wa miradi iliyokuwa imebakia mwaka 2012/13.
- Halmashauri nyingine ni mpya bado hazijaanza shughuli zote rasmi, kama zinavyoorodheshwa kwenye jedwali Na.19 hapo chini:

**Jedwali 19: Halmashauri ambazo hazikukaguliwa, 2012/2013**

| Na. | Halmashauri | Na. | Halmashauri |
|---|---|---|---|
| 1 | Wilaya ya Bukombe | 16 | Wilaya ya Mbozi |
| 2 | Mji wa Bariadi | 17 | Wilaya ya Busokeli |
| 3 | Manispaa ya Musoma | 18 | Wilaya ya Sumbawanga |
| 4 | Wilaya ya Serengeti | 19 | Manispaa ya Sumbawanga |
| 5 | Manispaa ya Ilemela | 20 | Wilaya ya Nkasi |
| 6 | Wilaya ya Kahama | 21 | Jiji la Dar es salaam |
| 7 | Mji wa Kahama | 22 | Manispaa ya Bukoba |
| 8 | Manispaa ya Ilala | 23 | Wilaya ya Karagwe |
| 9 | Manispaa ya Kinondoni | 24 | Wilaya ya Ngara |
| 10 | Manispaa ya Temeke | 25 | Wilaya ya Tarime |
| 11 | Manispaa ya Chunya | 26 | Mji wa Geita |
| 12 | Wilaya ya Kyela | 27 | Wilaya ya Singida |
| 13 | Jiji la Mbeya | 28 | Wilaya ya Chato |
| 14 | Mji wa Masasi | 29 | Wilaya ya Kasulu |
| 15 | Mji wa Njombe | 30 | Mji wa Mpanda |

### 2.3.4 Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji (WSDP)

**Utangulizi**

Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji ulibuniwa ili kuangalia mapungufu katika miundombinu ya maji mijini na vijijini, kuboresha rasilimali za usimamizi wa maji na hasa kuimarisha usimamizi wa ofisi za mabonde tisa (9) na taasisi za sekta zinazohusika na kuzijengea uwezo.

Mwaka 2002, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilitengeneza sera ya taifa ya maji, ikiwa na malengo ya kuwa na mkakati kabambe wa kitaifa na endelevu wa kuimarisha maendeleo na usimamizi katika rasilimali za maji. Hii itahakikisha mamlaka halali zinakuwepo ili kusimamia utekelezaji.

Mikakati ya kitaifa ya maendeleo ya sekta ya maji (NWSDS) imeonyesha jinsi wizara husika itakavyotekeleza Sera ya Taifa ya Maji ili kufikia malengo ya Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kuondoa Umaskini Tanzania (MKUKUTA). Hii itakuwa ni mwongozo katika kuweka mipango ya muda wa kati na muda

mfupi. Kwa maeneo mengine itatoa mwongozo katika kuunganisha mpango wa taifa wa maendeleo ya sekta ya maji na programu ya maendeleo ya sekta ya maji kama nyenzo katika kuandaa malengo ya muda wa kati na mrefu.

Wizara ya Maji imetayarisha Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji kwa kipindi cha mwaka 2006 hadi 2025; ambayo imejumuisha programu za kisekta tatu ambazo ni: (1) usimamizi wa rasilimali za maji (2) mradi wa usambazaji maji vijijini (3) mradi wa maji safi na majitaka mijini. Programu pia inajumuisha kuimarisha na kujenga uwezo wa taasisi zinazosimamia na kuhakikisha utekelezaji wa mradi wa sekta ya maji unafanikiwa.

Orodha ya watekelezaji wa programu ya maendeleo ya sekta ya maji waliokaguliwa katika mwaka wa fedha wa 2012/13, na matokeo ya ukaguzi wameorodheshwa hapa chini:

**(a) Watekelezaji wa programu ya maendeleo ya sekta ya maji waliopata hati zinazoridhisha**

Watekelezaji wa programu ya maendeleo ya sekta ya maji 119 wamepata hati inayoridhisha ambao ni sawa na 89.2% ya watekelezaji wote waliokaguliwa kama inavyoonekana kwenye jedwali Na. 20 hapo chini:

**Jedwali 20: Watekelezaji wa programu ya maendeleo ya sekta ya maji waliopata hati zinazoridhisha**

| Na | Watekelezaji | Na. | Watekelezaji |
|---|---|---|---|
| 1 | Akaunti Kuu ya Mradi Hazina | 61 | Wilaya ya Rorya |
| 2 | Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii | 62 | Wilaya ya Serengeti |
| 3 | Wizara ya Maji na Umwagiliaji | 63 | Wilaya ya Tarime |
| 4 | Manispaa ya Shinyanga | 64 | Wilaya ya Kwimba |
| 5 | Jiji la Tanga | 65 | Wilaya ya Magu |
| 6 | Wilaya ya Bahi | 66 | Wilaya ya Misungwi |
| 7 | Manispaa ya Dodoma | 67 | Wilaya ya Kahama |
| 8 | Wilaya ya Kondoa | 68 | Wilaya ya Kishapu |
| 9 | Wilaya ya Kongwa | 69 | Wilaya ya Maswa |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 10 | Wilaya ya Kibondo | 70 | Wilaya ya Meatu |
| 11 | Wilaya ya Kigoma | 71 | Jiji la Arusha |
| 12 | Manispaa ya Kigoma | 72 | Wilaya ya Arusha |
| 13 | Wilaya ya Iramba | 73 | Wilaya ya Babati |
| 14 | Wilaya ya Manyoni | 74 | Mji wa Babati |
| 15 | Wilaya ya Singida | 75 | Wilaya ya Hai |
| 16 | Manispaa ya Singida | 76 | Wilaya ya Hanang' |
| 17 | Wilaya ya Nzega | 77 | Wilaya ya Handeni |
| 18 | Wilaya ya Sikonge | 78 | Wilaya ya Kilindi |
| 19 | Wilaya ya Tabora | 79 | Wilaya ya Kiteto |
| 20 | Wilaya ya Urambo | 80 | Mji wa Korogwe |
| 21 | Wilaya ya Kilwa | 81 | Wilaya ya Longido |
| 22 | Wilaya ya Lindi | 82 | Wilaya ya Lushoto |
| 23 | Manispaa ya Lindi | 83 | Wilaya ya Mbulu |
| 24 | Wilaya ya Liwale | 84 | Wilaya ya Monduli |
| 25 | Wilaya ya Nachingwea | 85 | Wilaya ya Moshi |
| 26 | Jiji la Mbeya | 86 | Manispaa ya Moshi |
| 27 | Wilaya ya Kilombero | 87 | Wilaya ya Muheza |
| 28 | Wilaya ya Kilosa | 88 | Wilaya ya Mwanga |
| 29 | Wilaya ya Morogoro | 89 | Wilaya ya Ngorongoro |
| 30 | Manispaa ya Morogoro | 90 | Wilaya ya Pangani |
| 31 | Wilaya ya Mvomero | 91 | Wilaya ya Rombo |
| 32 | Wilaya ya Ulanga | 92 | Wilaya ya Same |
| 33 | Wilaya ya Masasi | 93 | Wilaya ya Siha |
| 34 | Wilaya ya Mtwara | 94 | Wilaya ya Simanjiro |
| 35 | Manispaa ya Mtwara | 95 | Manispaa ya Iringa |
| 36 | Wilaya ya Nanyumbu | 96 | Wilaya ya Makete |
| 37 | Wilaya ya Newala | 97 | Wilaya ya Iringa |
| 38 | Wilaya ya Tandahimba | 98 | Wilaya ya Kilolo |
| 39 | Wilaya ya Bagamoyo | 99 | Wilaya ya Ludewa |
| 40 | Wilaya ya Kibaha | 100 | Wilaya ya Mufindi |
| 41 | Mji wa Kibaha | 101 | Wilaya ya Mpanda |
| 42 | Wilaya ya Kisarawe | 102 | Mji wa Mpanda |
| 43 | Wilaya ya Mafia | 103 | Wilaya ya Kyela |
| 43 | Wilaya ya Mafia | 103 | Wilaya ya Kyela |
| 44 | Wilaya ya Mkuranga | 104 | Wilaya ya Mbarali |
| 45 | Wilaya ya Rufiji | 105 | Wilaya ya Ileje |
| 46 | Manispaa ya Ilala | 106 | Wilaya ya Njombe |
| 47 | Manispaa ya Kinondoni | 107 | Mji wa Njombe |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 48 | Manispaa ya Temeke | 108 | Wilaya ya Nkasi |
| 49 | Wilaya ya Biharamulo | 109 | Wilaya ya Sumbawanga |
| 50 | Wilaya ya Bukoba | 110 | Wilaya ya Mbinga |
| 51 | Manispaa ya Bukoba | 111 | Wilaya ya Namtumbo |
| 52 | Wilaya ya Karagwe | 112 | Wilaya ya Songea |
| 53 | Wilaya ya Missenyi | 113 | Manispaa Songea |
| 54 | Wilaya ya Muleba | 114 | Wilaya ya Tunduru |
| 55 | Wilaya ya Ngara | 115 | Wilaya ya Rungwe |
| 56 | Wilaya ya Bukombe | 116 | Wilaya ya Ruangwa |
| 57 | Wilaya ya Chato | 117 | Wilaya ya Mpwapwa |
| 58 | Wilaya ya Geita | 118 | Manispaa ya Tabora |
| 59 | Wilaya ya Bunda | 119 | Wilaya ya Igunga |
| 60 | Wilaya Musoma | | |

**(b) Watekelezaji wa programu ya maendeleo ya sekta ya maji waliopata hati yenye shaka**

Watekelezaji 11 wamepata hati ya ukaguzi yenye shaka ambao ni sawa na 8.3% ya watekelezaji wote waliokaguliwa kama inavyoonyeshwa kwenye jedwali Na.21 hapo chini:

**Jedwali 21: Watekelezaji waliopata hati yenye shaka**

| Na. | Watekelezaji |
|---|---|
| 1 | **Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino** |
| | • Matumizi ya ziadi ya Sh.14,121,242.<br>• Matumizi ya kiasi cha Sh.42,578,240 yalilipwa kwa kutumia vifungu visivyohusika. |
| 2 | **Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema** |
| | • Kiasi cha ruzuku ya maendeleo kilichoonyeshwa kilikosewa kwa kupunguzwa kwa Sh.41,510,000 ukilinganisha na mwaka uliopita.<br>• Fedha za ruzuku kwa ajili ya matumizi ya kawaida yaliongezwa kwa makosa kwa kiasi cha Sh.23,898,000. |
| 3 | **Halmashauri ya Wilaya ya Ukerewe** |
| | • Taarifa za ulinganifu za mwaka wa fedha uliopita zilionyeshwa kimakosa katika taarifa za fedha za mwaka 2012/13.<br>• Malipo ya Sh.3,815,000 yalilipwa kwa kutumia vifungu visivyohusika. |

| Na. | Watekelezaji |
|---|---|
| 4 | **Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga** |
| | • Matumizi yaliyofanywa bila ya kuwepo katika mpango Sh.251,268,770.<br>• Hati za malipo ya Sh.88,229,100 zilikuwa na nyaraka pungufu. |
| 5 | **Halmashauri ya Wilaya ya Bariadi** |
| | • Hati za malipo ya Sh.250,728,142 hazikuwasilishwa kwa ajili ya ukaguzi. |
| 6 | **Halmashauri ya Wilaya ya Karatu** |
| | • Kulikuwa na upungufu wa kiasi cha Sh.63,279,819 katika Mali, Mitambo na Vifaa<br>• Hati za malipo ya Sh.84,318,624 zilikuwa na nyaraka pungufu. |
| 7 | **Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe** |
| | • Mali, Mitambo na Vifaa vya thamani ya Sh.722,845,518.24 havikuthibitishwa.<br>• Hati za malipo ya Sh.18,762,000 zilikuwa na nyaraka pungufu. |
| 8 | **Halmashauri ya Wilaya ya Meru** |
| | • Hati za malipo ya Sh.30,925,421 zilikuwa na nyaraka pungufu.<br>• Hati za malipo ya Sh.4,160,000 hazikuwasilishwa kwa ajili ya ukaguzi. |
| 9 | **Halmashauri ya Wilaya ya Mkinga** |
| | • Fedha zilizopokelewa zilionyeshwa kwa kiasi kikubwa zaidi kwa Sh.29,840,546 katika taarifa ya fedha. |
| 10 | **Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya** |
| | • Malipo ya Sh.10,076,892 ya posho na mafuta yalizidi kiasi kilichoidhinishwa katika bajeti.<br>• Taarifa ya matumizi ilionyeshwa kwa makosa kwa upungufu wa kiasi cha Sh.144,736,007.<br>• Taarifa ya utendaji wa fedha haikuonyesha fedha zilizolipwa kwa ajili ya posho, mshahara na stahiki za watumishi kiasi cha Sh.29,595,000. |

| Na. | Watekelezaji |
|---|---|
| 11 | **Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu** |
| | • Salio anzia lililoonyeshwa kwa makosa katika taarifa ya fedha kwa upungufu wa Sh.110,888,731.<br>• Kiasi cha fedha kilichoonyeshwa katika taarifa ya mtiririko wa fedha kilikuwa ni zaidi kwa Sh.63,209,2300.<br>• Hakukuwa na taarifa ya ulinganifu baina ya fedha zilizoidhinishwa katika bajeti na kiasi halisi. |

**(c) Watekelezaji wa programu ya maendeleo ya sekta ya maji waliopata hati isiyoridhisha**

Watekelezaji watatu (3) wamepata hati ya ukaguzi isiyoridhisha, hii ni sawa na asilimia mbili nukta mbili (2.2%) ya watekelezaji wote waliokaguliwa kama inavyooneshwa kwenye jedwali Na.22 hapo chini:

**Jedwali 22: Watekelezaji wa programu ya maendeleo ya sekta ya maji waliopata hati isiyoridhisha**

| Na. | Watekelezaji wa WSDP |
|---|---|
| 1 | **Halmashauri ya wilaya ya Chunya** |
| | • Matumizi mabaya ya fedha za mradi wa maji kiasi cha Sh.226,559,557.53 kutoka katika akaunti ya maendeleo ya halmashauri.<br>• Matumizi yaliyofanywa nje ya bajeti Sh.8,555,000.<br>• Malipo ya kiasi cha Sh.11,905,300 yalikuwa na nyaraka pungufu. |
| 2 | **Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga** |
| | • Matumizi ya fedha za ruzuku kwa ajili ya shughuli za kawaida yalionyeshwa katika taarifa ya utendaji wa fedha kama Sh.200,000,000 wakati kidokezo namba II kilionyesha Sh.291,035,312.14.<br>• Taarifa za kiutendaje haikuainisha kiasi cha ruzuku ya maendeleo ambayo ilionyeshwa kwenye kidokezo Na. 27 kuwa Sh. 73,733,199.39.<br>• Fedha za ruzuku kwa ajili ya miradi ya maendeleo zimeonyeshwa ni Sh.200,000,000 katika taarifa ya mtiririko wa fedha, wakati kidokezo Na. 37 kimeonesha Sh.269,219,491.53 na hivyo kuleta |

| Na. | Watekelezaji wa WSDP |
|---|---|
| | tofauti ya Sh.69,219,491.53.<br>• Fedha zilizotumika kwa ajili ya shughuli za maendeleo kama ilivyoonyeshwa katika taarifa ya mtiririko wa fedha ni Sh.261,820,311.06 wakati kidokezo namba 37 kimeonyesha Sh.38,357,874.96. Pia ongezeko la Mali, Mitambo na Vifaa katika kidokezo namba 27 kimeonyesha Sh.400,829,369 hivyo kutia mashaka ya usahihi wake. |
| **3** | **Halmashauri ya Jiji la Mwanza** |
| | • Ongezeko la fedha za ruzuku kwa ajili ya shughuli za maendeleo Sh.226,800,123 halikuonyeshwa kwa usahihi katika taarifa ya mtiririko wa fedha.<br>• Fedha za ruzuku kwa ajili ya shughuli za kawaida Sh.28,813,953 hazikuonyeshwa kwa usahihi katika taarifa ya mtiririko wa fedha.<br>• Malipo ya Sh.2,544,000 ya miaka ya nyuma yalilipwa bila kuwepo katika bajeti iliyoidhinishwa.<br>• Malipo batili kwa kutumia dola za marekani badala ya shilingi za Tanzania yaliyoisababishia hasara halmashauri ya Sh.30,397,626 iliyotokana na badiliko la viwango vya kubadilisha fedha. |

**(d) Watekelezaji programu ya maendeleo ya sekta ya maji waliopata hati mbaya**

Mtekelezaji mmoja (1) tu ndiye amepata hati ya ukaguzi mbaya ambayo ni sawa na asilimia 0.8 ya watekelezaji wote waliokaguliwa kwa mwaka 2012/13, kama inavyoonekana kwenye jedwali Na. 23 hapo chini:

**Jedwali 23: Mtekelezaji wa programu ya maendeleo ya sekta ya maji aliyepata hati mbaya**

| Na. | Mtekelezaji |
|---|---|
| **1** | **Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi** |
| | • Halmashauri haikuandaa na kuwasilisha taarifa za fedha za mradi wa maji kwa mwaka wa fedha 2012/13 kwa ajili ya ukaguzi. |

**(e) Halmashauri ambazo hazikupewa fedha za programu ya maendeleo ya sekta ya maji**

Halmashauri tisa (9) hazikupewa fedha kwa ajili ya kutekeleza programu ya maendeleo ya sekta ya maji kwa mwaka wa fedha 2012/13 kama inavyoonekana kwenye jedwali Na.24 hapo chini:

**Jedwali 24: Halmashauri ambazo hazikupewa fedha za programu ya maendeleo ya sekta ya maji**

| Na. | Halmashauri |
|---|---|
| 1 | Manispaa ya Musoma |
| 2 | Jiji la Dar es salaam |
| 3 | Wilaya ya Makambako |
| 4 | Wilaya ya Busokeli |
| 5 | Manispaa ya Ilemela |
| 6 | Mji wa Geita |
| 7 | Mji wa Kahama |
| 8 | Mji wa Bariadi |
| 9 | Mji wa Masasi |

### 2.3.5 Miradi Mingine ya Maendeleo

Idadi ya miradi ya maendeleo iliyokaguliwa ni mia moja na mbili (102) ikijumuisha miradi inayofadhiliwa na Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika, Miradi inayofadhiliwa na Mfuko wa Kimataifa wa Kupambana na Ukimwi, Kifua Kikuu na Ukoma, Programu ya Maendeleo ya Umoja wa Mataifa na kadhalika.

Muhtasari wa hati za ukaguzi zilizotolewa kwa miradi ya Maendeleo na sababu ya kutoa hati hizo imeonyeshwa kwenye Jedwali Na. 25 na 26 hapa chini:

**Jedwali 25: Hati inayoridhishana isiyokuwa na mambo ya msisitizo**

| Na. | Jina la Mradi |
|---|---|
| 1 | Mradi wa Ongezeko wa Usalama wa Chakula (AFS) |
| 2 | Mradi wa Rasilimali/ Kitega Uchumi Wilayani Sekta ya Kilimo (DASIP) |
| 3 | Mradi wa Uzalishaji katika Kilimo Afrika ya Mashariki (EAAPP) |

| | |
|---|---|
| 4 | Haki ya Mfuko wa Maendeleo wa Upandikizaji (PBRDF) |
| 5 | SIDA/NORAD/MEM - Mradi wa Nishati ya Mimea (BIOFUEL) |
| 6 | Mradi wa Maendeleo wa Gesi Asilia |
| 7 | Wakala wa Nishati Vijijini-Mradi wa Maendeleo(WB REA) |
| 8 | Mradi wa Usimamizi na Uendelevu wa Rasilimali za Madini (SMMRP) |
| 9 | Mradi wa maendeleo ya Nishati Tanzania-Wizara ya Madini na Nishati (TEDAP) |
| 10 | Mradi wa Ubunifu Uliowazi katika Tasinia ya Uchimbaji Madini Tanzania -(TEITI) |
| 11 | Mradi wa Maendeleo Huduma za Msingi za Afya – Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii |
| 12 | Mradi wa Mtandao wa Maabara za Afya ya Umma Africa Mashariki |
| 13 | Mradi wa Kuimarisha Ufuatiliaji na Utathmini wa Taarifa (MESI) |
| 14 | Mradi wa Kuhifadhi Chakula vijijini (RFFP) |
| 15 | Mradi wa Kupunguza Vifo vya Wajawazito |
| 16 | Arusha-Namanga –Mradi wa Barabara |
| 17 | Mradi wa Kusaidia Sekta ya Barabara -DANIDA |
| 18 | Mradi wa Kusaidia Sekta ya Barabara (RSSP1) |
| 19 | Singida - Babati - Minjingu -Mradi wa Barabara |
| 20 | Mfuko wa Belgium kwa Usalama wa Chakula |
| 21 | Programu ya kuendeleza Eneo la Ziwa Tanganyika |
| 22 | Programu ya Masoko, Miundombinu, Ongezeko la Dhamani na Msaada wa Fedha Vijijini (MIVARF) |
| 23 | Programu ya Maboresho katika Utumishi wa Umma (II) |
| 24 | Mradi wa Maendeleo Huduma za Msingi za Afya – Tawala za mikoa na Serikali za Mitaa |
| 25 | Programu ya Usambazaji wa Maji Vijijini na Usafi wa Mazingira - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (RWSSP) |
| 26 | Dar-Isaka-Kigali/Keza-Gitega-Musongati Mradi wa Reli |
| 27 | Mradi wa Usimamizi wa Mazingira wa Ziwa Victoria (LVEMP II) |
| 28 | Programu ya Maboresho ya Sheria |

| | |
|---|---|
| 29 | Halmashauri ya Wilaya ya Magu - UNDP |
| 30 | Chuo kikuu Dar-es-Salaam- Kurugenzi ya Uchumi-UNDP |
| 31 | Ofisi ya Taifa ya Twakinu - UNDP |
| 32 | Wizara ya Afya na Usitawi wa Jamii - UNDP |
| 33 | Baraza la Taifa la Watu Wanaoishi na Virusi vya Ukimwi - UNDP |
| 34 | Ofisi ya Rais, Fedha na Uchumi –Zanzibar - UNDP |
| 35 | Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa - UNDP |
| 36 | Halmashauri ya Wilaya ya Hai- UNDP |
| 37 | Tume ya Mipango Ofisi ya Rais - UNDP |
| 38 | Wizara ya Maendeleo ya Jamii Jinsia na Watoto-UNDP |
| 39 | Mpango wa Kuwezesha vyombo vya Sheria – Baraza la Wawakilishi Zanzibar - UNDP |
| 40 | Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania - UNDP |
| 41 | Chama cha Msalaba Mwekundu - UNDP |
| 42 | Wizara ya Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Maendeleo ya Watoto-Zanzibar Mradi wa Kisheria Utekelezaji wa Sheria za Jinsia na Sera- UNDP |
| 43 | Katibu Tawala wa Mikoa wa Kilimanjaro - UNDP |
| 44 | Mpango wa Kuwezesha Vyombo vya Sheria – Bunge la Jamuhuri- UNDP |
| 45 | Tume ya Kudhiditi Ukimwi Tanzania- UNDP |
| 46 | Kuimarisha na Kukinga Mtandao wa Maeneo Kusini mwa Tanzania-UNDP |
| 47 | Mradi wa Mabasi yaendao kasi Mkoa wa Dar-es-salaam |
| 48 | Mradi wa Ubunifu Ulio wazi katika Tasinia ya Uchimbaji MadiniTanzania-(TEITI)-(Grant No. 12532) |
| 49 | Awamu ya Pili ya Mradi wa Usafirishaji Kanda ya Kati (SCTC) |
| 50 | Miradi ya Kusaidia Sekta ya Usafirishaji (TSSP) |
| 51 | Mradi wa Usimamizi wa Bahari na Pwani-IDA |
| 52 | Mradi wa Usimamizi wa Bahari na Pwani-GEF |
| 53 | Mpango wa Uhifadhi (ASP) |
| 54 | Mradi wa Kukuza Kilimo Kusini mwa Tanzania |

| | |
|---|---|
| | (SAGCOT) |
| 55 | Mradi wa Ushindanishi Sekta Binafsi – I (PSCP) |
| 56 | Mradi wa Ushindanishi Sekta Binafsi – II (PSCP) |
| 57 | Programu ya Kanda Miundombinu ya Mawasiliano |
| 58 | Mradi wa Habari Jamii na Maendeleo katika TEHAMA |
| 59 | Mradi wa Kuboresha Miji Tanzania-(TSCP- PMO RALG) |
| 60 | Wakala wa Uwezeshaji Usafiri Kanda ya Kati (CCTTFA) |
| 61 | Mradi wa Sayansi na Teknonolojia Elimu ya Juu |
| 62 | Mradi wa Uchambuzi na Utetezi wa sera –Tawala za Mikoa na serikali za Mitaa -UNICEF |
| 63 | Mradi wa Kukopesha Wajasiriamali wadogo Awamu ya II |
| 64 | Mradi wa Mpango Mkuu wa TakwimuTanzania |
| 65 | Mradi wa Maendeleo ya Biashara na Usafirishaji Kanda ya Afrika ya Mashariki –TPA |
| 66 | Mradi wa Maendeleo ya Biashara na Usafirishaji Kanda ya Afrika ya Mashariki–'SUMATRA' |
| 67 | Mradi wa Maendeleo wa Upatikanaji na Upanuzi wa Nishati Tanzania (TEDAP) –TANESCO |
| 68 | Mfuko Mkuu katika kutoa msaada sekta ya fedha |
| 69 | Mfuko Mkuu wa Kufadhili Makazi –Mfuko wa Pamoja |
| 70 | Mfuko Mkuu –Ukimwi |
| 71 | Mfuko Mkuu –Maendeleo ya Serikali za Mitaa na Tawala za Mikoa |
| 72 | Mfuko Mkuu sekta ya Sheria |
| 73 | Mfuko Mkuu wa Kitaifa wa Usambazaji Maji Safi Vijijini |
| 74 | Mfuko Mkuu -Mpango wa elimu shule za Msingi |
| 75 | Mfuko Mkuu –Mpango wa Maboresho na Usimamizi wa fedha |
| 76 | Mfuko Mkuu wa Sera ya rasilimali watu ya Mpango wa Maendeleo, Kuendeleza Sekta ya Kilimo |
| 77 | Mfuko Mkuu wa Mradi wa Mpango wa Kufuatilia Umaskini (Project Basket Fund ) |
| 78 | Mfuko Mkuu – Kuchangia Bajeti Kupunguza Umaskini |
| 79 | Mfuko Mkuu- Maboresho katika Sekta ya umma |

| | |
|---|---|
| 80 | Mfuko Mkuu programu ya maendeleo shule za Sekondari |
| 81 | Mfuko mkuu wa STATCAP |
| 82 | Mfuko Mkuu maboresho ya kisasa ya ukusanyaji kodi |
| 83 | Tume ya taifa ya kudhiditi ukimwi -Tanzania - Mfumo wa Taifa wa sekta mbalimbali |
| 84 | Programu ya kusaidia sekta ya Afya Sehemu ya 3- kusaidia mwitikio wa sekta mbalimbali shirikishi na VVU/Ukimwi unayotekelezwa na Tume ya Taifa ya kudhibiti Ukimwi -Tanzania |
| 85 | Programu ya maendeleo shule za Msingi |
| 86 | Programu ya Usimamizi wa fedha na Maboresho awamu ya nne (PFMRP) |
| 87 | Mradi wa kitaifa wa sekta mbalimbali na Mkakati shirikishi katika Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa |
| 88 | Mradi wa kusaidia Sekta ya Afya - Tawala za Mikoa na Serikali za mitaa |
| 89 | Mradi wa Kuboresha Miundombinu ya Afya, ADF Loan NumberF/TAN/HEA (-1)-REH/98/26 |
| 90 | Mfuko wa Kimataifa wa Kupambana na Ukimwi, Kifua Kikuu na Malaria- Mfuko Mkuu -Hazina |
| 91 | Mfuko wa Kimataifa wa Kupambana na Ukimwi, Kifua Kikuu na Malaria –Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii |
| 92 | Mfuko wa Kimataifa wa Kupambana na Ukimwi, Kifua Kikuu na Malaria Mzunguko wa nane Akaunti fedha za kigeni Benki kuu |
| 93 | Mfuko wa Kimataifa wa Kupambana na Ukimwi, Kifua Kikuu na Malaria- Programu ya Kitaifa ya Kudhibiti Ukimwi |
| 94 | Ufuatiliaji na tathmini ya Mfuko wa Kimataifa wa Kupambana na Ukimwi, Kifua Kikuu na Malaria mzunguko wa nane-Wizara ya Afya na Ustawi Wa Jamii |
| 95 | Uimarishaji Mfumo wa Afya- Mfuko wa Kimataifa wa Kupambana na Ukimwi, Kifua Kikuu na Malaria mzunguko wa Tisa (9) |
| 96 | Mfuko wa Kimataifa wa Kupambana na Ukimwi, Kifua Kikuu na Malaria -Ofisi ya Waziri Mkuu |

| | |
|---|---|
| | Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa |
| 97 | Mfuko wa Kimataifa wa Kupambana na Ukimwi, Kifua Kikuu na Malaria -Tume ya Kudhiditi Ukimwi Tanzania |
| 98 | Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Afya- Mwanza - Mfuko wa Kimataifa wa Kupambana na Ukimwi, Kifua Kikuu na Malaria Mzunguko wa Tisa (9) |
| 99 | Mfuko wa Kimataifa wa Kupambana na Ukimwi, Kifua Kikuu na Malaria - Kitengo cha Uchunguzi wa Magonjwa |

**Jedwali 26: Miradi Mitatu (3) iliyopata hati yenye shaka**

| Na | Jina la Mradi |
|---|---|
| **1** | **Wizara ya Afya – Zanzibar - UNDP** |
| | • Kiasi cha Sh.32,774,000 hakikuwa na nyaraka za kuthibitisha uhalali wa malipo.<br>• Kiasi cha Sh.100,423,100 kilipokelewa na wizara lakini hakikutumika kwa kipindi cha mwaka husika hata hivyo hakikurudishwa kwenye mfuko wa Shirika la Afya Duniani. Aidha hakuna ushahidi kuwa idhini ilitolewa kwa ajili ya kupelekwa kiasi hicho mwaka wa fedha unaofuata.<br>• Kiasi cha Sh.7,045,000 kilitumika kwa ajili ya ukarabati wa maeneo mawili ya mazoezi kwa vitendo kwa wauguzi na wakunga wanafunzi, matumizi haya hayahusiani na mradi.<br>• Kiasi cha Sh.9,068,472 kilikosa maelezo, ikiwa ni tofauti iliyopo kati ya kitabu cha fedha na taarifa ya mapato na matumizi kwa ajili ya mradi wa UNICEF. |
| **2** | **Chama cha Kutetea Haki za Watoto -UNDP** |
| | • Zabuni za manunuzi za kiasi cha Sh.1,017,735,624 hazikutangazwa kinyume na kifungu Na. 28 cha Sheria ya Manunuzi ya umma. |
| **3** | **Taasisi ya Utafiti wa Dawa-Afrika (AMREF)-Tanzania – UNDP** |
| | • Taasisi ilijumuisha fedha iliyotengwa kiasi Sh.505,406,450 ambayo haijatumika kwenye matumizi kinyume na matakwa ya taaluma. |

# SURA YA TATU

## UTEKELEZAJI WA MAPENDEKEZO KATIKA RIPOTI ZA KAGUZI ZA MIAKA YA NYUMA

### 3.0 Utangulizi

Sura hii inalenga kutoa taarifa ya utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa katika ripoti za kaguzi za miaka ya nyuma. Hii inaangalia jinsi menejimenti ilivyoyashughulikia masuala yaliyoibuliwa katika ripoti zilizotangulia na masuala yaliyoibuliwa kwa mwaka huu wa fedha na jinsi mapendekezo yaliyotolewa yalivyofanyiwa kazi.

Madhumuni ya mapendekezo ya ukaguzi yanayotolewa ni kumfanya mkaguliwa kufanya maboresho katika usimamizi wa fedha na kudhibiti rasilimali za taasisi. Kutokushughulikiwa kwa wakati mapendekezo ya ukaguzi yaliyotolewa kwenye taarifa kwa upande wa miradi kunaweza kusiwe na maboresho katika mfumo wa usimamizi na matumizi ya rasilimali.

Matatizo ya kutoshughulikia mapungufu yaliyoainishwa na ukaguzi yanapelekea uwezekano wa matatizo hayo kujirudia kwa miaka inayofuata. Hii inaweza kumaanisha kuwa afisa masuuli na uongozi hautoi uzito wa kutosha katika kushughulikia matatizo haya.

Orodha ya mapungufu yaliyotolewa miaka ya nyuma ambayo hayajashughulikiwa na mapungufu yaliyojitokeza kuhusu usimamizi wa fedha za miradi kuanzia mwaka wa fedha 2010/11 hadi 2012/13 yameonyeshwa katika Jedwali Na.27 hapa chini kwa kila mradi:

**Jedwali 27: Mchanganuo wa utekelezaji wa mapendekezo katika ripoti za kaguzi za miaka ya nyuma**

| Mradi | 2010/2011 | 2011/2012 | 2012/2013 |
|---|---|---|---|
| ASDP | 15,157,333,147 | 9,086,703,965.97 | 33,176,375,908 |
| HBF | 5,723,114,166 | 10,982,257,870.41 | 11,707,805,048 |
| TASAF | 971,165,939.57 | 0 | 4,509,012,022 |
| WSDP | 0 | 220,078,175 | 57,904,259,184 |

Mchanganuo katika Jedwali hapo juu unaoonyesha kuwa menejimenti pamoja na uongozi wa miradi hawajachukua hatua madhubuti za kuyashughulikia mapendekezo ya Ukaguzi yaliyotolewa.

Orodha ya miradi ambayo wasimamizi wa miradi hiyo hawajashughulikia mapendekezo yaliyotolewa katika ripoti za kaguzi za miaka ya nyuma ni kama ifuatavyo:

## 3.1 Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo (ASDP)

Halmashauri nyingi hazijafanya vizuri katika kuyashughulikia na kutekeleza mapendekezo yaliyotolewa miaka ya nyuma. Katika ukaguzi wa mwaka huu, Halmashauri 93 zilikuwa na masuala ya miaka ya nyuma ambayo hayajatekelezwa yenye thamani ya Sh.33,176,375,908 kama ilivyoonyeshwa katika **Kiambatisho namba I**.

## 3.2 Mfuko wa Maendeleo ya Afya (HBF)

Mapitio ya utekelezaji wa masuala yaliyoainishwa katika ukaguzi wa miaka iliyopita na hasa mambo yaliyokuwa na kasoro, yalionyesha kuwa masuala yenye thamani ya Sh.11,707,805,048 katika Halmashauri tisini na sita (96) hayakutekelezwa kama ilivyoonyeshwa katika **kiambatisho namba II.**

Hata hivyo kasoro katika mapendekezo ya Ukaguzi imepungua kwa kiasi cha Sh.5,259,143,704 kutoka mwaka 2010/11 hadi 2011/12 na kupungua tena kwa Sh.725,547,178 kutoka mwaka 2011/12 hadi 2012/13.

## 3.3 Mfuko wa Maendeleo ya Jamii Tanzania (TASAF)

Tathmini ya utekelezaji wa mapendekezo katika ripoti za kaguzi za miaka ya nyuma inaonyesha utekelezwaji wa baadhi ya mapendekezo isipokuwa masuala yenye thamani ya Sh.4,509,012,022 kama ilivyoonyeshwa katika **Kiambatisho namba III.**

Mwelekeo unaonyesha kuwa hali ya kutekelezwa kwa mapendekezo yaliyotolewa katika kaguzi za miaka ya nyuma, yalikuwa vizuri kwa mwaka 2011/12; hata hivyo kuna ongezeko ya Sh.4,509,012,022 kwa mwaka 2012/13.

## 3.4 Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji (WSDP)

Mapitio ya utekelezaji wa masuala yaliyoibuliwa katika kaguzi za miaka iliyopita inaonyesha kuwa mambo mengi hayajafanyiwa kazi. Masuala yenye thamani ya Sh.57,904,259,184 na Dola za Marekani 641,318 kama ilivyoonyeshwa katika **kiambatanisho namba IV** bado kutekelezwa.

Hata hivyo, hakuna juhudi za dhati zilizochukuliwa kutekeleza mapendekezo yaliyotolewa katika kaguzi za miaka ya nyuma kwa kuwa kumekuwa na ongezeko la Sh.57,684,181,009 kutoka mwaka 2011/12 hadi 2012/13 sawa na asilimia 99.6.

## 3.5 Miradi Mingine

Mapitio ya utekelezaji wa masuala yaliyoibuliwa katika kaguzi za miaka iliyopita na hasa mambo yaliyoonyesha kasoro, yasiyofanyiwa kazi ni masuala yenye thamani ya Sh.23,855,012,728.12, Yuro 347,572 na Dola za Marekani 668,758,776.04 kama ilivyoonyeshwa katika **Kiambatanishi V.**

# SURA YA NNE

# UTENDAJI WA KIFEDHA

## 4.0 Utangulizi

Sura hii inatoa mchanganuo na mwelekeo wa utendaji wa kifedha katika miradi ya maendeleo ikiwemo sekta ya kilimo, afya, maendeleo ya jamii, maji pamoja na miradi mingine ya maendeleo katika kipindi cha mwaka 2012/13. Miradi hii inafadhiliwa na washirika mbalimbali wa maendeleo pamoja na Serikali ya Tanzania kama inavyoonyeshwa hapo chini:

## 4.1 Programu ya Maendeleo Katika Sekta ya Kilimo

### 4.1.1 Utangulizi

Programu hii inajumuisha mipango ya kuendeleza kilimo kitaifa na kisekta inayofadhiliwa kwa pamoja na Serikali ya Tanzania na Washirika wa Maendeleo kupitia Mfuko wa Maendeleo katika Sekta ya Kilimo.

Mwongozo wa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo (ASDP) ulianzishwa kwa pamoja na wizara tano za kisekta ambazo hutoa mwongozo na mchakato wa kutekeleza mpango mkakati wa kuendeleza sekta ya kilimo (ASDS). Shughuli za maendeleo kitaifa zitazingatia mpango mkakati wa wizara ambapo shughuli za maendeleo katika wilaya zitatekelezwa na mamlaka za Serikali za Mitaa (LGAs).

### 4.1.2 Mfuko wa Kuchangia Sekta ya Maendeleo ya Kilimo - Hazina

Programu ya maendeleo ya sekta ya kilimo inapata fedha kutoka kwa washirika wa maendeleo, mikopo, na michango ya wahisani mbalimbali wakiwemo Ubalozi wa Ireland na Ubalozi wa Japani, Muungano wa Ulaya, Shirika la Kimataifa la Maendeleo na Benki ya Maendeleo ya Afrika.

Katika mwaka wa fedha 2012/13 Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo ilipokea Dola za Marekani 29,995,493 kutoka kwa washirika wa maendeleo  na vilevile kulikuwa

na salio anzia kiasi cha Dola za Marekani 14,803,078 na kufanya fedha zilizokuwepo kuwa Dola za Marekani 44,798,571. Kiasi ambacho kilihamishwa kutoka akaunti ya Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo ni Dola za Marekani 29,281,162 hivyo kiasi cha fedha kilichobaki mwishoni mwa mwaka ambacho hakikupelekwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ni jumla ya Dola za Marekani 15,517,409. Mchanganuo wa michango ya washirika wa maendeleo ni kama ilivyoonyeshwa kwenye Jedwali Na. 28 hapa chini:

Inasikitisha kuona kiasi cha Dola za Marekani 597,599 ambazo hazikutumiwa na watekelezaji wa miradi pamoja na kiasi cha Dola za Marekani 15,517,409 kilichobaki mwishoni mwa mwaka ambacho hakikuhamishwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi hivyo imesababisha kutotekelezwa kwa shughuli za miradi kama ilivyokuwa imepangwa.

**Jedwali 28: Akaunti Kuu ya Mradi**

| **Maelezo** | **2012/13** |
|---|---|
| **Akaunti Na.9931206251** | **USD** |
| Salio anzia 1/7/2011 | 14,803,078 |
| Shirika la Kimataifa la Maendeleo- Benki ya Dunia | 8,000,000 |
| Mkopo kutoka Shirika la Kimataifa la Maendeleo ya Kilimo (IFAD) | 15,545,254 |
| Fedha kutoka Ubalozi wa Ireland | 5,852,640 |
| Kiasi ambacho hakikutumika kwenye miradi | 597,599 |
| **Jumla ya Fedha** | **44,798,571** |
| **Kiasi cha Fedha Kilichohamishwa** | |
| Wizara ya Kilimo | 15,624,571 |
| Halmashauri | 9,839,479 |
| Wizara ya Mifugo na Uvuvi | 2,577,927 |
| Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa | 287,637 |
| Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko | 951,548 |
| **Jumla ya Kiasi cha Fedha Kilichohamishwa** | **29,281,162** |
| **Salio 30/6/2013** | **15,517,409** |

Fedha zilizohamishwa kwenda kwenye Wizara kama ilivyoonyeshwa hapo juu zilijumuishwa kwenye fungu la maendeleo la Wizara husika na kukaguliwa ipasavyo.

### 4.1.3 Fedha zilizotumwa kwenda Halmashauri

Katika mwaka wa fedha 2012/13 halmashauri zilikuwa na jumla ya shilingi 56,057,565,281.66 kiasi hicho kinajumuisha salio anzia la shilingi 33,606,929,980.66 ikiwa ni bakaa ya fedha inayotokana na kipindi cha mwaka wa fedha 2011/12 kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za programu ya maendeleo katika sekta ya kilimo. Maelezo ya kina kwa kila halmashauri yako kwenye **Kiambatisho VI.**

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2013, kulikuwa na bakaa ya shilingi 14,778,757,617.09, hii inaonyesha kuwa halmashauri ziliweza kutumia shilingi 41,278,807,664.57 sawa na asilimia 73.64 ya fedha iliyokuwepo kwa ajili ya kutekeleza shughuli za programu ya maendeleo katika sekta ya kilimo. Mchanganuo ni kama unavyoonekana kwenye Jedwali Na. 29 hapa chini:-

**Jedwali 29: Vyanzo vya fedha Programu ya Kilimo**

| Maelezo | Kiasi (Sh.) |
|---|---:|
| Salio anzia 1/7/2012 | 33,606,929,980.66 |
| Kiasi kilichopokelewa | 22,450,635,301.00 |
| **Jumla ya fedha zilizopo** | **56,057,565,281.66** |
| Kiasi kilichotumika | 41,278,807,664.57 |
| **Bakaa hadi 30 Juni, 2013** | **14,778,757,617.09** |

### 4.1.4 Fedha zilizotumwa Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa

Katika mwaka 2012/13, Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ilikuwa na jumla ya shilingi 454,916,329 kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za programu ya kilimo. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2013 kulikuwa na bakaa ya shilingi 427,706.36, hii inaonyesha kuwa kiasi cha shilingi 454,488,622.64 zilitumika sawa na asilimia 99.9% ya fedha zilizokuwepo. Mchanganuo ni kama unavyoonekana kwenye Jedwali Na.30 hapa chini:

**Jedwali 30: Mchanganuo wa fedha za TAMISEMI**

| Maelezo | Kiasi (Sh.) |
|---|---|
| Salio Anzia 1/7/2012 | 4,329.00 |
| Kiasi Kilichopokelewa | 454,912,000.00 |
| Jumla ya Fedha Zilizopo | **454,916,329.00** |
| Kiasi Kilichotumika | 454,488,622.64 |
| **Bakaa hadi 30 Juni, 2013** | **427,706.36** |

## 4.2 Ufadhili wa Mfuko wa Maendeleo ya Afya

### 4.2.1 Utangulizi

Washirika wa Mfuko wa Maendeleo ya Afya nchini huchangia fedha kupitia akaunti maalumu katika Benki Kuu ya Tanzania na baadaye kuhamisha fedha hizo kwenda Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, TAMISEMI na Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa kutoa fedha kwa mgao wa robo mwaka kupitia Akaunti Kuu ya Hazina. Ufadhili huu hufuata mfumo wa Benki Kuu ya Tanzania ambapo mihadi ya Washirika wa maendeleo hujumuishwa na kuwa sehemu ya bajeti ya mwaka ya taasisi husika.

Mfuko wa Maendeleo ya Afya hauhifadhiwi katika akaunti pekee bali huwekwa pamoja katika akaunti za maendeleo kwa halmashauri zinazotumika pia kwa ajili ya miradi mingine ya maendeleo.

### 4.2.2 Uchambuzi wa Fedha Mfuko wa Maendeleo ya Afya

Mfuko wa Maendeleo ya Afya hupata michango ya fedha kutoka kwa washirika mbalimbali wa maendeleo. Katika mwaka wa fedha 2012/13, Mfuko huu ulipokea kiasi cha Dola za Marekani 103,759,216.76 kutoka kwa Washirika wa Maendeleo na dola za Marekani 205,441.07 zilirejeshwa na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii. Kulikuwa na salio anzia la dola za Marekani 2,161,094.65 na hivyo kufanya kiasi kilichokuwepo kuwa dola za Marekani 106,125,752.48. Fedha za mradi huu huwekwa katika akaunti za kigeni kwa mfumo wa Dola za Marekani katika akaunti iliyopo Benki Kuu ya Tanzania chini ya usimamizi wa Mhasibu Mkuu wa Serikali kama inavyoonyeshwa katika jedwali Na. 31 hapa chini:

**Jedwali 31: Vyanzo vya Fedha vya Mfuko wa Maendeleo ya Afya**

| Washirika wa Maendeleo | Kiasi (Dola za Marekani) |
|---|---|
| Jamhuri ya Ireland | 8,142,750 |
| Uholanzi | 14,066,811.44 |
| CIDA | 28,727,237.32 |
| KFW | 8,986,229 |
| Uswisi | 4,302,925 |
| Mfuko wa Umoja wa Mataifa Maendeleo ya Watoto | 1,000,000 |
| IDA | 25,000,000 |
| UNFPA/UNDP | 600,000 |
| Ubalozi wa Denmark | 12,933,264 |
| **Jumla Ndogo** | **103,759,216.76** |
| Salio la mwaka 2010/2011 | 205,441.07 |
| Salio anzia 01 Julai 2012 | 2,161,094.65 |
| **Jumla Kuu** | **106,125,752.48** |

### 4.2.3 Uhamishaji wa fedha kwenda kwa Wadau wa Maendeleo ya Afya, Dola za Marekani 98,366,677.11

Katika mwaka 2012/13 kiasi cha Dola za Marekani 98,366,677.11 kilihamishwa kwenda kwa wadau wa maendeleo ya afya na kufanya salio la kufungia mwaka kuwa Dola za Marekani 7,759,075.37 hadi kufikia tarehe 30 Juni 2013 kama inavyoonyeshwa katika Jedwali Na.32 hapo chini:

**Jedwali 32: Mapokezi na Uhamishaji wa fedha kwenda kwa Wadau wa afya**

| Mapokezi ya fedha | Kiasi(Dola za Marekani) 2012/2013 | Kiasi(Dola za Marekani) 2011/2012 |
|---|---|---|
| Kiasi Kisichotumika Mwaka 2010/11 | 205,441.07 | 386,033.17 |
| Salio la Kuanzia 01 Julai 2012 | 2,161,094.65 | 3,806,363.71 |
| Umoja wa Mataifa Mipango ya Maendeleo (UNDP) | 600,000 | 600,000 |
| Ubalozi wa Denmark | 12,933,264 | 17,942,000 |

| | | |
|---|---|---|
| Jamhuri ya Watu wa Ireland | 8,142,750 | 8,810,100 |
| Uholanzi | 14,066,811.44 | 23,384,873.63 |
| CIDA | 28,727,237.32 | 24,492,995 |
| KFW | 8,986,229 | 9,430,169 |
| Uswisi | 4,302,925 | 3,244,997.30 |
| UNICEF | 1,000,000 | 1,000,000 |
| Norway | - | 5,216,484.09 |
| IDA- Banki ya Dunia | 25,000,000 | 10,000,000 |
| **Jumla Mapokezi ya Fedha** | **106,125,752.48** | **108,314,016.17** |
| **Uhamishaji** | | |
| Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii | 38,654,507.32 | 52,414,115.83 |
| Serikali za Mitaa | 58,794,483.64 | 53,297,699.56 |
| TAMISEMI | 433,063.17 | 441,105.86 |
| Katibu Tawala Mikoa | 484,622.98 | - |
| **Jumla ya Fedha Zilizohamishwa** | **98,366,677.11** | **106,152,921.27** |
| **Salio Linaloishia 30 Juni 2013** | **7,759,075.37** | **2,610,949.6** |

### 4.2.4 Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii

#### 4.2.4.1 Utendaji wa Kifedha

Wahisani wa maendeleo huchangia fedha zao katika mfuko wa pamoja kwenye Akaunti Kuu iliyopo Benki Kuu ya Tanzania na baadaye fedha hizo hupelekwa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa mfumo wa robo mwaka. Uchangiaji kwenye wizara hupitia mfumo wa kawaida wa usimamizi wa Fedha Benki Kuu ambapo mihadi ya kifedha hujumuishwa katika bajeti ya mwaka ya wizara.

Fedha kutoka katika mfuko wa kuchangia hupelekwa katika Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii na hutolewa katika mfumo wa kawaida wa Serikali wa kugawa fedha. Fedha za mfuko za uchangiaji huwa sehemu ya fedha zinazotunzwa Benki Kuu na kutolewa kwa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa matumizi yake. Sambamba na hilo fedha za mfuko wa maendeleo ya afya hazitunzwi katika akaunti pekee bali

huchanganywa katika akaunti ya maendeleo ambapo fedha za vyanzo vingine vya miradi ya maendeleo huchangiwa katika akaunti hiyo.

Katika mwaka unaoishia tarehe 30 Juni, 2013 Wizara ilipokea Sh.76,753,238,000. Matumizi halisi yalikuwa Sh.69,939,114,029.36 na kufanya salio la fedha zisizotumika kuwa Sh.6,814,123,970.64 hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2013 ambapo Sh.1,843,363,870.64 zilihamishwa kwenda akaunti ya amana na Sh.4,970,760,100 zilihamishiwa akaunti kuu iliyoko Benki Kuu ya Tanzania kama inavyoonyeshwa katika Jedwali Na.33 hapo chini:-

**Jedwali 33: Vyanzo vya Fedha kwa Mfuko wa Maendeleo ya Afya – Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii**

| **Maelezo** | **Kiasi (Shilingi)** |
|---|---:|
| Kiasi kilichopokelewa | 76,753,238,000.00 |
| Kiasi kilichotumika | 69,939,114,029.36 |
| **Kiasi kilichobaki** | **6,814,123,970.64** |
| Uhamisho kwenda Akaunti ya Amana | 1,843,363,870.64 |
| **Kiasi kilichorejeshwa kwenda Akaunti Kuu** | **4,970,760,100.00** |

### 4.2.5 TAMISEMI

Programu ya Sekta ya Afya huchangiwa na Ireland, Uholanzi, Norway, Ujerumani, Benki ya Dunia na Shirika la Maendeleo na Ushirikiano la Uswisi. Katika mwaka 2012/13 programu ilipokea kiasi cha Sh.687,000,000.

Kwa mujibu wa taarifa ya mapato na matumizi TAMISEMI ilikuwa na kiasi cha fedha kwa ajili ya program hii cha Sh.1,199,637,403.42 kuhusisha salio la kuanzia la Sh.512,637,403.42. Hata hivyo hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2013 kulikuwa na kiasi kisichotumika cha Sh.518,995,683 sawa na asilimia 43 kuashiria kwamba mradi ulitumia Sh.680,641,720.42 sawa na asilimia 57 kama inavyoonyeshwa katika Jedwali Na.34 hapa chini:-

**Jedwali 34: Vyanzo vya fedha kwa mfuko wa Maendeleo ya Afya TAMISEMI**

| **Maelezo** | **Kiasi (Sh.)** |
|---|---|
| Salio anzia 1/7/2012 | 512,637,403.42 |
| **Ongeza:** Mapokezi ya Fedha | 687,000,000 |
| Kiasi kilichopatikana | 1,199,637,403.42 |
| **Toa:** Matumizi | 680,641,720.42 |
| **Kiasi kilichosalia mpaka tarehe 30/06/2013** | **518,995,683** |

### 4.2.6 Serikali za Mitaa

Katika mwaka wa fedha Serikali za Mitaa zilipokea fedha kama inavyoonyeshwa katika Jedwali Na.35 na kwa undani katika kiambatisho namba VII.

**Jedwali 35: Vyanzo vya Fedha Mfuko wa Maendeleo**

| **Maelezo** | **Kiasi (Shilingi)** |
|---|---|
| Salio la Kuanzia tarehe 1/7/2012 | 12,290,342,621 |
| Ongeza: Fedha zilizopokelewa | 89,632,095,709 |
| Kiasi Kilichopatikana | 101,922,438,330 |
| Toa: Matumizi | 75,340,283,154 |
| Kiasi kilichobakia tarehe 30/6/2013 | 26,582,155,175 |

## 4.3 Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF)

### 4.3.1 Mapato ya Mfuko

Mfuko wa Maendeleo ya Jamii unafadhiliwa na Benki ya Dunia kupitia Shirika la Maendeleo ya Kimataifa (IDA). Mkataba kati ya Tanzania na Benki ya Dunia ulisainiwa tarehe 19 Januari; 2005 kwa kiasi cha jumla ya Dola za Marekani milioni 150. Kiasi cha Shilingi milioni 129 zilitokana na mkopo toka Benki ya Dunia na Dola za Marekani milioni 21 zilitokana na ruzuku.

Jumla ya Sh. 27,239,913,495 zilikuwepo kwa ajili ya kutekeleza shughuli za mradi kwa mwaka 2012/13 na kiasi hiki kilijumuisha bakaa ya mwanzo ya Sh. 12,815,934,118.93 ya miaka iliyopita. Hadi kufikia tarehe 30/06/2013 kulikuwa na salio hasi la Shilingi 1,344,592,676.53 hii inamaanisha

Sh.28,584,506,161.62 zilitumika katika utekelezaji wa miradi kama ilivyoonyeshwa katika Jedwali Na. 36 hapa chini:

**Jedwali 36: Vyanzo vya Fedha na Matumizi**

| Maelezo | Kiasi (Sh.) 2012/2013 | Kiasi (USD) 2012/2013 |
|---|---:|---:|
| Salio 1/7/2012 | 12,815,934,118.93 | 7,911,070.44 |
| Benki ya Dunia | 11,267,671,899.15 | 6,767,370.51 |
| Mchango wa Serikali | 584,000,000.00 | 300,300.30 |
| Wengine | 3,459,266,021.25 | 2,077,637.25 |
| Upungufu wa ubadilishaji wa fedha | (886,958,554.24) | (482,257.39) |
| **Mapato kwa mwaka** | **14,423,979,366.16** | **8,663,050.67** |
| **Jumla ya fedha zilizokuwepo kwa mwaka** | **27,239,913,495.08** | **16,574,121.11** |
| Matumizi kwa mwaka | 28,584,506,161.62 | 17,167,871.57 |
| **Salio 30/6/2013** | **(1,344,592,676.53)** | **(593,750.45)** |

### 4.3.2 Fedha iliyopelekwa Halmashauri

Katika mwaka wa fedha 2012/13, jumla ya Sh.29,165,256,151 zilikuwepo kwenye halmashauri, kiasi hiki kilijumuisha bakaa ya Sh.6,121,150,154 ya mwaka uliopita. Hadi kufikia tarehe 30/06/2013 kulikuwa na salio la kiasi cha Sh.2,931,725,987 sawa na asilimia 10 ya fedha iliyopelekwa halmashauri, hii inamaanisha kuwa matumizi yalikuwa jumla ya Sh. 26,233,530,165 kama ilivyoonyeshwa kwenye Jedwali Na. 37 hapa chini. Bakaa hii ilitokana na kutokutekelezwa kwa miradi kama ilivyokuwa imepangwa. **(Rejea kiambatanisho Na.VIII)**

**Jedwali 37: Fedha zilizopelekwa Mamlaka za Serikali za Mitaa**

| Maelezo | Kiasi (Sh.) |
|---|---|
| Salio 1/7/2012 | 6,121,150,154 |
| Fedha iliyopokelewa | 23,044,105,997 |
| **Jumla** | **29,165,256,151** |
| Matumizi | 26,233,530,165 |
| **Salio 30/6/2013** | **2,931,725,987** |

### 4.3.3 Mpango wa Uhawilishaji Fedha kwa Kaya Masikini (TASAF III Productive Social Safety Net)

Hii ni programu mpya ya TASAF ambayo inatarajiwa kutekelezwa kwa kipindi cha miaka kumi kuanzia mwaka 2012 na kuimarisha mafanikio yaliyopatikana kwenye TASAF II kwa kutumia njia ya jamii kujiletea maendeleo yake, kusaidia utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya jamii, shughuli za kuimarisha maisha, kuongeza upelekaji wa fedha katika programu, kusaidia utekelezaji wa miundo mbinu, pamoja na kujenga uwezo katika utekelezaji bora wa programu za maendeleo.

TASAF III ilipokea jumla ya kiasi cha Shs 20,120,091,504 kwa mwaka wa fedha 2012/13 sawa na Dola za Marekani 12,268,348.48. Kwa mwaka huu wa kwanza wa utekelezaji TASAF III imetumia kiasi cha Sh. 15,706,772,694.86 sawa na Dola za Marekani 9,577,300.43 hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2013 na kubakiwa na bakaa ya kiasi cha Sh. 4,413,318,809.14 (sawa na Dola za Marekani 2,691,048.05). Mchanganuo umeonyeshwa katika Jedwali Na. 38 hapo chini:

**Jedwali 38**: **Mpango wa Uhawilishaji Fedha kwa Kaya Masikini**

| Maelezo | Kiasi( Sh) | Kiasi(Dola za Marekani) |
|---|---|---|
| Bakaa 1/07/2012 | - | - |
| Fedha Zilizopokelewa | | |
| IDA | 21,786,814,520.00 | 13,284,643.00 |
| Hasara katika | (1,666,723,016.00) | (1,016,294.52) |

| | | |
|---|---|---|
| ubadilishaji wa fedha | | |
| **Jumla ya Fedha** | **20,120,091,504.00** | **12,268,348.48** |
| Matumizi | 15,706,772,694.86 | 9,577,300.43 |
| **Bakaa 30/06/2013** | **4,413,318,809.14** | **2,691,048.05** |

## 4.4 Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji

### 4.4.1 Utendaji wa Kifedha wa Mfuko wa Sekta ya Maji

**(a) Akaunti Kuu ya Mradi Hazina**

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2012/13 Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ikishirikiana na washirika wa maendeleo iliwezesha kupatikana kwa kiasi cha Dola za Marekani 89,765,293. Hata hivyo kulikuwa na bakaa ya kiasi cha Dola za Marekani 29,734,919 katika akaunti kuu hivyo kufanya jumla ya Dola za Marekani 119,506,424 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika sekta hii. Kati ya fedha hizo kiasi cha Dola za Marekani 102,848,573 kilihamishwa kwenda sehemu mbalimbali ikiwemo kiasi cha Dola za Marekani 15,882,015 kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa, Dola za Marekani 150,352 kwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Dola za Marekani 56,568,687 kwa Wizara ya Maji, Dola za Marekani 4,292,554 kwa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, Dola za Marekani 94,388 kwa Ofisi ya Waziri Mkuu – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Dola za Marekani 25,860,578 kwa miradi mbalimbali hivyo kubaki na bakaa ya Dola za Marekani 16,657,851 ilipofikia tarehe 30 Juni, 2013 kama ilivyoanishwa katika Jedwali Na.39 hapo chini:

**Jedwali 39: Utendaji Kifedha katika Akaunti Kuu ya Mradi Hazina**

| **Maelezo** | **Kiasi - USD** |
|---|---|
| Salio 1/7/2012 | 29,734,919 |
| Benki ya Maendeleo ya Afrika | 12,638,254 |
| Shirika la Maendeleo la Uingereza (DFID) | 26,882,350 |
| Shirika la Maendeleo la Kimataifa(IDA) | 32,670,000 |
| Benki ya Maendeleo ya Ujerumani (KFW) | 17,574,688 |
| Fedha zilizorejeshwa | 6,213 |

| | |
|---|---:|
| **Jumla ya Fedha** | **119,506,424** |
| **Uhamishaji wa Fedha** | |
| Mamlaka za Serikali za Mitaa | 15,882,015 |
| Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi | 150,352 |
| Wizara ya Maji | 56,568,687 |
| Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii | 4,292,554 |
| Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI | 94,388 |
| WSDP (Forex) | 25,860,578 |
| **Jumla ya fedha zilizohamishwa** | **102,848,573** |
| **Bakaa 30/06/2013** | **16,657,851** |

**(b) Chanzo cha Fedha za Mradi wa Maji**

Katika kipindi cha mwaka 2012/13 kulikuwa na kiasi cha Sh.474,069,998,451 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika sekta ya maji. Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ikishirikiana na washirika wa maendeleo ilitoa kiasi cha Sh. 315,432,908,022 na kulikuwa na kiasi cha Sh.80,215,610,874 ikiwa bakaa katika kipindi cha mwaka wa fedha 2011/12 pamoja na kiasi cha Sh. 78,421,479,555 ikiwa ni salio la fedha zilizopelekwa kwa watekelezaji wa miradi kama ilivyoanishwa katika Jedwali Na.40 na 41 hapo chini:

**Jedwali 40: Chanzo cha Fedha za Mradi wa Maji 2012/13**

| **Serikali ya Tanzania/Wadau wa Maendeleo** | **Kiasi (Sh)** |
|---|---:|
| Mchango wa Serikali Tanzania | 104,000,000,000 |
| Wadau wa Mfuko wa Pamoja | 140,600,387,785 |
| Wadau wa mifuko mbalimbali | 66,208,015,031 |
| Mchango kutoka kwa Jamii | 3,644,457,889 |
| Rekebisho: kutokana na kubadilika kwa thamani ya kubadilisha fedha za kigeni | 980,047,317 |
| **Jumla ya Michango** | **315,432,908,022** |
| **Ongeza:** Salio anzia 1/7/2012 | 80,215,610,874 |
| Salio la fedha zilizopelekwa kwa watekelezaji wa Miradi | 78,421,479,555 |
| **Jumla ya kiasi kilichokuwepo kwa mwaka** | **474,069,998,451** |
| **Toa:** Matumizi kwa mwaka | 275,858,611,472 |

| | |
|---|---|
| **Bakaa 30 Juni, 2013** | **198,211,386,979** |

**Jedwali 41: Mchango Kutoka kwa Washirika wa Maendeleo**

| **Wahisani** | **Kiasi (Sh.)** |
|---|---|
| Shirika la Maendeleo la Kimataifa (IDA) | 51,072,912,990 |
| Benki ya Maendeleo ya Ujerumani (KFW) | 27,446,096,400 |
| Banki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) | 19,748,781,686 |
| Shirika la Maendeleo la Uingereza (DFID) | 42,332,596,707 |
| **JUMLA** | **140,600,387,783** |

**Mchoro 1**: Mchango Kutoka kwa Washirika wa Maendeleo




### (c) Mamlaka za Serikali za Mitaa

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2012/13, halmashauri 131 zilipewa jumla ya kiasi cha Sh. 144,932,139,042 zilizojumuisha salio anzia la Sh. 63,900,019,304 kutekeleza Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji kwenye halmashauri. Hata hivyo, mpaka kufikia 30/06/2013 halmashauri zilibakiwa na kiasi cha Sh. 79,387,536,594 sawa na asilimia 54.8 ya kiasi kilichokuwepo kwa mwaka. Hii inamaanisha halmashauri zilitumia kiasi cha Sh.65,544,602,448 sawa na asilimia 45.2 ya fedha zote zilizokuwepo. Taarifa zaidi zimeonyeshwa kwenye Jedwali Na.42 hapo chini na kiambatanisho Na.IX cha ripoti hii.

**Jedwali 42: Utendaji wa Kifedha – Mamlaka za Serikali za Mitaa**

| **Maelezo** | **Kiasi (Sh.)** |
|---|---:|
| Salio 1/7/2012 | 63,900,019,304 |
| Fedha iliyopokelewa | 81,032,119,738 |
| **Jumla ya fedha** | **144,932,139,042** |
| Matumizi | 65,544,602,448 |
| **Salio 30/6/2013** | **79,387,536,594** |

**(d) Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii**

Katika mwaka 2012/13, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii ilipata jumla ya Sh. 8,208,560,000 kutekeleza shughuli mbalimbali za mradi wa maji. Fedha hizo zilijumuisha salio anzia Sh. 531,060,000 na Sh. 7,677,500,000 kutoka kwenye Mfuko wa Maendeleo ya Afrika (ADF).

Hata hivyo, mpaka kufikia 30/06/2013 wizara ilishatumia kiasi cha Sh.7,484,099,190 sawa na asilimia 91 ya fedha zote zilizokuwepo. Hivyo wizara ilibakisha kiasi cha Sh.724,460,810 kama salio kwa mwaka husika kama inavyoonekana kwenye jedwali Na.43 hapo chini:

**Jedwali 43: Utendaji wa Kifedha - Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii**

| **Maelezo** | **Kiasi (Sh.)** |
|---|---:|
| Salio 1/7/2012 | 531,060,000 |
| Fedha zilizopokelewa | 7,677,500,000 |
| **Jumla ya fedha** | **8,208,560,000** |
| Matumizi | 7,484,099,190 |
| **Salio 30/06/2013** | **724,460,810** |

## 4.5 Miradi Mingine

### 4.5.1 Mfuko wa Kimataifa wa Kupambana na Ukimwi, Kifua Kikuu na Malaria

#### 4.5.1.1 Akaunti Kuu - Hazina

Katika mwaka wa fedha 2012/13 Wizara ya Fedha ilipokea kiasi cha Dola za Marekani 53,409,012 kutoka Mfuko wa Kimataifa wa Kupambana na Kifua Kikuu, Ukimwi na Malaria. Kati ya fedha hizo kiasi cha Dola za Marekani 12,961,164

kilikwenda Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii na kiasi cha Dola za Marekani 36,528,885 kilihamishiwa kwenye akaunti ya Maendeleo na kubaki na salio Dola za Marekani 3,918,962 kama inavyoonekana kwenye Jedwali Na. 44 hapa chini:

**Jedwali 44: Mapato na Matumizi - Hazina**

| **Maelezo** | **Kiasi (Dola za Marekani)** |
|---|---|
| **Fedha zilizokuwepo 2012/13** | **53,409,011** |
| **Uhamisho wa fedha kwenda:** | |
| Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii | 12,961,164 |
| Akaunti ya Maendeleo | 36,528,885 |
| **Jumla ya fedha iliyohamishwa** | **49,490,049** |
| **Salio 30/06/2013** | **3,918,962** |

### 4.5.1.2 Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii

Katika kipindi cha mwaka 2012/13, wizara ilikuwa na kiasi cha Sh.171,071,916,834.83 kwa ajili ya Mfuko wa Kimataifa wa Kupambana na Malaria, Kifua Kikuu na Ukimwi, kiasi chote kilipelekwa katika shughuli husika kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 45 hapa chini:

**Jedwali 45: Mapato na Matumizi - Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii**

| **Maelezo** | **Kiasi (Sh.)** |
|---|---|
| Salio 1.7.2012 | 0 |
| Kiasi kilichopokelewa | 171,071,916,834.83 |
| Kiasi cha fedha iliyopo | 171,071,916,834.83 |
| Matumizi | 171,071,916,834.83 |
| **Salio 30/06/2013** | **0** |

### 4.5.1.3 Mzunguko wa Nane Akaunti Fedha za Kigeni Benki Kuu

Katika kipindi cha mwaka 2012/13 Benki Kuu ya Tanzania ilikuwa na kiasi cha Dola za Marekani 82,118,029.68 kwa ajili ya Mfuko wa Kimataifa wa Kupambana na Malaria, Kifua Kikuu na Ukimwi, kiasi kilichotumika ni Dola za Marekani 75,190,264.39 sawa na asilimia 91.56 ya kiasi kilichotolewa hivyo kubaki na salio la Dola za Marekani 6,927,765.29 kama inavyoonekana kwenye jedwali Na. 46 hapa chini:

**Jedwali 46: Mapato na Matumizi - Akaunti ya Fedha za Kigeni Benki Kuu**

| Maelezo | Kiasi (Dola za Marekani) |
|---|---|
| Salio 1/7/2012 | 12,764,286.92 |
| Kiasi kilichopokelewa | 69,353,742.76 |
| **Jumla ya fedha** | **82,118,029.68** |
| Matumizi | 75,190,264.39 |
| **Salio 30/6/2013** | **6,927,765.29** |

### 4.5.1.4 Programu ya Kitaifa ya Kudhibiti Ukimwi

Katika kipindi cha mwaka 2012/13, Programu ya Kitaifa ya Kudhibiti Ukimwi ilikuwa na kiasi cha Sh.2,563,924,218.58 ikijumuisha Sh.1,932,197,775.81 salio la mwaka 2011/12. Matumizi halisi yalikuwa Sh.1,939,429,375.19 ikiwa ni asilimia 76 ya fedha yote na kuwa na bakaa ya mwaka ya kiasi cha Sh.624,494,843.39 kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 47 hapo chini:

**Jedwali 47: Mapato na Matumizi Programu ya Kitaifa ya Kudhibiti Ukimwi**

| Maelezo | Kiasi (Sh.) |
|---|---|
| Salio 1/7/2012 | 1,932,197,775.81 |
| Fedha iliyopokelewa | 631,726,442.77 |
| **Jumla ya Fedha** | **2,563,924,218.58** |
| Matumizi | 1,939,429,375.19 |
| **Salio 30/06/2013** | **624,494,843.39** |

### 4.5.1.5 Ufuatiliaji na Tathmini Mzunguko wa Nane-Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii

Katika mwaka 2012/13, Ufuatiliaji na Tathmini Mzunguko wa Nane-Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii ulikuwa na kiasi cha Sh.213,608,578.88 na matumizi halisi yalikuwa ni Sh.65,629,252.45 ikiwa ni asilimia 31 ya fedha zote na kuwa na bakaa ya kiasi cha Sh.147,979,326.43 mwisho wa mwaka kama inavyoonyeshwa katika Jedwali Na. 48 hapo chini:

**Jedwali 48: Mapato na Matumizi - Ufuatiliaji na Tathmini**

| Maelezo | Kiasi (Sh.) |
|---|---:|
| Salio 1/7/2013 | 58,774,401.14 |
| Fedha iliyopokelewa | 154,834,177.74 |
| **Jumla ya fedha** | **213,608,578.88** |
| Matumizi | 65,629,252.45 |
| **Salio 30/06/2013** | **147,979,326.43** |

### 4.5.1.6 Uimarishaji Mfumo wa Afya - Mzunguko wa Tisa (9)

Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii ilikuwa na kiasi cha Sh.29,332,429,025.86 kwa ajili ya uimarishaji wa Mfumo wa Afya Mzunguko wa Tisa. Kiasi kilichotumika ni Sh.17,153,672,079.68 sawa na asilimia 58 ya kiasi kilichotolewa hivyo kubaki na salio la Sh. 12,178,756,946.18 mwisho wa mwaka kama inavyoonekana kwenye Jedwali Na. 49 hapa chini:

**Jedwali 49: Mapato na Matumizi - Uimarishaji Mfumo wa Afya**

| Maelezo | Kiasi (Sh.) |
|---|---:|
| Salio 1/7/2012 | 4,435,551,638.86 |
| Fedha iliyopokelewa | 24,896,877,387.00 |
| **Jumla ya fedha** | **29,332,429,025.86** |
| Matumizi | 17,153,672,079.68 |
| **Salio 30/06/2013** | **12,178,756,946.18** |

### 4.5.1.7 Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa

Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ilikuwa na kiasi cha Sh.397,404,533.84 kutoka katika Mfuko wa Kimataifa wa Kupambana na Malaria, Kifua Kikuu na Ukimwi. Kiasi kilichotumika ni Sh.393,485,774.20 sawa na asilimia 99 ya kiasi kilichotolewa hivyo kubaki na salio la Sh.3,918,759.64 mwisho wa mwaka kama inavyoonekana kwenye Jedwali Na. 50 hapa chini:

**Jedwali 50: Mapato na Matumizi Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa**

| Maelezo | Kiasi (Sh.) |
|---|---:|
| Salio 1/7/2012 | 75,795,339.37 |
| Fedha iliyopokelewa toka GF | 193,721,483.88 |
| Fedha iliyorejeshwa ambayo haikutumika | 127,887,710.59 |
| **Jumla ya fedha** | **397,404,533.84** |
| Matumizi | 393,485,774.20 |
| **Salio 30/06/2013** | **3,918,759.64** |

### 4.5.1.8 Tume ya Kudhiditi Ukimwi Tanzania

Tume ya Kudhibiti Ukimwi Tanzania ilikuwa na kiasi cha Sh.1,738,553,509 kutoka kwenye Mfuko wa Kimataifa wa Kupambana na Malaria, Kifua Kikuu na Ukimwi. Kiasi kilichotumika ni Sh.1,431,317,491.05 sawa na asilimia 82 ya kiasi kilichotolewa hivyo kubaki na salio la Sh.307,236,017.69 mwisho wa mwaka kama inavyoonekana kwenye Jedwali Na. 51 hapa chini:

**Jedwali 51: Mapato na Matumizi Tume ya Kudhiditi Ukimwi**

| Maelezo | Kiasi (Sh.) |
|---|---:|
| Salio 1/7/2012 | 1,419,815,924.04 |
| Fedha iliyopokelewa | 318,737,584.70 |
| **Jumla ya fedha** | **1,738,553,508.74** |
| Matumizi | 1,431,317,491.05 |
| **Salio 30/06/2013** | **307,236,017.69** |

### 4.5.1.9 Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Afya Mwanza - Mzunguko wa Tisa (9)

Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Afya Mwanza – Mfuko wa Kimataifa wa Kupambana na Ukimwi, Kifua Kikuu na Malaria Mzunguko wa Tisa (9) ulikuwa na kiasi cha Sh.2,415,941,804.97. Matumizi halisi yalikuwa ni Sh.2,412,364,742.92 sawa na asilimia 99 ya fedha yote na kuwa na bakaa mwisho wa mwaka ya kiasi cha Sh.3,577,062.05 kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 52 hapo chini:

**Jedwali 52: Mapato na Matumizi Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Afya - Mwanza**

| **Maelezo** | **Kiasi (Sh.)** |
|---|---:|
| Salio 1/7/2012 | 12,634,047.84 |
| Fedha kutoka GF | 1,558,358,875.00 |
| Fedha za ndani zilizohamishwa | 344,948,882.13 |
| Kiasi kilichotoka akaunti ya amana | 500,000,000.00 |
| **Jumla ya Fedha** | **2,415,941,804.97** |
| Matumizi | 2,412,364,742.92 |
| **Salio 30/6/2013** | **3,577,062.05** |

### 4.5.1.10 Kitengo cha Uchunguzi wa Magonjwa

Katika kipindi cha mwaka 2012/13, Kitengo cha Uchunguzi wa Magonjwa kilikuwa na kiasi cha Sh.1,596,406,020 ikiwa ni salio la fedha la mwaka 2011/12. Hadi kufikia tarehe 30/06/2013 matumizi yalikuwa Sh. 1,530,408,214 ikiwa ni sawa na asilimia 96 ya fedha yote iliyokuwepo; hivyo kufanya salio ishia kuwa Sh.42,012,316 kama inayoonekana kwenye Jedwali Na. 53 hapa chini:

**Jedwali 53: Mapato na matumizi - Kitengo cha Uchunguzi wa Magonjwa**

| **Maelezo** | **Kiasi (Sh.)** |
|---|---:|
| Salio 1/7/2012 | 1,596,406,020 |
| Matumizi | 1,530,408,214 |
| **Salio 30/6/2013** | **42,012,316** |

### 4.5.2 Miradi Mingine

Taarifa ya utendaji wa fedha kwa miradi mingine 102 ambayo ilikaguliwa ilikuwa na jumla ya Sh.513,682,759,109.18 na Dola za Marekani 1,827,473,581.84 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi hiyo. Matumizi halisi yalikuwa ni Sh.332,082,129,223.27 na Dola za Marekani 1,675,991,257.08, hivyo salio ishia mwishoni mwa mwaka lilikuwa Sh.181,600,629,885.80 na Dola za Marekani 151,482,324.76 kama ilivyo kwenye mchanganuo katika **Kiambatisho X.**

# SURA YA TANO

## UDHAIFU KATIKA USIMAMIZI WA FEDHA

### 5.0 Utangulizi

Sura hii inalenga kutoa upungufu uliobainika katika kusimamia fedha za miradi ya maendeleo uliotokana na ukaguzi. Sehemu hii inahusu utekelezaji wa miradi ya maendeleo na masuala muhimu yaliyoibuliwa kwa mwaka huu wa fedha.

Madhumuni ya matokeo na mapendekezo ya ukaguzi ni kumsaidia mkaguliwa kufanya maboresho katika usimamizi wa fedha na kudhibiti rasilimali za taasisi.

Orodha ya mapungufu yaliyojitokeza kuhusu usimamizi wa fedha za miradi yameonyeshwa hapa chini kwa kila mradi:

### 5.1 Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo (ASDP)

#### 5.1.1 Malipo Yenye Nyaraka Pungufu, Sh. 470,661,014

Kulikuwa na malipo ya Sh. 470,661,014 yenye nyaraka pungufu. Kati ya kiasi hiki, Halmashauri ya Wilaya ya Tarime ilikuwa na sehemu kubwa ya asilimia 21, ikifuatiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Nanyumbu yenye asilimia 16 na Halmashauri ya Wilaya ya Rorya ni ya tatu kwa kuwa na asilimia 9.9. Mchanganuo wa Halmashauri umeonyeshwa katika jedwali Na.54 hapa chini:

**Jedwali 54: Malipo yenye Nyaraka Pungufu**

| Na | Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---:|
| 1 | Wilaya ya Tarime | 96,513,700 |
| 2 | Wilaya ya Nanyumbu | 74,857,020 |
| 3 | Wilaya ya Rorya | 46,606,158 |
| 4 | Wilaya ya Kondoa | 32,360,401 |
| 5 | Wilaya ya Mbozi | 28,504,857 |
| 6 | Manispaa ya Sumbawanga | 25,925,798 |
| 7 | Wilaya ya Kilwa | 18,672,580 |
| 8 | Wilaya ya Kasulu | 17,579,000 |
| 9 | Wilaya ya Ukerewe | 16,028,000 |
| 10 | Wilaya ya Kwimba | 15,990,000 |

| | | |
|---|---|---|
| 11 | Wilaya ya Kiteto | 13,958,000 |
| 12 | Wilaya ya Bunda | 13,165,000 |
| 13 | Wilaya ya Nachingwea | 10,733,500 |
| 14 | Wilaya ya Kilosa | 9,815,000 |
| 15 | Wilaya ya Mtwara | 8,524,400 |
| 16 | Wilaya ya Ruangwa | 6,918,000 |
| 17 | Wilaya ya Bukombe | 6,800,000 |
| 18 | Wilaya ya Rungwe | 5,759,500 |
| 19 | Wilaya ya Songea | 5,449,600 |
| 20 | Wilaya ya Mbinga | 5,124,000 |
| 21 | Wilaya ya Sumbawanga | 3,747,500 |
| 22 | Wilaya ya Nkasi | 2,805,000 |
| 23 | Wilaya ya Mbulu | 2,769,000 |
| 24 | Wilaya ya Mafia | 1,040,000 |
| 25 | Wilaya ya Longido | 1,015,000 |
| | **Jumla** | **470,661,014** |

Hata hivyo, kiasi cha malipo yenye nyaraka pungufu kimeongezeka kwa Sh.76,605,318.50 ukilinganisha na mwaka 2011/12 ambao ulionyesha Sh. 394,055,695.50 kama malipo yenye nyaraka pungufu.

### 5.1.2 Hati za Malipo zisizokaguliwa,Sh.703,778,713

Hati za malipo za thamani ya Sh. 703,778,713 zilizoandikwa kwenye daftari la fedha hazikuweza kupatikana wakati wa ukaguzi. Hii ni kinyume na Agizo Na.34 (1) la LAFM, 2009 na Kifungu Na.45 (5) cha Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa ya mwaka 1982. Halmashauri kumi na moja (11) zilionekana kuwa na matumizi yasiyokuwa na hati za malipo, ikiongozwa na Bariadi iliyokuwa na asilimia 69, ikifuatiwa na Nachingwea yenye asilimia 11.54 na ya tatu ni Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino yenye asilimia 7.5. Usahihi na uhalali wa malipo yaliyofanyika haukuweza kuthibitishwa kwa kukosekana kwa nyaraka na imepunguza mawanda ya ukaguzi.

Mchanganuo wa halmashauri zinazohusika umeonyeshwa kwenye Jedwali Na.55 hapa chini:

**Jedwali 55: Hati za malipo zisizokaguliwa**

| Na | Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|
| 1 | Wilaya ya Bariadi | 485,803,736 |
| 2 | Wilaya ya Nachingwea | 81,236,566 |
| 3 | Wilaya ya Chamwino | 52,541,489 |
| 4 | Wilaya ya Lindi | 34,708,200 |
| 5 | Wilaya ya Liwale | 16,070,000 |
| 6 | Wilaya ya Kisarawe | 14,672,500 |
| 7 | Wilaya ya Mbozi | 7,221,222 |
| 8 | Wilaya ya Kilwa | 6,000,000 |
| 9 | Wilaya ya Morogoro | 2,200,000 |
| 10 | Wilaya ya Mafia | 1,845,000 |
| 11 | Wilaya ya Sumbawanga | 1,480,000 |
| | **Jumla** | **703,778,713** |

Hata hivyo, kiasi cha hati za malipo zisizokaguliwa kimeongezeka kwa Sh.383,716,498 ukilinganisha na mwaka 2011/12 ambao ulionyesha Sh.320,062,215 kama hati za malipo zisizokaguliwa.

### 5.1.3 Matumizi yaliyofanywa kwa kutumia vifungu Visivyohusika Sh.632,382,256

Matumizi ya jumla ya Sh.632,382,256 yalilipwa kwa kutumia vifungu visivyohusika kinyume na Agizo Na. 23(1) la LAFM, 2009. Matumizi yaliyofanywa nje ya vifungu vilivyoidhinishwa yanadhihirisha kwamba kazi ambazo zingegharimu shilingi 632,382,256 na ambazo ziliidhinishwa hazikufanyika na hivyo kusababisha uwezekano mkubwa wa kuzidisha au kupunguza gharama halisi za matumizi yaliyofanyika katika kila kifungu.
Mchanganuo wa halmashauri 19 zilizohusika umeonyeshwa katika Jedwali Na. 56 hapa chini:

**Jedwali 56: Matumizi yaliyofanywa kwa kutumia vifungu visivyohusika**

| Na | Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|
| 1 | Wilaya ya Nachingwea | 196,800,655 |
| 2 | Wilaya ya Sikonge | 150,260,651 |
| 3 | Wilaya ya Lindi | 92,991,000 |
| 4 | Wilaya ya Bagamoyo | 47,439,218 |

| | | |
|---|---|---|
| 5 | Wilaya ya Tabora | 33,121,000 |
| 6 | Wilaya ya Kisarawe | 16,796,068 |
| 7 | Wilaya ya Rorya | 16,701,200 |
| 8 | Wilaya ya Songea | 13,865,000 |
| 9 | Wilaya ya Arusha | 9,334,805 |
| 10 | Wilaya ya Kahama | 8,320,000 |
| 11 | Wilaya ya Liwale | 7,215,000 |
| 12 | Wilaya ya Pangani | 6,878,584 |
| 13 | Wilaya ya Siha | 6,195,400 |
| 14 | Wilaya ya Lindi | 6,109,000 |
| 15 | Wilaya ya Ileje | 5,000,000 |
| 16 | Wilaya ya Mafia | 4,716,175 |
| 17 | Wilaya ya Nkasi | 3,900,000 |
| 18 | Wilaya ya Rombo | 3,550,000 |
| 19 | Manispaa ya Kigoma | 3,188,500 |
| | **Jumla** | **632,382,256** |

Kutokana na jedwali hapo juu, Halmashauri ya Wilaya ya Nachingwea iliongoza kwa kuwa na asilimia 31, ikifuatiwa na Sikonge yenye asilimia 24 na Lindi yenye asilimia 15.

Hata hivyo, kiasi cha matumizi yaliyofanywa kwa kutumia vifungu visivyohusika kimeongezeka kwa Sh.460,693,507.79 ukilinganisha na mwaka 2010/11 ambao ulikuwa na kiasi cha Sh.171,688,748.21

### 5.1.4 Matumizi yaliyofanywa nje ya Bajeti iliyodhinishwa Sh.328,423,420

Halmashauri 11 zilifanya matumizi yenye thamani ya jumla ya Sh.328,423,420 nje ya bajeti iliyoidhinishwa kinyume na Agizo Na.17(2)&(3) na 18(1) la Memoranda ya Fedha za Serikali za Mitaa ya mwaka 2009. Hii ina maana kuwa kuna baadhi ya kazi zilizokuwa kwenye bajeti iliyoidhinishwa ambazo hazikutekelezwa kutokana na kutozingatia sheria ya matumizi. Mchanganuo wa halmashauri zilizohusika umeonyeshwa katika Jedwali Na.57 hapa chini:

**Jedwali 57: Matumizi yaliyofanywa nje ya Bajeti iliyodhinishwa**

| Na | Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|
| 1 | Wilaya ya Lindi | 96,620,000 |
| 2 | Wilaya ya Urambo | 95,256,827 |
| 3 | Wilaya ya Liwale | 39,605,000 |
| 4 | Wilaya ya Nachingwea | 27,850,300 |
| 5 | Wilaya ya Chamwino | 22,805,000 |
| 6 | Wilaya ya Bahi | 16,780,000 |
| 7 | Wilaya ya Kilwa | 10,997,580 |
| 8 | Wilaya ya Songea | 8,542,000 |
| 9 | Wilaya ya Sumbawanga | 6,647,713 |
| 10 | Manispaa ya Lindi | 2,139,000 |
| 11 | Wilaya ya Mpwapwa | 1,180,000 |
| | **Jumla** | **328,423,420** |

### 5.1.5 Malipo yasiyokubalika Sh. 4,111,033

Kifungu Na.13.2.2 katika Mwongozo wa makubaliano ya shughuli za Mfuko wa Maendeleo ya Kilimo mwaka 2006 kinaelezea kuwa, manunuzi yote ya pembejeo za kilimo na kazi zinazohusiana na kilimo hazitakiwi kulipiwa kodi ya ongezeko la thamani (VAT). Halmashauri mbili (2) zilitumia kiasi cha Sh. 4,111,033 ambacho ni kodi ya ongezeko la thamani katika manunuzi waliyoyafanya.

Mchanganuo wa malipo yasiyokubalika umeonyeshwa kwenye Jedwali Na.58 hapa chini:

**Jedwali 58: Malipo yasiyokubalika**

| Na | Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|
| 1 | Manispaa ya Kigoma | 1,906,780 |
| 2 | Wilaya ya Singida | 2,204,253 |
| | **Jumla** | **4,111,033** |

### 5.1.6 Malipo ya mwaka uliopita yaliyofanyika bila kibali Sh.40,025,931

Uchunguzi wa hati (vocha) za malipo ulibaini kuwa, halmashauri sita (6) zilifanya malipo ya Sh. 40,025,931 kwa ajili ya kulipia madeni ya mwaka wa fedha 2011/12 bila ya

kuidhinishwa katika bajeti ya mwaka 2012/13 kinyume na Agizo Na.22 (1) la LAFM, 2009. Mchanganuo wa halmashauri zilizohusika ni kama inavyoonekana kwenye Jedwali Na.59 hapa chini:

**Jedwali 59: Malipo yaliyofanyika bila kibali**

| Na | Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|
| 1 | Wilaya ya Kondoa | 14,590,000 |
| 2 | Wilaya ya Misenyi | 12,487,425 |
| 3 | Wilaya ya Kasulu | 6,841,506 |
| 4 | Wilaya ya Kahama | 2,087,000 |
| 5 | Wilaya ya Kisarawe | 2,020,000 |
| 6 | Wilaya ya Ukerewe | 2,000,000 |
| | **Jumla** | **40,025,931** |

### 5.1.7 Fedha zilizosalia bila kutumika Sh. 14,778,757,617.09

Wizara ya Fedha ina akaunti kuu ya Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo ambayo inatunza fedha kabla haijazihamishia kwenye akaunti za watekelezaji mbalimbali. Ukaguzi ulibaini kiasi cha Sh. 14,778,757,617.09 cha miaka ya nyuma kilikuwa kwenye akaunti za Halmashauri. Fedha hizo zilitolewa katika mwaka wa fedha 2011/12 lakini zilikuwa hazijatumika na sababu zikiwa ni ucheleweshwaji wa kuhamisha fedha, fedha hizo kukosa matumizi na utaratibu mrefu kwa manunuzi yanayohitaji mikataba. Mchanganuo wa fedha zisizotumika umeonyeshwa katika **kiambatisho Na. VI**. Miradi ambayo haijatekelezwa inaendelea kuwa na madhara katika utendaji wa halmashauri.

Hata hivyo, kiasi cha fedha zilizosalia bila kutumika kimepungua kwa Sh.17,459,161,573.60 ukilinganisha na mwaka wa fedha 2011/12 ambao ulionyesha Sh.32,237,919,190.67 kama fedha zilizosalia bila kutumika.

### 5.1.8 Upungufu wa watumishi 7,471 katika idara za Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo

Tathmini ya idadi ya watumishi wanaotakiwa katika idara za Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo ilibaini kuwa, kwa mujibu wa ikama zilizoandaliwa na halmshauri mbalimbali, halmashauri themanini (80) zilikuwa na upungufu wa

watumishi wapatao 7,471 kama ilivyoonyeshwa katika **kiambatisho Na. XI.** Upungufu wa watumishi unapunguza ufanisi katika utekelezaji na usimamiaji wa shughuli za kilimo na hivyo kukwamisha juhudi za serikali katika kuinua na kuboresha sekta ya kilimo.

### 5.1.9 Upungufu wa Fedha za ruzuku zisizopelekwa Halmashauri Sh. 22,277,845,446

Tathmini ya bajeti zilizotengwa na kuidhinishwa na halmashauri ulibainisha kuwa shughuli mbalimbali za Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo hazikutekelezwa. Kiasi cha Sh. 22,277,845,446 ambacho ni bajeti ya ruzuku kutoka Serikali Kuu hakikupelekwa katika halmshauri hamsini na sita (56) kama ilivyoonyeshwa katika **kiambatisho namba XII.** Upungufu wa fedha za ruzuku zisizopelekwa katika halmashauri kwa mujibu wa bajeti zilizoidhinishwa unaathiri utekelezaji na ufanisi wa usimamizi wa miradi ya programu ya maendeleo ya sekta ya kilimo na hivyo kukwamisha lengo la serikali la kuinua na kuendeleza kilimo.

## 5.2 Mfuko wa Maendeleo ya Afya

### 5.2.1 Bakaa Kubwa ya Fedha isiyotumika Sh. 26,582,155,175

Katika mwaka wa fedha 2012/13 Mamlaka za Serikali za Mitaa zilikuwa na fedha kiasi cha Sh. 101,922,438,330 kwa ajili ya kugharamia shughuli za Mfuko wa Maendeleo ya Afya katika halmashauri. Kiasi kilichotumika kilikuwa ni Sh.75,340,283,154 na kuwa na salio la Sh.26,582,155,175 ambayo ni sawa na asilimia 26 ya fedha iliyokuwepo. Hali hii inaonyesha kwamba huduma zilizokusudiwa kwa jamii hazikutolewa kwa kiwango kilichokusudiwa. Halmashauri zilizohusika zimeonyeshwa katika **kiambatisho Na VII**.

### 5.2.2 Kukosekana kwa taarifa za robo mwaka za mkaguzi wa ndani zinazohusu masuala ya Mfuko wa Maendeleo ya Afya

Tathmini iliyofanywa kwenye vitengo vya ukaguzi wa ndani kwenye halmashauri kumi na tano (15) kwa kipindi cha mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2013 ilionyesha kuwa kitengo cha ukaguzi wa ndani hakikuandaa taarifa za robo mwaka zinazojitegemea za ukaguzi wa Mfuko wa Maendeleo ya Afya ambazo zingeonyesha udhaifu unaohusu mfuko huo kinyume na Aya 6.3(b) ya Mwongozo wa Mpango

Kabambe wa Afya wa mwaka 2011, hivyo shughuli zilizotekelezwa za Mfuko wa Maendeleo ya Afya hazikukaguliwa ili kubainisha mapungufu. Idadi ya halmashauri zimeonyeshwa kwenye Jedwali Na. 60 hapo chini:

**Jedwali 60: Kukosekana kwa taarifa za robo mwaka za mkaguzi wa ndani**

| Na. | Halmashauri |
|---|---|
| 1 | Wilaya ya Handeni |
| 2 | Wilaya ya Korogwe |
| 3 | Wilaya ya Muheza |
| 4 | Wilaya ya Pangani |
| 5 | Jiji la Tanga |
| 6 | Wilaya ya Hai |
| 7 | Wilaya ya Moshi |
| 8 | Wilaya ya Same |
| 9 | Wilaya ya Kongwa |
| 10 | Manispaa ya Kigoma |
| 11 | Manispaa ya Tabora |
| 12 | Wilaya ya Urambo |
| 13 | Manispaa ya Sumbawanga |
| 14 | Mji wa Mpanda |
| 15 | Wilaya ya Karagwe |

### 5.2.3 Masurufu yasiorejeshwa, Sh.28,605,000

Masurufu yenye jumla ya Sh.28,605,000 yanayohusu halmashauri saba (7) hayakurejeshwa baada ya kazi iliyokusudiwa kukamilika kinyume na Agizo 40(3) la LAFM, 2009. Orodha ya halmashauri na kiasi cha masurufu ambayo hayajarejeshwa imeonyeshwa kwenye jedwali Na.61 hapo chini:

**Jedwali 61: Masurufu yasiyorejeshwa**

| Na. | Halmashauri | Kiasi (Sh) |
|---|---|---|
| 1 | Wilaya ya Bunda | 7,795,000 |
| 2 | Wilaya ya Tandahimba | 6,594,000 |
| 3 | Wilaya ya Monduli | 4,099,000 |
| 4 | Wilaya ya Handeni | 3,825,000 |

| | | |
|---|---|---|
| 5 | Wilaya ya Lushoto | 2,400,000 |
| 6 | Wilaya ya Mbinga | 1,992,000 |
| 7 | Wilaya ya Arusha | 1,900,000 |
| **Jumla** | | **28,605,000** |

### 5.2.4 Malipo yenye nyaraka pungufu Sh. 1,660,648,887

Kulikuwa na malipo ya jumla ya Sh.1,660,648,887 kwenye halmashauri hamsini na nne (54) ambayo yalikuwa na nyaraka pungufu kinyume na Agizo Na.8(2)(c) la LAFM, 2009. Uhalali wa matumizi yaliyofanywa haukuweza kuthibitishwa wakati wa ukaguzi. Chamwino ilikuwa na sehemu kubwa ya asilimia 21 ikifuatiwa na Halmashauri ya Manispaa ya Ilala yenye asilimia 16 na ya tatu ni Halmashauri ya Rungwe iliyokuwa na asilimia 8. Orodha ya halmashauri hizo na kiasi kilichohusishwa kimeonyeshwa kwenye **Kiambatisho Na.XIII**

Hata hivyo kiasi cha malipo yenye nyaraka pungufu kimepungua kutoka mwaka 2010/11 hadi 2011/12 kwa Sh.1,436,601,225 na kuongezeka kwa Sh.1,389,584,288 kwa mwaka 2011/12 hadi 2012/13.

### 5.2.5 Kukosekana kwa hati za malipo, Shs 927,786,976

Katika kipindi cha mwaka 2012/13, hati za malipo zenye jumla ya Sh. 927,786,976 hazikuwasilishwa wakati wa ukaguzi kinyume na Agizo 34(1) la LAFM, 2009, hivyo uhalali wa malipo hayo kwenye halmashauri kumi na saba (17) haukuweza kuthibitishwa. Maelezo ya hati za malipo ambazo hazikuwasilishwa kwa kila halmashauri ni kama inavyoonekana kwenye Jedwali Na.62 hapo chini:

Hata hivyo jumla ya hati za malipo ambazo hazikuwasilishwa wakati wa ukaguzi zimeongezeka kutoka mwaka 2010/2011 hadi 2011/2012 kwa Sh.631,699,698.

**Jedwali 62: Hati za malipo zilizokosekana**

| Na. | Halmashauri | Kiasi (Sh) |
|---|---|---|
| 1 | Wilaya ya Bariadi | 575,028,244 |
| 2 | Wilaya ya Musoma | 77,114,000 |
| 3 | Wilaya ya Kilwa | 65,406,990 |
| 4 | Wilaya ya Chamwino | 65,158,200 |
| 5 | Wilaya ya Bukombe | 35,373,972 |
| 6 | Wilaya ya Longido | 29,766,385 |
| 7 | Wilaya ya Namtumbo | 24,881,000 |
| 8 | Wilaya ya Maswa | 15,327,500 |
| 9 | Wilaya ya Manyoni | 7,827,648 |
| 10 | Wilaya ya Kilosa | 6,369,000 |
| 11 | Manispaa ya Lindi | 5,039,537 |
| 12 | Wilaya ya Masasi | 4,942,000 |
| 13 | Wilaya ya Sumbawanga | 3,840,000 |
| 14 | Wilaya ya Monduli | 3,732,500 |
| 15 | Wilaya ya Newala | 3,225,000 |
| 16 | Wilaya ya Mbinga | 2,780,000 |
| 17 | Wilaya ya Rufiji/Utete | 1,975,000 |
| **Jumla** | | **927,786,976** |

### 5.2.6 Matumizi yaliyolipiwa kwenye vifungu visivyostahili Sh.383,197,259

Matumizi yenye jumla ya Sh.383,197,259 kwenye halmashauri ishirini na nane (28) yalilipiwa kwenye vifungu visivyostahili kinyume na Agizo 23(1) la LAFM, 2009 kama inavyoonekana kwenye **Kiambatisho Na. XIV**.

### 5.2.7 Matumizi yaliyofanywa nje ya bajeti iliyoidhinishwa Sh.564,460,287

Katika kipindi cha mwaka 2012/13, halmashauri ishirini na tano zililipa jumla ya Sh.564,460,287 kwa ajili ya shughuli mbalimbali kutoka katika Mfuko wa Maendeleo wa Afya. Hata hivyo shughuli zilizotekelezwa hazikuwa na uhusiano na shughuli zilizokusudiwa kutekelezwa kutokana na kutokuwepo kwenye mpango kabambe wa afya wa Halmashauri (CCHP) wa mwaka 2012/2013. Maelezo zaidi yako kwenye **Kiambatisho XV**.

### 5.2.8 Malipo yasiyokubalika ya kodi ya ongezeko la thamani Sh.5,819,093

Halmashauri mbili (2) zilinunua bidhaa na huduma kutoka kwa wazabuni mbalimbali ambapo kiasi kilicholipwa kilijumuisha kodi ya ongezeko la thamani la Sh. 5,819,093. Hata hivyo makubaliano yaliyofikiwa kati ya washirika wa maendeleo na serikali ni kwamba malipo kwa ajili ya ununuzi wa bidhaa, vifaa vya ujenzi na huduma, kwa kutumia fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Afya yasitozwe kodi ya ongezeko la thamani na serikali. Jedwali Na.63 linaonyesha halmashauri zilizofanya malipo yasiyokubalika.

**Jedwali 63: Malipo yasiyokubalika ya kodi ya ongezeko la thamani**

| Na. | Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|
| 1 | Wilaya ya Singida | 3,794,093 |
| 2 | Wilaya ya Manyoni | 2,025,000 |
| **Jumla** | | **5,819,093** |

### 5.2.9 Upungufu wa wataalamu katika Idara ya Afya

Kutokana na muundo wa utumishi katika kila halmashauri, kuna idadi maalum ya watumishi/wataalamu wanaopaswa kufanya kazi katika idara ya afya ili kuboresha utendaji na kuongeza ufanisi katika kutoa huduma za afya ndani ya halmashauri husika. Hata hivyo ukaguzi ulibaini upungufu wa wataalamu wapatao elfu kumi na moja, mia saba na nne (11,704) wa Idara za Afya kwenye halmashauri hamsini na sita. Idadi ya upungufu wa wataalam kwenye kila halmashauri umeonyeshwa kwenye **Kiambatisho Na.XVI**

## 5.3 Mfuko wa Maendeleo ya Jamii Tanzania (TASAF)

### 5.3.1 Miradi yenye thamani ya Sh. 1,090,493,650.42 iliyokuwa kwenye bajeti haikutekelezwa

Ukaguzi ulibaini utekelezaji wa miradi mingi ulikuwa haujaanza ingawa halmashauri zilikwishahamisha fedha kwenda kwenye akaunti za miradi husika kama ilivyoonyeshwa katika Jedwali Na. 64 hapo chini:

Hata hivyo hali imeboreshwa kwa kiasi kwani kwa mwaka 2011/12 kiasi cha miradi iliyopelekewa fedha na haikutekelezwa ilikuwa Sh.1,651,661,060.43.

**Jedwali 64: Miradi iliyopelekewa fedha lakini haijafanyika**

| Na. | Halmashauri | Maelezo | Kiasi (Sh) |
|---|---|---|---|
| 1 | Wilaya ya Rorya | Ukarabati wa barabara, mabwawa na mashine za kusaga | 493,000,000 |
| 2 | Wilaya ya Nanyumbu | Miradi ya ujenzi na uhifadhi wa barabara | 295,452,411 |
| 3 | Wilaya ya Morogoro | Ujenzi wa barabara za Kolero, Kungwi, Kanisani na Lundi hadi Tambuu | 199,454,800 |
| 4 | Wilaya ya Bagamoyo | Ujenzi wa soko la samaki | 57,883,014 |
| 5 | Wilaya ya Mvomero | Ufugaji wa kuku na mbuzi | 43,528,675 |
| 8 | Wilaya ya Muleba | Kupachika dari katika shule ya msingi Makangora | 1,174,750 |
| | **Jumla** | | **1,090,493,650** |

### 5.3.2 Miradi iliyokamilika lakini haijaanza kutoa huduma Sh.393,488,168

Wakaguzi walitembelea miradi iliyokwisha kamilika katika halmashauri na kubaini kuwa ingawa miradi hiyo imekamilika lakini bado haijaanza kutumika kama ilivyoonyeshwa katika Jedwali Na. 65 hapo chini:

Hata hivyo hakuna maboresho katika kutumia miradi iliyokamilika kwani kwa mwaka wa fedha 2011/12 kulikuwa na miradi yenye thamani ya Sh.69,630,512.32 ambayo haijaanza kutumika ingawa imekamilika.

**Jedwali 65: Miradi iliyokamilika lakini haijaaza kutumika**

| Na. | Halmashauri | Mradi | Kiasi (Sh) |
|---|---|---|---|
| 1 | Wilaya Handeni | Ujenzi wa tanki la maji na hosteli | 11,124,298 |
| 2 | WilayaShinyanga | Ujenzi wa soko | 59,647,550 |
| 3 | Wilaya Longido | Ujenzi wa nyumba za walimu, mashimo ya vyoo na bwalo la chakula | 145,457,320 |
| 4 | Wilaya Rorya | Ujenzi wa lambo | 177,259,000 |
| | **Jumla** | | **393,488,168** |

### 5.3.3 Miradi ambayo haijakamilika Sh. 1,576,618,867

Ukaguzi umebaini kuwa baadhi ya miradi iliyopangwa kutekelezwa kwa mwaka wa fedha 2012/13 haijakamilika kwa kiasi cha shilingi 1,576,618,867. Orodha ya miradi hiyo ambayo haijakamilika ni kama ilivyoonyeshwa kwenye Jedwali Na. 66 hapa chini:

Hata hivyo kuna maboresho katika kukamilisha miradi iliyopangwa kwani miradi isiyokamilika kwa mwaka 2010/11 ilikuwa Sh.3,035,766,732 ikilinganishwa na Sh.1,576,618,867 kwa mwaka 2012/13.

**Jedwali 66: Miradi ambayo haijakamilika**

| Na. | Halmashauri | Mradi | Kiasi (Sh) |
|---|---|---|---|
| 1 | Wilaya ya Muleba | Ujenzi wa mashimo ya vyoo shule ya msingi Kangaza | 6,818,000 |
| 2 | Wilaya ya Meatu | Ujenzi wa barabara za Mshikamano-Malugala na Kabondo-Mwafuguji | 3,500,000 |
| 3 | Wilaya ya Bunda | Ujenzi wa barabara ya Busambu-Namalana na Nyaburundu –Marakmbeka jumla ya km 10.1 | 1,738,398.5 |
| 4 | Wilaya ya Rorya | Ujenzi wa lambo Panyako | 39,754,320 |
| 5 | Manispaa ya Shinyanga | Ukarabati wa barabara za Ihapa, Ibinzamata, Songambele na Bushola jumla ya km 17.3 | 9,025,000 |
| 6 | Wilaya ya | Upandaji miti na kuzuia | 36,876,101 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | Hanang” | mmomonyoko wa udongo maeneo ya Ming”enyi na Garbapi | |
| 8 | Wilaya ya Mbulu | Ujenzi wa vyoo kituo cha kutunza mazingira Masieda | 16,363,335 |
| 9 | Mji wa ya Korogwe | Ujenzi zahanati ya Mtonga Sh. 14,016,055 na Zahanati ya Msambiazi Sh.17,380,617 | 31,396,672 |
| 10 | Wilaya ya Kilwa | Ukarabati wa barabara kilometa 16,na ujenzi wa OPD Mchakama na Kiranjeranje | 161,585,196 |
| 11 | Wilaya ya Ruangwa | Ujenzi na ukarabati wa barabara za Halmashauri ya Wilaya. | 729,425,996.37 |
| 12 | Wilaya ya Tunduru | Ukarabati wa barabara ya Majimaji-Magomeni | 15,224,559.60 |
| 13 | Wilaya ya Bahi | Ukarabati wa lambo kijiji cha Chibeela na ujenzi wa mabanda ya ng’ombe | 43,726,150 |
| 14 | Wilaya ya Kiteto | Ukarabati wa barabara kijiji cha Mesere | 31,433,752 |
| 15 | Wilaya ya Ulanga | Mradi wa mashine ya kusaga na shughuli za useremala | 18,669,647 |
| 16 | Wilaya ya Kondoa | Mradi wa usambazaji wa maji | 125,351,500 |
| 17 | Wilaya ya Babati | Ujenzi wa soko kijiji cha Vilima vitatu | 72,720,324 |
| 18 | Wilaya ya Longido | Ujenzi wa barabara na makalavati | 233,009,917 |
| | | **Jumla** | **1,576,618,867** |

### 5.3.4 Fedha za TASAF Sh. 121,281,774 hazijapokelewa katika akaunti ya Halmashauri ya Mkinga

Malipo kutoka TASAF makao makuu kwenda halmashauri ya Wilaya ya Mkinga kwa mwaka wa fedha 2012/13 linaonyesha kuwa kiasi cha Sh.121,281,774 zilipelekwa katika halmashauri ya wilaya ya Mkinga lakini uchambuzi wa kikaguzi umeonyesha kuwa fedha hizo hazijaingia kwenye akaunti ya halmashauri ya Mkinga.

Fedha hizo zilikusudiwa kutumika kwa ajili ya kutekeleza miradi iliyoonyeshwa katika Jedwali Na. 67 hapo chini:

**Jedwali 67: Fedha zilizohamishwa lakini hazijapokelewa**

| Halmashauri | Mradi | Kiasi(Sh) |
|---|---|---|
| Wilaya ya Mkinga | Upandaji miti kiasi cha ekari 1200 katika vijiji vya Mwakikaya, Kisiwani, Mayoyo na Kibewani | 121,281,774 |
| | **Jumla** | **121,281,774** |

### 5.3.5 Matumizi yaliyolipwa kutoka kwenye vifungu visivyohusika Sh.75,933,865.15

Matumizi yenye thamani ya Sh.75,933,865.15 yalilipiwa kwenye vifungu visivyostahili kinyume na Kifungu 21 cha LAFM, 2009 kama ilivyoonyeshwa katika Jedwali Na. 68 hapo chini:

Hata hivyo matumizi yaliyolipiwa kwenye vifungu visivyohusika yameongezeka kwa kiasi cha Sh. 61,670,895.47 ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2011/12.

**Jedwali 68: Matumizi yaliyolipiwa kwenye vifungu visivyohusika**

| Na. | Halmashauri | Kiasi (Sh) |
|---|---|---|
| 1 | Wilaya ya Bunda | 589,130 |
| 2 | Wilaya ya Musoma | 6,442,433 |
| 3 | Wilaya ya Rorya | 20,040,000 |
| 4 | Wilaya ya Shinyanga | 6000,000 |
| 5 | Wilaya ya Ngorongoro | 260,000 |
| 6 | Wilaya ya Handeni | 6,721,679.29 |
| 7 | Wilaya ya Liwale | 7,636,675.86 |
| 8 | Wilaya ya Longido | 12,198,547 |
| 9 | Wilaya ya Lindi | 3,315,000 |
| 10 | Wilaya ya Kilosa | 815,000 |
| 11 | Wilaya ya Tunduru | 5,957,700 |
| | **Jumla** | **75,933,865.15** |

### 5.3.6 Malipo yenye hati pungufu Sh.385,477,516

Ukaguzi wa hati za malipo ulibaini kuwa kulikuwa na malipo yenye thamani ya Sh.385,477,516 ambayo hayakuwa na viambatanisho vinavyohusika hii ni kinyume na Agizo Na. 10(2)

(d) la LAFM, 2009 kama ilivyoonyeshwa katika Jedwali Na. 69 hapo chini:

Hata hivyo kwa mwaka 2011/12 hadi 2012/13 hati za malipo zisizo na viambatanisho ziliongezeka kwa Sh. 232,133,430.89

**Jedwali 69: Malipo yenye hati pungufu**

| Na. | Halmashauri | Kiasi(Sh) |
|---|---|---|
| 1 | Wilaya ya Rorya | 1,900,000 |
| 2 | Wilaya ya Sengerema | 9,630,000 |
| 3 | Wilaya ya Karatu | 2,070,000 |
| 4 | Wilaya ya Longido | 234,955,721 |
| 5 | Wilaya ya Liwale | 17,673,694 |
| 6 | Manispaa ya Lindi | 675,493.46 |
| 7 | Wilaya ya Nachingwea | 24,220,700 |
| 8 | Wilaya ya Ruangwa | 19,570,500 |
| 9 | Wilaya ya Kilosa | 8,817,257.60 |
| 10 | Manispaa ya Mtwara Mikindani | 2,444,700 |
| 11 | Wilaya ya Bagamoyo | 57,899,450 |
| 12 | Wilaya ya Kisarawe | 1,340,000 |
| 13 | Wilaya ya Misungwi | 285,000 |
| 14 | Wilaya ya Kiteto | 2,435,000 |
| 15 | Manispaa ya Songea | 780,000 |
| | **Jumla** | **384,697,516** |

### 5.3.7 Kukosekana kwa hati za malipo Sh. 14,467,373

Kulikuwa na malipo yenye thamani ya Sh. 14,467,373 ambayo hati zake za malipo hazikuwasilishwa kwa ajili ya ukaguzi hii ni kinyume na Agizo Na.104(2) la LAFM, 2009. Katika mazingira haya, uhakika na uhalali wa hayo matumizi haukuweza kuthibitika. Ufafanuzi unapatikana katika jedwali Na. 70 hapa chini:

**Jedwali 70: Hati za Malipo zilizokosekana**

| Na. | Halmashauri | Kiasi(Sh) |
|---|---|---|
| 1 | Wilaya ya Bariadi | 440,000 |
| 2 | Wilaya ya Sengerema | 9,630,000 |
| 3 | Wilaya ya Kilosa | 2,275,000 |
| 4 | Wilaya ya Kilwa | 675,493 |
| 5 | Wilaya ya Nachingwea | 1,446,880 |
| **Jumla** | | **14,467,373** |

### 5.3.8 Ongezeko la Mali, Mitambo na Vifaa bila viambatanisho Sh.351,395,763

Taarifa za hesabu za Halmashauri ya Jiji la Mwanza zilionyesha ongezeko la Mali, Mitambo na Vifaa kwa kiasi cha Sh.351,395,763. Hata hivyo, haikuweza kuwasilisha viambatanisho vya ongezeko hilo hivyo uhalali wa gharama hiyo haukuweza kuthibitishwa.

## 5.4 Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji (WSDP)

### 5.4.1 Masurufu yasiyorejeshwa Sh.4,100,000

Masurufu yanayofikia kiasi cha Sh. 4,100,000 kwa halmashauri mbili yalitolewa kipindi cha mwaka wa fedha 2012/13, hayakurejeshwa baada ya kukamilika kwa shughuli zilizokusudiwa. Hii ni kinyume na Agizo Na. 40(3) la LAFM, 2009. Orodha ya halmashauri husika imeonyeshwa kwenye Jedwali Na.71 hapa chini

Hata hivyo, masurufu yasiyorejeshwa yamepungua kutoka Sh. 5,273,600 mwaka 2011/12 hadi Sh. 4,100,000 kwa mwaka 2012/13.

**Jedwali 71: Masurufu yasiyorejeshwa**

| Na. | Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---:|
| 1 | Manispaa ya Lindi | 3,600,000 |
| 2 | Wilaya ya Karatu | 500,000 |
| **Jumla** | | **4,100,000** |

### 5.4.2 Malipo yenye nyaraka pungufu Sh.1,422,428,791

Kulikuwa na malipo yenye nyaraka pungufu ya jumla ya kiasi cha Sh. 1,422,428,791 yaliyofanywa kinyume na Kanuni Na. 95(4) ya Sheria ya Fedha za Umma ya mwaka 2001 (iliyorekebishwa 2004) na Kifungu Na. 45(5) cha Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa ya mwaka 1982 pamoja na Agizo Na. 8(2)(c) la LAFM, 2009. Maelezo zaidi yameonyeshwa kwenye kiambatisho Na.XVII cha ripoti hii.

Hata hivyo malipo hayo yameongezeka kwa kiasi cha Sh.1,000,791,275 kutoka mwaka 2011/12 mpaka Sh.1,422,428,791 kwa mwaka 2012/13.

### 5.4.3 Upungufu wa wataalamu Idara ya Maji katika Halmashauri

Ukaguzi ulibaini upungufu wa wataalamu wa maji katika idara za maji katika halmashauri nyingi nchini na hii imeathiri utekelezaji na usimamiaji wa miradi ya maji katika halmashauri. Ukaguzi uliofanyika katika halmashauri mia moja ishirini na tisa (129) ulionyesha upungufu wa wataalamu wa maji kama ilivyoonyeshwa kwenye kiambatisho Na. XVIII cha ripoti hii.

### 5.4.4 Fedha zilizotengwa kwa ajili ya usafi wa mazingira katika shule za msingi hazikupelekwa Sh.1,512,000,000

Ukaguzi ulibaini kuwa kiasi cha Sh.1,512,000,000 kilitengwa kwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa ajili ya matumizi ya shughuli za usafi wa mazingira katika shule za msingi. Hata hivyo fedha hizo hazikupelekwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa kuwa Wizara ilishindwa kutekeleza masharti ya mradi kama ilivyotakiwa.

## 5.5 MIRADI MINGINE

### 5.5.1 Malipo yenye nyaraka pungufu Sh. 3,579,568,088 na Dola za Marekani 2,958,445.22

Ukaguzi wa hati za malipo na viambatisho vyake umebaini malipo yenye thamani ya Sh.3,579,568,088 na Dola za Marekani 2,958,445.22 ambayo yamekosa viambatisho vinavyohusika kama ilivyoonyeshwa kwenye Jedwali Na. 72 hapa chini:

Hata hivyo, matumizi yenye nyaraka pungufu kwa mwaka 2012/13 yameongezeka ikilinganishwa na Sh.77,621,537 na dola za Marekani 154,071.29 kwa mwaka 2011/12.

**Jedwali 72: Matumizi yenye nyaraka pungufu**

| Na | Aina ya Mradi | Kiasi (Sh.) | Kiasi ( Dola za Marekani) |
|---|---|---|---|
| 1 | Mradi wa Uzalishaji katika Kilimo Afrika ya Mashariki (EAAPP) | 15,196,767 | |
| 2 | Programu ya Maboresho ya Sheria | 13,340,000 | |
| 3 | Mradi wa Usimamizi na Uendelevu wa Rasilimali za Madini (SMMRP) | 43,129,200 | |
| 4 | Programu ya Maboresho katika Utumishi wa Umma (II) | 68,890,000 | |
| 5 | Mradi wa Kuboresha Miji Muhimu Tanzania (TSCP) | 1,427,446,216 | |
| 6 | Chama cha Msalaba Mwekundu - UNDP | 35,027,000 | |
| 7 | Katibu Tawala wa Mikoa wa Kilimanjaro - UNDP | 11,722,000 | |
| 8 | Mradi wa Sayansi na Teknonolojia Elimu ya Juu | | 109,457.98 |
| 9 | Mfuko wa Kimataifa wa Kupambana na Ukimwi, Kifua Kikuu na Malaria-Programu ya Kitaifa ya Kudhibiti Ukimwi | 1,481,800,080 | |
| 10 | Mradi wa Kuboresha Ushindani wa Biashara katika Sekta Binafsi Nchini (Private Sector Competitiveness Project (PSCP) - Component I) | | 2,848,987.24 |
| 11 | Wakala wa Kusimamia Usafiri wa Haraka Dar es Salaam (DART)) | 63,652,000 | |
| 12 | Mradi wa Kuhakikisha Usalama wa Chakula (Accelerated Food Security Project) | 419,364,825 | |
| **Jumla** | | **3,579,568,088** | **2,958,445.22** |

## 5.5.2 Matumizi yasiyokubalika Sh.673,335,837.79

Kiasi cha Sh.673,335,837.79 kililipwa na miradi mbalimbali kwa matumizi yasiyohusiana na shughuli za miradi kama ilivyoonyeshwa kwenye Jedwali Na. 73 hapa chini:

**Jedwali 73: Matumizi yasiyokubalika**

| Na. | Jina la Mradi | Kiasi(Sh) |
|---|---|---|
| 1 | Mfuko wa Kimataifa wa Kupambana na Ukimwi, Kifua Kikuu na Malaria- Programu ya Kitaifa ya Kudhibiti Ukimwi | 65,016,000 |
| 2 | Mradi wa Usimamizi Endelevu wa Rasilimali za Madini (SMMRP) | 85,525,100 |
| 3 | Programu ya Usambazaji wa Maji Vijijini na Usafi wa Mazingira - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (RWSSP) | 8,231,740.82 |
| 4 | Mradi wa Kuboresha Miji Muhimu Tanzania (TSCP)-Kigoma | 455,170,586 |
| 5 | Programu ya Maboresho ya Sheria | 59,392,410.97 |
| **Jumla** | | **673,335,837.79** |

Hata hivyo mwelekeo unaonyesha kuwa matumizi yasiyokubalika yameongezeka ikilinganishwa na mwaka 2011/12 ambapo kulikuwa na Sh.299,227,621 na Dola za Marekani 16,976.80.

## 5.5.3 Masurufu yasiyorejeshwa Sh.28,727,900

Mradi wa Uzalishaji katika Kilimo Afrika ya Mashariki (EAAPP) ulitoa kiasi cha Sh. 28,727,900 kama masurufu kwa watumishi mbalimbali kwa ajili ya kutekeleza shughuli za mradi. Hatahivyo, matumizi ya kiasi hicho hayajaonyeshwa kinyume na kanuni 103(1) ya Sheria ya Fedha za Umma ya mwaka 2001(iliyorekebishwa 2004). Kiasi hicho kimepungua ikilinganishwa na Sh.11,641,000 na Dola za Marekani 159,913.91 kilichoripotiwa mwaka 2011/12.

### 5.5.4 Mikataba iliyosainiwa ambayo haikuwepo katika Mpango kazi wa mwaka Sh.803,038,366

Mikataba 9 yenye thamani ya Sh.803,038,366 ilisainiwa na uongozi wa Mfuko Mkuu–Mpango wa Maboresho na Usimamizi wa Fedha (PFMRP) miezi ya mwisho ya mwaka na haikuwepo katika mpango kazi wa mwaka 2012/13.

### 5.5.5 Malipo yasiyo na tija- USD 50,813.19

Mradi wa Sayansi na Teknolojia Elimu ya Juu (STHEP) katika Taasisi ya Teknolojia Dar-es-salaam ilimlipa M/S Agumba Computers Ltd malipo ya awali ya asilimia 10, Dola za Marekani 50,813.19 ya gharama yote ya mkataba. Hata hivyo, mzabuni hajawasilisha bidhaa kwa muda wa miezi kumi na nane (18) sasa kuanzia tarehe 17/07/2012. Hali kadhalika mkataba haukuwa wazi kwa vile haukuonyesha kipindi cha utekelezaji wa mkataba ambao ungesaidia uongozi wa mradi kutoza tozo kwa ajili ya ucheleweshaji wa kazi kama walivyokubaliana pande zote mbili.

### 5.5.6 Malipo ya ada ya ushauri yaliyolipwa zaidi Dola za Marekani 54,033

Kiasi cha Dola za Marekani 54,033 kililipwa zaidi kutoka kwenye Mfuko wa Biashara na Uchumi kwa ajili ya kuratibu maonyesho na kongamano la wawekezaji kwa ajili ya Mradi wa Kukuza Kilimo Kusini mwa Tanzania (SAGCOT).

## SURA YA SITA

## MAPITIO YA TARATIBU NA MIKATABA YA MANUNUZI

### 6.0 Utangulizi

Katika kipindi cha ukaguzi wa taarifa za fedha za miradi ya maendeleo kwa mwaka 2012/13, ukaguzi ulibaini mapungufu katika manunuzi ya huduma na vifaa yaliyofanyika kutoka Mfuko wa Huduma za Jamii, Programu ya Maendeleo Sekta ya Kilimo, Programu ya Mradi wa Maendeleo ya Sekta ya Maji, Mfuko wa Maendeleo ya Sekta ya Afya na miradi mingine ya maendeleo. Mapungufu yaliyobainika yalitokana kwa kiasi kikubwa na kutozingatia Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka, 2004 na Kanuni zake za mwaka 2005 kama ilivyoonyeshwa hapa chini:

### 6.1 Programu ya Maendeleo katika Sekta ya Kilimo

#### 6.1.1 Manunuzi yaliyofanywa bila idhini ya Bodi za Zabuni Sh.119,854,861

Manunuzi mengi yaliyofanywa kwa mikataba yalikuwa na mapungufu mengi kutokana na usimamizi mbovu wa mikataba. Ilibainika kuwa halmashauri nne (4) zilifanya manunuzi ya kiasi cha Sh.119,854,861 bila idhini ya Bodi ya Zabuni kinyume na kanuni Na.40 na 41 ya Kanuni za Manunuzi ya Umma, 2005. Mchanganuo wa halmashauri zilizohusika ni kama inavyoonekana kwenye jedwali Na.74 hapa chini:-

**Jedwali 74: Manunuzi yaliyofanywa bila idhini ya Bodi za Zabuni**

| Na | Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---:|
| 1 | Wilaya ya Kasulu | 27,435,930 |
| 2 | Wilaya ya Tarime | 14,480,000 |
| 3 | Wilaya ya Mufindi | 35,183,416 |
| 4 | Wilaya ya Mbinga | 42,755,515 |
| | **Jumla** | **119,854,861** |

Hata hivyo, kiasi cha manunuzi yaliyofanywa bila idhini ya Bodi za Zabuni kimepungua kwa Sh.150,247,851 ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2011/12 ambapo kulikuwa na Sh.270,102,712.

### 6.1.2 Ununuzi wa mali toka kwa wauzaji binafsi bila kibali cha Bodi ya Zabuni Sh.34,610,451

Kanuni Na. 68(5) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za mwaka 2005, ambayo inaagiza kuwepo na orodha ya wauzaji waliopendekezwa na Bodi ya Zabuni na hatimaye taasisi inayofanya ununuzi iandae utaratibu wa kupata bei kutoka kwa wauzaji wote waliochaguliwa. Hata hivyo, halmashauri nne (4) zilikiuka Kanuni Na. 68 (5) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za mwaka 2005 kwa kufanya ununuzi wa mali, kazi za ujenzi na zisizo za ushauri kutoka kwa wauzaji ambao hawakuthibitishwa na Bodi za Zabuni kama ilivyoonyeshwa kwenye Jedwali Na. 75 hapa chini:

**Jedwali 75: Ununuzi wa mali toka kwa wauzaji binafsi bila kibali cha Bodi ya Zabuni**

| Na | Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|
| 1 | Wilaya ya Kasulu | 22,652,000 |
| 2 | Wilaya ya Ruangwa | 7,596,650 |
| 3 | Wilaya ya Arusha | 1,211,801 |
| 4 | Wilaya ya Mwanga | 3,150,000 |
| | **Jumla** | **34,610,451** |

### 6.1.3 Manunuzi yaliyofanywa bila kushindanisha Wazabuni Sh.21,358,611

Kufuata taratibu za Sheria za Manunuzi ni suala la lazima katika kuhakikisha kuwa gharama nafuu za manunuzi zinapatikana kutoka kwa watoa huduma. Halmashauri tatu (3) zilifanya manunuzi yenye thamani ya Sh.21,358,611 bila kushindanisha wazabuni. Hii ni kinyume na Kanuni Na. 68 (4) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma, 2005. Mchanganuo wa Halmashauri zilizohusika ni kama inavyoonekana kwenye jedwali Na. 76 hapa chini:-

**Jedwali 76: Manunuzi yaliyofanywa bila kushindanisha Wazabuni**

| Na | Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|
| 1 | Wilaya ya Kondoa | 2,999,000 |
| 2 | Wilaya ya Kibondo | 8,129,611 |
| 3 | Manispaa ya Ilala | 10,230,000 |
| | **Jumla** | **21,358,611** |

### 6.1.4 Manunuzi ya mali na vifaa bila kuingizwa kwenye daftari Sh.47,475,847.76

Kumbukumbu kwa ajili ya matumizi ya vifaa hazikutunzwa ipasavyo na hivyo haikuwa rahisi kuchunguza matumizi ya vifaa hivyo kinyume na Agizo Na. 54(3) la LAFM, 2009. Pia matumizi ya vifaa vyenye thamani ya Sh.47,475,847.76 hayakuweza kubainika kwasababu halmashauri kumi na moja (11) hazikuingiza vifaa zilizonunua kwenye daftari. Mchanganuo wa halmashauri zilizohusika ni kama inavyoonekana kwenye Jedwali Na. 77 hapa chini:-

**Jedwali 77: Mali na vifaa ambavyo havikuingizwa kwenye daftari**

| Na | Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---:|
| 1 | Wilaya ya Chamwino | 5,182,900 |
| 2 | Wilaya ya Kongwa | 7,000,000 |
| 3 | Wilaya ya Singida | 6,675,650 |
| 4 | Wilaya ya Ruangwa | 4,312,194 |
| 5 | Wilaya ya Mtwara | 1,449,858.76 |
| 6 | Wilaya ya Geita | 4,823,500 |
| 7 | Wilaya ya Mwanga | 5,773,295 |
| 8 | Wilaya ya Mbulu | 2,459,800 |
| 9 | Wilaya ya Ileje | 1,675,000 |
| 10 | Wilaya ya Kyela | 5,200,000 |
| 11 | Wilaya ya Sumbawanga | 2,923,650 |
| | **Jumla** | **47,475,847.76** |

Hii inaweza kusababisha matumizi mabaya ya rasilimali bila kugundulika.

### 6.1.5 Mali na Vifaa Vilivyolipiwa lakini havikupokelewa Sh. 84,249,527

Mali na vifaa vya thamani ya Sh. 84,249,527 vilivyonunuliwa kwa kutumia fedha za Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo havikupokelewa. Hii ni kinyume na Agizo Na. 71 (b) la LAFM, 2009. Mchanganuo wa halmashauri nne (4) zilizohusika ni kama inavyoonekana kwenye jedwali Na. 78 hapa chini:

**Jedwali 78 : Mali na Vifaa Vilivyonunuliwa lakini Havikupokelewa**

| Na | Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|
| 1 | Wilaya ya Bukoba | 46,694,527 |
| 2 | Wilaya ya Manyoni | 25,000,000 |
| 3 | Manispaa ya Tabora | 9,255,000 |
| 4 | Jiji la Mwanza | 3,300,000 |
| | **Jumla** | **84,249,527** |

Hata hivyo, kiasi cha mali na vifaa vilivyonunuliwa lakini havikupokelewa kimeongezeka kwa Sh.7,702,664 ikilinganishwa na mwaka 2011/12 ambao ulikuwa na Sh.76,546,863 kama mali na vifaa vilivyonunuliwa lakini havikupokelewa.

### 6.1.6 Mafuta yaliyotumika bila kuonyeshwa katika leja za magari Sh. 23,009,441

Tathmini ya udhibiti na usimamizi wa mafuta ilionyesha kuwa, kiasi cha lita 10,297 za mafuta yenye thamani ya Sh.23,009,441 kilionyeshwa katika leja za mafuta kimetumika. Hata hivyo, ukaguzi wa leja zinazotunza taarifa za magari ulibaini kuwa mafuta hayo hayakuonyeshwa katika leja hizo. Hii inaashiria kuwa mafuta yaliyotolewa hayakutumiwa na magari ya halmashauri husika. Mchanganuo wa halmashauri saba (7) zilizohusika ni kama inavyoonekana kwenye jedwali Na. 79 hapa chini:

**Jedwali 79: Mafuta yaliyotumika bila kuonyeshwa katika leja za magari**

| Na | Halmashauri | Lita | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|
| 1 | Wilaya ya Singida | 3,190 | 6,675,650 |
| 2 | Wilaya ya Kiteto | 2,500 | 6,490,000 |
| 3 | Wilaya ya Mtwara | 1,146 | 2,329,644 |
| 4 | Wilaya ya Iramba | 1,000 | 2,125,000 |
| 5 | Wilaya ya Ruangwa | 870 | 1,914,000 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 6 | Wilaya ya Kibaha | 921 | 1,800,147 |
| 7 | Wilaya ya Ileje | 670 | 1,675,000 |
| | **Jumla** | **10,297** | **23,009,441** |

## 6.2 Mfuko wa Maendeleo ya Afya

### 6.2.1 Manunuzi ya bidhaa na huduma bila idhini ya Bodi za Zabuni Sh. 904,023,258

Manunuzi mengi yanayopangwa kufanyika hayatekelezwi kikamilifu kutokana na usimamizi hafifu wa mikataba. Usimamizi wa mikataba ni mchakato unaoziwezesha pande zote mbili kutimiza matakwa na majukumu yaliyoanishwa kwenye mkataba ili kufikia malengo yaliyokusudiwa. Ukaguzi ulibaini kuwa halmashauri kumi na tatu (13) zilifanya manunuzi ya kiasi cha Sh. 904,023,258 kutoka kwa wazabuni mbalimbali bila idhini ya Bodi za Zabuni kinyume na Kanuni Na. 40 na 41 ya Sheria ya Manunuzi ya Umma,2004 ambazo zinataka mananuzi yote yapitishwe na kuidhinishwa na afisa masuuli na kupewa kibali na bodi ya zabuni. Mchanganuo wa halmashauri zilizohusika ni kama inavyoonekana kwenye jedwali namba 80 hapa chini:-

**Jedwali 80: Manunuzi ya bidhaa na huduma bila idhini ya Bodi za Zabuni**

| Na | Halmashauri | Kiasi (Sh) |
|---|---|---|
| 1 | Wilaya ya Kasulu | 360,283,250 |
| 2 | Wilaya ya Nzega | 103,171,380 |
| 3 | Wilaya ya Songea | 82,335,750 |
| 4 | Wilaya ya Magu | 77,563,000 |
| 5 | Wilaya ya Musoma | 75,360,000 |
| 6 | Wilaya ya Rombo | 66,783,300 |
| 7 | Wilaya ya Bahi | 52,387,050 |
| 8 | Wilaya ya Manyoni | 35,279,000 |
| 9 | Wilaya ya Longido | 19,986,900 |
| 10 | Wilaya ya Urambo | 16,817,000 |
| 11 | Wilaya ya Kondoa | 5,904,628 |
| 12 | Wilaya ya Arusha | 4,480,000 |
| 13 | Wilaya ya Missenyi | 3,672,000 |
| **Jumla** | | **904,023,258** |

### 6.2.2 Ununuzi wa mali toka kwa wauzaji binafsi bila kibali cha Bodi za Zabuni Sh. 297,695,684

Kanuni Na. 68(5) ya Sheria za Manunuzi ya Umma ya mwaka 2004, inaagiza kwamba kuwepo na orodha ya wauzaji waliopendekezwa na bodi ya zabuni na hatimaye taasisi inayofanya ununuzi iandae maombi kwa njia ya dodoso za ununuzi kwa wauzaji wote waliochaguliwa. Hata hivyo, halmashauri kumi na tisa (19) zilikiuka kanuni hiyo kwa kufanya ununuzi wa mali, kazi za ujenzi na kazi zisizo za ushauri zenye thamani ya Sh.297,695,684 kutoka kwa wauzaji ambao hawakuthibitishwa na Wakala wa Serikali wa Manunuzi ya Umma pamoja na bodi za zabuni za halmashauri kama ilivyoonyeshwa kwenye jedwali Na. 81 hapa chini:

Hata hivyo kiasi cha manunuzi ya mali toka kwa wauzaji binafsi bila kibali cha bodi za zabuni kimeongezeka kutoka mwaka 2011/12 hadi mwaka 2012/13 kwa Sh.176,304,181.

**Jedwali 81: Ununuzi wa mali toka kwa wauzaji binafsi bila kibali cha Bodi za Zabuni**

| Na. | Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|
| 1 | Wilaya ya Sengerema | 55,502,500 |
| 2 | Wilaya ya Bukoba | 39,314,368 |
| 3 | Wilaya ya Musoma | 37,500,000 |
| 4 | Wilaya ya Serengeti | 29,106,991 |
| 5 | Wilaya ya Arusha | 23,272,100 |
| 6 | Wilaya ya Kasulu | 19,704,750 |
| 7 | Wilaya ya Monduli | 17,458,200 |
| 8 | Wilaya ya Kilolo | 12,600,000 |
| 9 | Mji wa Mpanda | 12,540,450 |
| 10 | Wilaya ya Sumbawanga | 9,731,380 |
| 11 | Wilaya ya Kyela | 6,802,000 |
| 12 | Manispaa ya Tabora | 5,900,000 |
| 13 | Wilaya ya Kisarawe | 5,558,000 |
| 14 | Manispaa ya Sumbawanga | 5,032,475 |
| 15 | Wilaya ya Biharamulo | 5,000,000 |
| 16 | Wilaya ya Mkinga | 4,980,000 |
| 17 | Wilaya ya Missenyi | 3,675,000 |
| 18 | Wilaya ya Ngara | 2,798,720 |
| 19 | Wilaya ya Rorya | 1,218,750 |
| **Jumla** | | **297,695,684** |

### 6.2.3 Manunuzi ya vifaa na bidhaa yaliyofanywa bila kushindanisha wazabuni Sh. 267,422,480

Ukaguzi ulibaini vifaa na bidhaa vyenye thamani ya jumla Sh.267,422,480 vilivyonunuliwa na halmashauri kumi na nne (14) ambavyo vilinunuliwa bila bei shindani kinyume na Kanuni Na. 28 ya Sheria ya Manunuzi ya Umma za mwaka 2004 pamoja na Jedwali la Kwanza la Kanuni zinazoongoza taratibu za zabuni katika halmashauri za mwaka 2007 kama inavyoonekana kwenye jedwali Na.82 hapo chini.

**Jedwali 82: Manunuzi ya vifaa na bidhaa yaliyofanywa bila kushindanisha wazabuni**

| Na. | Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|
| 1 | Wilaya ya Nkasi | 104,749,870 |
| 2 | Wilaya ya Kibondo | 33,911,820 |
| 3 | Wilaya ya Lindi | 32,814,000 |
| 4 | Wilaya ya Nzega | 22,243,080 |
| 5 | Wilaya ya Longido | 19,986,900 |
| 6 | Manispaa ya Bukoba | 12,752,000 |
| 7 | Wilaya ya Chato | 10,000,000 |
| 8 | Wilaya ya Monduli | 9,440,810 |
| 9 | Wilaya ya Missenyi | 6,000,000 |
| 10 | Wilaya ya Kyela | 4,890,000 |
| 11 | Wilaya ya Mufindi | 3,750,000 |
| 12 | Wilaya ya Nachingwea | 3,159,000 |
| 13 | Wilaya ya Tabora | 2,495,000 |
| 14 | Wilaya ya Ruangwa | 1,230,000 |
| **Jumla** | | **267,422,480** |

### 6.2.4 Manunuzi ya mali na vifaa bila kuingizwa kwenye daftari Sh. 374,479,679

Matumizi ya vifaa na mali yenye thamani ya Sh.374,479,679 yaliyoagizwa na kulipiwa hayakuweza kuthibitika kutokana na kutoingizwa kwenye daftari la vifaa husika kinyume na Agizo 54(3) la LAFM, 2009. Katika mapitio ya manunuzi ilibainika kuwa halmashauri kumi na tisa (19) hazikuingiza vifaa na mali zilizonunua kwenye daftari la vifaa. Mchanganuo wa halmashauri zilizohusika ni kama inavyoonekana kwenye Jedwali Na. 83 hapa chini:-

**Jedwali 83: Manunuzi ya mali na vifaa bila kuingizwa kwenye daftari**

| Na. | Halmashauri | Kiasi (Sh) |
|---|---|---|
| 1 | Wilaya ya Mpanda | 91,256,200 |
| 2 | Wilaya ya Maswa | 57,981,200 |
| 3 | Manispaa ya Kinondoni | 50,613,560 |
| 4 | Manispaa ya Ilala | 31,069,600 |
| 5 | Wilaya ya Mafia | 25,816,823 |
| 6 | Wilaya ya Urambo | 21,800,000 |
| 7 | Manispaa ya Sumbawanga | 21,320,500 |
| 8 | Wilaya ya Masasi | 15,882,396 |
| 9 | Wilaya ya Ruangwa | 8,848,000 |
| 10 | Wilaya ya Longido | 8,286,000 |
| 11 | Wilaya ya Bukombe | 7,800,000 |
| 12 | Wilaya ya Hanang' | 6,628,750 |
| 13 | Jiji la Tanga | 5,353,500 |
| 14 | Wilaya ya Chato | 4,725,000 |
| 15 | Wilaya ya Musoma | 4,641,000 |
| 16 | Wilaya ya Arusha | 3,758,650 |
| 17 | Wilaya ya Nachingwea | 3,541,000 |
| 18 | Wilaya ya Sumbawanga | 3,200,000 |
| 19 | Wilaya ya Rufiji/Utete | 1,957,500 |
| **Jumla** | | **374,479,679** |

### 6.2.5 Mali na Vifaa Vilivyonunuliwa lakini Havijapokelewa, Sh.527,767,998

Katika kipindi cha mwaka 2012/13, kiasi cha Sh. 527,767,998 kililipwa kwa kutumia fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Afya kabla ya kupokea bidhaa na vifaa kutoka kwa wazabuni na wauzaji mbalimbali. Hata hivyo vifaa na mali havijapokelewa kinyume na Kanuni 122 ya Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka, 2004 inayosisitiza uwepo wa taarifa ya kupokea vifaa kwanza na baadaye malipo kuidhinishwa. Orodha ya halmashauri kumi na nane (18) na thamani ya mali na vifaa ambavyo havijapokelewa ni kama inavyoonekana kwenye Jedwali Na. 84 hapo chini:

Hata hivyo kiasi cha bidhaa na mali ambazo zililipiwa na kutokupokelewa kimepungua kutoka mwaka 2010/11 hadi mwaka 2011/12 kwa Sh.141,737,496 na kuongezeka kwa

Sh.347,064,013 katika kipindi cha mwaka 2011/12 hadi 2012/13.

**Jedwali 84: Mali na Vifaa Vilivyonunuliwa lakini havijapokelewa**

| Na | Halmashauri | Kiasi ( Sh) |
|---|---|---|
| 1 | Wilaya ya Geita | 226,638,600 |
| 2 | Wilaya ya Sengerema | 106,852,100 |
| 3 | Wilaya ya Rorya | 56,532,650 |
| 4 | Wilaya ya Karagwe | 22,996,700 |
| 5 | Wilaya ya Muleba | 18,758,000 |
| 6 | Wilaya ya Misungwi | 15,946,928 |
| 7 | Wilaya ya Bukombe | 14,026,000 |
| 8 | Wilaya ya Mkuranga | 11,900,000 |
| 9 | Wilaya ya Nzega | 11,745,000 |
| 10 | Wilaya ya Bahi | 10,313,200 |
| 11 | Wilaya ya Shinyanga | 9,000,000 |
| 12 | Jiji la Tanga | 8,277,700 |
| 13 | Wilaya ya Tarime | 3,533,500 |
| 14 | Wilaya ya Pangani | 3,521,500 |
| 15 | Manispaa ya Shinyanga | 2,699,600 |
| 16 | Manispaa ya Bukoba | 2,077,800 |
| 17 | Wilaya ya Makete | 1,748,720 |
| 18 | Wilaya ya Longido | 1,200,000 |
| **Jumla** | | **527,767,998** |

### 6.2.6 Manunuzi ya dawa na vifaa tiba bila kibali cha Bohari Kuu ya Dawa Sh.1,025,278,064

Ili kufanya manunuzi yenye tija, vifaa tiba na dawa vinapaswa kununuliwa kutoka Bohari Kuu ya Dawa. Endapo bidhaa husika hazitapatikana Bohari Kuu itatoa kibali cha kununua kutoka kwa wazabuni binafsi. Ukaguzi ulibaini vifaa tiba na dawa zenye thamani ya Sh.1,025,278,064 vilivyonunuliwa na halmashauri thelathini (30) kwa wazabuni binafsi bila kibali kutoka Bohari Kuu ya Dawa kinyume na Kanuni ya 4 ya Kanuni za Bodi ya Zabuni ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa ya mwaka 2007 na Kifungu Na. 51 cha Sheria za Manunuzi ya Umma ya mwaka 2004 kama inavyoonekana kwenye **kiambatisho Na. XIX**

Hata hivyo kiasi cha vifaa tiba na dawa zilizonunuliwa bila idhini ya Bohari Kuu ya Dawa kimeongezeka kwa Sh.118,787,960 kutoka mwaka 2010/11 hadi mwaka 2011/12 na pia kuendelea kuongezeka kutoka mwaka 2011/12 hadi mwaka 2012/13 kwa Sh.613,058,464.

### 6.2.7 Manunuzi ya huduma na bidhaa yaliyofanywa kwa fedha taslim Shs 42,679,688

Halmashauri saba (7) ziliwapa watumishi kiasi cha Sh.42,679,688 ikiwa ni fedha taslim kwa ajili ya kununua vifaa na bidhaa mbalimbali za halmashauri kinyume na Agizo Na. 68 la LAFM, 2009, ambalo linataka uagizaji wa bidhaa na vifaa ufanywe kwanza kwa kutumia njia ya kuagiza kupitia hati ya kuagizia bidhaa na ndipo malipo yafanywe kwa kutumia hundi. Kutokana na kutozingatia Agizo hilo kuna uwezakano, mali na bidhaa zilizonunuliwa kuwa za bei ya juu na zisizokuwa na ubora unaotakiwa. Orodha ya halmashauri imeonyeshwa kwenye Jedwali Na. 85 hapa chini:

**Jedwali 85: Manunuzi ya huduma na vifaa yaliyofanywa kwa fedha taslimu**

| Na. | Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|
| 1 | Wilaya ya Kasulu | 9,696,000 |
| 2 | Wilaya ya Lushoto | 6,895,000 |
| 3 | Wilaya ya Kigoma | 6,480,000 |
| 4 | Wilaya ya Kahama | 6,360,000 |
| 5 | Wilaya ya Ngorongoro | 6,018,000 |
| 6 | Wilaya ya Rombo | 3,015,000 |
| 7 | Wilaya ya Simanjiro | 2,190,688 |
| 8 | Wilaya ya Babati | 2,025,000 |
| **Jumla** | | **42,679,688** |

## 6.3 Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF)

### 6.3.1 Manunuzi yaliyofanywa bila ushindanishi wa bei Sh.22,239,994

Kanuni Na. 68(4) ya Sheria ya Manunuzi ya Umma 2004, inataka orodha ya bei kutoka kwa wazabuni angalau watatu tofauti iweze kulinganishwa na manunuzi yafanyike kutoka kwa muuzaji mwenye bei na bidhaa bora. Kinyume na kanuni

hii manunuzi yafuatayo yamefanyika bila ushindanishi kama ilivyoonyeshwa katika jedwali Na. 86 hapo chini:

**Jedwali 86: Manunuzi yaliyofanywa bila ushindanishi wa bei**

| Na. | Halmashauri | Mzabuni | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|
| 1 | Wilaya ya Liwale | Mistry Garage LTD | 6,572,324 |
| 2 | Wilaya ya Lindi | Agape General Suplier | 828,170 |
| 3 | Manispaa ya Mtwara Mikindani | Alpha Computer | 1,898,000 |
| 4 | Wilaya ya Tandahimba | Intermech Engineering | 11,350,000 |
| 5. | Wilaya yaHandeni | Lyakuvi Investment | 1,591,500 |
| | **Jumla** | | **22,239,994** |

### 6.3.2 Manunuzi ya vifaa ambavyo havikuingizwa kwenye leja Sh.31,187,725

Malipo ya kiasi cha Sh.31,187,725 yamefanyika katika halmashauri nne tofauti ambapo vifaa vilivyonunuliwa havikuingizwa katika daftari la kumbukumbu la manunuzi (leja). Halmashauri hizo ni kama ilivyoonyeshwa katika Jedwali Na. 87 hapa chini:

**Jedwali 87: Vifaa ambavyo havikuingizwa kwenye leja**

| Namba | Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|
| 1 | Wilaya ya Handeni | 2,000,000 |
| 2 | Wilaya ya Lindi | 1,046,500 |
| 3 | Wilaya ya Ruangwa | 26,100,225 |
| 4 | Wilaya ya Masasi | 2,041,000 |
| | **Jumla** | **31,187,725** |

## 6.4 Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji

### 6.4.1 Miradi ambayo haikukamilika Sh.50,553,789,814

Wakati wa ukaguzi, miradi ya kiasi cha Sh.50,553,789,814.66 ilikuwa haijatekelezwa au kukamilishwa. Miradi hiyo inahusisha Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii na halmashauri sabini na tisa (79) mpaka kufikia mwishoni mwa mwaka wa fedha 2012/13 kama ilivyoonyeshwa kwenye kiambatisho Na. XX:

### 6.4.2 Vifaa vya thamani ya Sh. 56,567,949 havijaingizwa kwenye vitabu

Vifaa vya thamani ya Sh.56,567,949 vilivyonunuliwa na halmashauri kumi na tisa (19) viligundulika kutoingizwa kwenye vitabu vya halmashauri husika. Maelezo zaidi yamo kwenye Jedwali Na.88 hapa chini:

**Jedwali 88: Vifaa ambavyo havijaingizwa kwenye vitabu**

| Na. | Halmashauri | Kiasi (Sh) | Na. | Halmashauri | Kiasi (Sh) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Wilaya ya Kilwa | 5,384,000 | 11 | Wilaya ya Musoma | 3,192,600 |
| 2 | Wilaya ya Lindi | 2,508,100 | 12 | Wilaya ya Serengeti | 3,930,000 |
| 3 | Manispaa ya Lindi | 5,413,591 | 13 | Wilaya ya Sengerema | 1,280,000 |
| 4 | Wilaya ya Nachingwea | 2,795,900 | 14 | Wilaya ya Babati | 2,785,800 |
| 5 | Wilaya ya Ruangwa | 4,076,790 | 15 | Mji wa Babati | 2,013,250 |
| 6 | Wilaya ya Mtwara | 2,900,016 | 16 | Wilaya ya Hanang’ | 3,276,423 |
| 7 | Wilaya ya Mtwara | 2,277,000 | 17 | Wilaya ya Same | 1,521,750 |
| 8 | Wilaya ya Kibaha | 1,625,629 | 18 | Wilaya ya Simanjiro | 883,140 |
| 9 | Wilaya ya Rufiji | 7,815,360 | 19 | Wilaya ya Songea | 2,262,000 |
| 10 | Wilaya ya Biharamulo | 626,600 | **JUMLA** | | **56,567,949** |

Hata hivyo, vifaa ambavyo havijaingizwa kwenye vitabu vimeongezeka kwa Sh.27,972,900 ukilinganisha na mwaka wa fedha 2011/12.

### 6.4.3 Vifaa vilivyonunuliwa bila bei shindani Sh.29,873,400

Ukaguzi ulibaini vifaa vyenye thamani ya jumla ya Sh.29,873,400 vilivyonunuliwa na Halmashauri ya Wilaya ya Kibondo bila bei shindani kinyume na Kanuni Na. 28 ya Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2004 pamoja na Jedwali la Kwanza la Kanuni zinazoongoza taratibu za Tenda katika Halmashauri za mwaka 2007.

Hata hivyo thamani ya manunuzi ya vifaa vilivyonunuliwa bila bei shindani imeongezeka kwa Sh.19,947,501 ukilinganisha na mwaka 2011/12.

### 6.4.4 Manunuzi kutoka kwa wauzaji wasioidhinishwa, Sh.33,347,622

Ukaguzi ulibaini vifaa vyenye thamani ya jumla ya Sh.33,347,622 vilivyonunuliwa na halmashauri tatu (3) kutoka kwa wasambazaji ambao hawakuidhinishwa na tenda bodi za halmmashauri husika kwa ajili ya usambazaji wa vifaa kwa mwaka wa fedha 2012/13 kinyume na Kanuni Na.40 ya Sheria ya Manunuzi wa Umma ya Mwaka 2004. Maelezo zaidi yameonyeshwa kwenye Jedwali namba 89 hapa chini:

**Jedwali 89: Manunuzi kutoka kwa wasambazaji wasioidhinishwa**

| Na. | Halmashauri | Kiasi (Sh) |
|---|---|---|
| 1 | Wilaya ya Lindi | 3,300,000 |
| 2 | Wilaya ya Ruangwa | 14,894,622 |
| 3 | Wilaya ya Chato | 2,714,000 |
| 4 | Wilaya ya Rorya | 6,490,000 |
| 5 | Wilaya ya Hanang’ | 3,305,000 |
| 6 | Wilaya ya Ileje | 2,644,000 |
| | **Jumla** | **33,347,622** |

Hata hivyo, manunuzi ya bidhaa kutoka kwa wasambazaji wasioidhinishwa yameongezeka kwa Sh.8,047,585 kutoka mwaka 2011/12 hadi 2012/13.

### 6.4.5 Manunuzi yasiyokuwepo kwenye mpango wa manunuzi wa mwaka Sh.1,093,736,378

Ukaguzi ulibaini kuwa halmashauri mbili (2) zilifanya manunuzi ambayo hayakuwepo kwenye mpango wa manunuzi wa mwaka yenye thamani ya Sh.1,093,736,378. Hii ni kinyume na Kifungu Na. 45 cha Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2004 na hadidu za rejea za kutekeleza mradi wa maji kati ya serikali na wadau wa maendeleo kama ilivyooneshwa kwenye jedwali Na.90 hapo chini:

**Jedwali 90: Manunuzi yasiyokuwepo kwenye mpango wa manunuzi wa mwaka**

| Na. | Halmashauri | Kiasi (Sh) |
|---|---|---|
| 1 | Wilaya ya Tabora | 802,236,378 |
| 2 | Wilaya ya Muheza | 291,500,000 |
| **Jumla** | | **1,093,736,378** |

### 6.4.6 Zabuni zilizotolewa bila kutangazwa Sh.163,550,159

Ukaguzi ulibaini kuwa, kinyume na Kanuni ya 80(3) na 80(5) ya Sheria ya Manunuzi ya Umma, 2004, halmashauri mbili (2) zilitoa zabuni za kiasi cha Sh.163,550,159 bila kutangaza kama inavyoonekana kwenye Jedwali Na.91 hapo chini:

**Jedwali 91: Zabuni zilizotolewa bila kutangazwa**

| Na. | Halmashauri | Kiasi (Sh) |
|---|---|---|
| 1 | Wilaya ya Nanyumbu | 67,549,359 |
| 2 | Wilaya ya Mkuranga | 96,000,800 |
| **Jumla** | | **163,550,159** |

### 6.4.7 Miradi kamilifu isiyokuwa na tija Sh.2,082,757,820

Ukaguzi ulibaini kuwa halmashauri kumi na tatu (13) zililipa kiasi cha Sh. 2,082,757,820 kwa wakandarasi mbalimbali kwa ajili ya miradi ya maji.

Hata hivyo wakati wa kuhakiki miradi iliyotekelezwa, iligundulika kuwa miradi hiyo haikuweza kutoa maji kwa jamii lengwa. Matumizi haya hayakuleta manufaa na ni hasara kwa umma. Taarifa zaidi zinaonekana kwenye jedwali Na.92 hapa chini:

**Jedwali 92: Miradi kamilifu isiyokuwa na tija**

| Na. | Halmashauri | Kiasi (Sh) | Na. | Halmashauri | Kiasi (Sh) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Wilaya ya Tabora | 93,635,600 | 8 | Wilaya ya Karagwe | 77,301,500 |
| 2 | Wilaya ya Kondoa | 19,082,000 | 9 | Wilaya ya Bunda | 495,145,715 |
| 3 | Wilaya ya Urambo | 89,147,050 | 10 | Wilaya ya Handeni | 7,076,796 |
| 4 | Wilaya ya Kilwa | 53,758,816 | 11 | Mji wa Korogwe | 170,952,082 |
| 5 | Wilaya ya Kilombero | 322,497,186 | 12 | Wilaya ya Rombo | 9,650,000 |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 6 | Wilaya ya Bagamoyo | 193,798,765 | 13 | Wilaya ya Mpanda | 26,000,000 |
| 7 | Wilaya ya Bukoba | 524,712,310 | **Jumla** | | **2,082,757,820** |

### 6.4.8 Mikataba iliyotolewa bila kibali cha Bodi za Zabuni Sh.1,256,270,949

Ukaguzi wa mikataba na viambatanisho vyake ulibaini kuwa halmashauri saba (7) zilitoa mikataba kwa wakandarasi yenye jumla ya Sh.1,256,270,949 bila kibali cha bodi za zabuni. Hii ni kinyume na Kanuni ya 41(1) ya Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2004. Taarifa zaidi zimo kwenye jedwali Na.93 hapa chini:

**Jedwali 93: Mikataba iliyotolewa bila kibali cha Bodi za Zabuni**

| Na. | Halmashauri | Kiasi (Sh) |
|---|---|---|
| 1 | Wilaya ya Chamwino | 338,676,323 |
| 2 | Wilaya ya Iramba | 51,500,000 |
| 3 | Wilaya ya Kilwa | 467,743,056 |
| 4 | Wilaya ya Magu | 319,113,820 |
| 5 | Wilaya ya Karatu | 41,187,750 |
| 6 | Wilaya ya Mbulu | 25,500,000 |
| 7 | Wilaya ya Songea | 12,550,000 |
| **Jumla** | | **1,256,270,949** |

### 6.4.9 Kompyuta zilizonunuliwa na kupokelewa bila kufanyiwa tathmini ya ubora Sh. 72,452,802

Kanuni Na.126 na 127 ya GN Na.97 ya mwaka 2005 inamtaka Afisa Masuuli kuunda kamati ya kuchunguza na kutoa taarifa juu ya ubora wa bidhaa zilizopokelewa.

Mapitio ya malipo mbalimbali yaliyofanywa kwa ajili ya kutekeleza shughuli za mradi wa maji chini ya Wizara ya Maji yalibaini kuwa, kiasi cha Sh. 72,452,802 kililipwa kwa ajili ya manunuzi ya iPads na kompyuta mpakato kwa matumizi ya ofisi.

Hata hivyo, hakukuwa na taarifa wala hati ya ushahidi kuwa bidhaa zilizopokelewa na wizara zilikuwa na ubora.

## 6.5 Miradi Mingine

Yafuatayo ni mapungufu yaliyojitokeza katika manunuzi yaliyoyofanywa kwenye miradi mingine:

### 6.5.1 Manunuzi ya vifaa yasiyoingizwa kwenye vitabu (Leja) Sh.10,399,662,211

Kiasi cha Sh.10,399,662,211 hakijaingizwa katika daftari la kumbukumbu la vifaa hivyo kusababisha kukosekana kwa mtiririko mzuri katika uwekaji wa kumbukumbu. Miradi 6 (sita) ilinunua vifaa ambavyo havijaingizwa katika daftari la kumbukumbu kama ilivyoonyeshwa katika jedwali Na.94 hapa chini:

**Jedwali 94:Vifaa visivyo ingizwa kwenye leja**

| Na. | Jina la Mradi | Kiasi (Shs) |
|---|---|---|
| 1 | Ongezeko la Usalama wa Chakula | 10,295,426,000 |
| 2 | SIDA/NORAD/MEM - Mradi wa Nishati ya Mimea | 14,067,400 |
| 3 | Usimamizi wa Mazingira wa Ziwa Victoria (LVEMP II) | 14,773,125 |
| 4 | Shirika la Afya Duniani -Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii | 7,000,000 |
| 5 | Kuimarisha na Kukinga Mtandao wa Maeneo Kusini mwa Tanzania- UNDP | 26,393,686 |
| 6 | Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Afya- Mwanza - Global Fund Mzunguko wa Tisa (9) | 42,002,000 |
| **Jumla** | | **10,399,662,211** |

Hata hivyo, kuna ongezeko kubwa la vifaa visivyoingizwa kwenye leja kwa mwaka 2012/13 ukilinganisha na Sh.164,716,608 kwa mwaka 2011/12 na Sh.4,051,263,000 kwa 2010/11.

### 6.5.2 Manunuzi yaliyofanywa bila kushindanisha wazabuni Sh.69,205,000

Uongozi wa Mradi wa Kusimamia Mazingira ya Baharini na Ukanda wa Pwani (MACEMP - GEF)" walifanywa manunuzi ya Sh.69,205,000 bila kushindanisha wazabuni kinyume na Kifungu (a) cha Jedwali la Kwanza la Kanuni za Manunuzi ya Umma la mwaka 2005. Hata hivyo, manunuzi yaliyofanywa bila kushindanisha wazabuni yamepungua ukilinganisha na Sh.2,049,143,383 kwa mwaka 2011/12.

### 6.5.3 Tozo ya riba kwa kuchelewa kulipa madai Sh.766,119,372.44 na Dola za Marekani 182,742

Kiasi cha Sh.766,119,372.44 na Dola za Marekani 182,742 kililipwa kama tozo ya riba kwa sababu ya kucheleweshwa malipo ya hati za madai kwa wakandarasi kama ilivyoonyeshwa kwenye jedwali Na.95 hapa chini.

**Jedwali 95: Tozo ya riba kwa kuchelewesha malipo ya wakandarasi**

| Na. | Aina ya Mradi | Kiasi(Sh) | Kiasi (Dola za Marekani) |
|---|---|---|---|
| 1 | Kusaidia Sekta ya Barabara (RSSP) | 85,785,249.44 | |
| 2 | DANIDA wa Kusaidia Sekta ya Barabara | 680,334,123 | 182,742 |
| **Jumla** | | **766,119,372.44** | **182,742** |

Kucheleweshwa kwa malipo ya wakandarasi kumesababisha kuongezeka kwa tozo ya riba kutoka Sh.19,053,525.36 kwa mwaka uliopita na kufikia Sh.766,119,372.44 na Dola za Marekani 182,742 kwa mwaka 2012/13. Serikali inashauriwa kupeleka kiasi cha fedha kinachotosheleza na kwa wakati.

# SURA YA SABA

# KAGUZI MAALUM

## 7.0 Utangulizi

Kifungu cha 29 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma ya mwaka 2008 na Kanuni Na.79(1) ya Kanuni za Ukaguzi wa Umma ya mwaka 2009 kinampa mamlaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kufanya ukaguzi maalum kutokana na maombi kutoka kwa Afisa Masuuli au mtu yeyote, Taasisi, Mamlaka ya Umma, Wizara, Idara, Wakala, Mamlaka ya Serikali za Mitaa na vyombo vingine. Kanuni pia inampa CAG mamlaka ya kufanya ukaguzi maalum pale anapoona inafaa. Katika mwaka 2012/13, kaguzi maalum mbili (2) za miradi zilifanyika. Muhtasari wa masuala yaliyojitokeza katika kaguzi hizi ni kama ifuatavyo:

## 7.1 Ukaguzi maalum wa Mfuko wa Maendeleo ya Afya (HBF)

Ukaguzi maalum wa Mfuko wa Maendeleo ya Afya ilijumuisha halmashauri kumi na nne ambazo zilichaguliwa kutokana na taarifa za utendaji za mpango kabambe wa afya za mwaka 2011/12. Kati ya halmashauri 14, halmashauri 4 zilichaguliwa kutoka katika halmashauri zilizofanya vizuri, halmashauri 6 kutoka katika halmashauri ambazo hazikufanya vizuri na halmashauri 4 zilichaguliwa na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii.

Matokeo ya ukaguzi maalum wa Mfuko wa Maendeleo ya Afya yamegawanywa katika maeneo manne kama inavyoonekana hapa chini:

1. Mipango ya ugawaji na usambazaji wa fedha za ruzuku za Mfuko wa Afya.
2. Mipango ya usimamizi wa matumizi ya rasilimali za Mfuko wa Maendeleo ya Afya kwa halmashauri ambazo zilichaguliwa.
3. Thamani ya fedha na ufuatiliaji wa fedha zilizotumika.
4. Utoaji wa taarifa za matumizi ya fedha za ruzuku katika ngazi ya mkoa na taifa kwa ujumla.

Makundi matatu ya halmashauri yaliyochaguliwa kulingana na taarifa ya utendaji wa mpango kabambe wa afya ni kama ilivyoonyeshwa hapo chini:

**Kundi Na.1-Kutoka halmashauri zilizofanya vizuri**
1. Wilaya ya Kiteto
2. Wilaya ya Mtwara
3. Wilaya ya Mvomero
4. Wilaya ya Masasi

**Kundi Na.2-Kutoka halmashauri ambazo hazikufanya vizuri**
1. Manispaa ya Lindi
2. Wilaya ya Mbarali
3. Manispaa ya Sumbawanga
4. Wilaya ya Muleba
5. Mji wa Kibaha
6. Mji wa Mpanda

**Kundi Na.3-Halmashauri zilizochaguliwa na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii**
1. Wilaya ya Chamwino
2. Wilaya ya Iramba
3. Wilaya ya Pangani
4. Wilaya ya Iringa

**Matokeo ya Ukaguzi**

(a) Ukaguzi maalum uligundua mambo yafuatayo katika kugawa, kupanga na kusambaza fedha za ruzuku za Mfuko wa Afya:

**(i) Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii ilitumia kanuni moja elekezi katika kugawa fedha kwenye halmashauri**

Kanuni elekezi katika kukokotoa mgawanyo wa fedha zinazokwenda halmashauri haikufanyiwa mapitio ambayo yanahusiana na mabadiliko ya idadi ya watu, vifo chini ya miaka mitano (5), takwimu za umasikini na mwelekeo wa masuala ya afya katika wilaya.

(ii) **Kumekuwa na ucheleweshwaji wa kukidhi matakwa na vipengele muhimu vilivyoanishwa kwenye makubaliano yaliyofikiwa kati ya washirika wa maendeleo na Serikali na hivyo kupelekea ucheleweshwaji wa fedha**
Mapitio ya muhtasari yanaonyesha kuwa makubaliano baina ya pande mbili yalichelewa kuidhinishwa, kwani kwa mwaka 2010/11 yaliidhinishwa mwezi wa tisa na kwa mwaka 2011/12 yaliidhinishwa mwezi wa nane, kutokana na kucheleweesha kuwasilisha nyaraka muhimu na hii ilipelekea ucheleweshwaji wa fedha.

(iii) **Kumekuwa na ucheleweshwaji wa fedha zinazopelekwa kwenye Halmashauri**
Taarifa hii inaonyesha kuwa fedha zilizopelekwa kwa ajili ya robo ya kwanza na ya pili zilipokelewa mwishoni mwa robo ya pili ya mwaka kwa kipindi cha miaka miwili ambayo ilikaguliwa. Pia kulikuwa na ucheleweshwaji wa kuhamisha fedha kutoka akaunti maalum katika Benki Kuu ya Tanzania (Holding Account) kwenda kwenye halmashauri kupitia akaunti ya Hazina. Ucheleweshwaji huu ulikuwa ni wa kati ya siku nne hadi arobaini na nne (4-44).

(iv) **Washirika wa miradi ya maendeleo hawakutekeleza ahadi zao kulingana na makubaliano yaliyoafikiwa baina ya pande mbili kwa kipindi cha mwaka 2010/2011**
Kulingana na makubaliano yaliyoafikiwa baina ya pande zote mbili, Benki ya Dunia iliahidi kutoa kiasi cha dola za Marekani milioni ishirini na mbili, lakini makao makuu ya benki hiyo yaliidhinisha na kutuma kiasi cha Dola za Marekani milioni kumi tu. Kiasi ambacho hakikutolewa na benki hiyo kiliathiri mipango na utekelezaji wa shughuli zilizoanishwa kwenye bajeti ya mwaka huo.

(v) **Mapitio ya taarifa za robo mwaka zinaonyesha kuwa Ofisi za Katibu Tawala Mikoa hazipeleki kwa wakati taarifa za robo mwaka TAMISEMI**
Ofisi za Katibu Tawala Mikoa hazipeleki TAMISEMI taarifa za robo mwaka za halmashauri kwa wakati kinyume na Aya 4.2 ya mwongozo wa Mpango Kabambe wa Afya wa mwaka, 2011.

(vi) **Ripoti hii ya ukagazi maalum inaelezea ucheleweshwaji katika kutekeleza shughuli za mpango kabambe wa afya**
Halmashauri zilichelewa kutekeleza shughuli mbalimbali kutokana na ucheleweshwaji wa fedha. Ukaguzi ulibaini ucheleweshwaji wa kuhamisha fedha kutoka akaunti za halmashauri kwenda sehemu mbalimbali zinazotekeleza shughuli za afya.

(vii) **Ilibanika kuwa kiasi cha fedha cha Mfuko wa Maendeleo ya Afya ambacho hakikutumika kwa mwaka husika hakiendani na makadirio ya gharama za utekelezaji wa shughuli zilizobaki**
Makadirio ya gharama za utekelezaji wa shughuli ambazo hazikufanyika kama ilivyopangwa yalionekana kuwa juu zaidi ya kiasi cha fedha kilichobaki. Haya yalibanika katika ukaguzi maalum wa mwaka 2010/11 na 2011/12.

(viii) **Shughuli ambazo hazikufanyika kwa mwaka husika katika baadhi ya Halmashauri na kutokutekelezwa mwaka unaufuata**
Ilibainika kuwa shughuli zisizotekelezwa katika mwaka husika na hivyo kupaswa kutekelezwa mwaka unaofuata ambazo ni asilimia 40 kwa mwaka 2010/11 na asilimia 45 kwa mwaka 2011/12 hazikutekelezwa katika miaka iliyofuata. Udhaifu huu ulionekana katika halmashauri nane kati ya 14 zilizofanyiwa uchunguzi.

(ix) **Ucheleweshwaji wa kupeleka fedha katika akaunti za afya**
Kumekuwa na ucheleweshaji wa kupeleka fedha kutoka katika akaunti ya maendeleo kwenda katika akaunti za afya za halmashauri. Ilibainika kwa wastani inachukua siku kumi na tisa katika zoezi zima la uhamishaji wa fedha.

**(b) Mipango, usimamizi na matumizi ya rasilimali za Mfuko wa Maendeleo ya Afya katika Halmashauri zilizochaguliwa**

i) **Ugumu katika utumiaji wa rasilimali za afya zisizopitia kwenye Mfuko wa Maendeleo ya Afya**

ruzuku zinazotolewa na baadhi ya wahisani ambao hawachangii moja kwa moja kwenye Mfuko wa Sekta ya Afya kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli maalum zilizopangwa ambazo wakati mwingine haziendani na vipaumbele vya halmashauri hivyo kuleta ugumu katika utekelezaji.

ii) **Ilionekana kuwa baadhi ya watumishi wanaohusika na masuala ya mipango katika Halmashauri hawakupata mafunzo ya kutosha katika mchakato mzima wa kuandaa bajeti**

Hii ilibanika wakati wa mahojiano na watumishi wanohusika na masuala ya mipango. Pia baadhi ya Mamlaka za serikali za mitaa hazikuwa na Mwongozo wa Mpango Kabambe wa Afya wa Novemba 2011.

iii) **Kwa ujumla mchakato wa uandaaji wa Mpango Kabambe wa Afya haukuwa shirikishi**

Ukaguzi ulibaini kuwa wadau wanaosimamia maswala ya afya katika ngazi za chini hawakushirikishwa kikamilifu katika mchakato wa maandalizi ya mwisho ya Mpango Kabambe wa Afya. Ushirikishwaji wa wadau uliishia katika hatua za mwanzo za maandalizi. Kadhalika ilibainika halmashauri kwa kiasi fulani hazikufuata mwongozo wa mpango wa afya katika maandalizi.

**(c) Thamani ya Fedha kwa kazi zilizofanyika kwenye Halmashauri zilizochaguliwa**

Tathmini ya thamani ya fedha kwa kazi zilizofanyika katika halmashauri zilizoteuliwa kukaguliwa ilionyesha kuwa asilimia 31 ya fedha zote za halmashauri katika sekta ya afya hutoka katika mfuko wa maendeleo ya afya isipokuwa ruzuku ya mishahara. Hivyo, inaonekana halmashauri hazina uwezo wa kuendelea kutoa huduma bila kutegemea fedha za mfuko wa maendeleo ya afya. Halmashauri zilikiri kuwa tatizo la kutopata mgao wa fedha kulingana na shughuli za afya zilizopangwa kutekelezwa, kunasababisha kukwamisha utekelezaji wa shughuli muhimu za utoaji huduma za afya. Upungufu huo wa fedha unaathiri shughuli za kila siku za kamati za usimamizi wa shughuli za afya na mambo mengine

yasiyohusiana na ulipaji wa mishahara yanayotekelezwa katika ngazi za chini za halmashauri.

Manunuzi ya vifaa tiba kwa kutumia fedha za mfuko wa maendeleo ya Afya hayakufuata taratibu za sheria ya manunuzi. Ilibainika baadhi ya manunuzi yaliyofanywa yalikuwa chini ya kiwango na ubora uliotarajiwa.

**Ukaguzi maalum unaohusiana na fedha za ruzuku za mfuko wa maendeleo ya afya katika kipindi cha mwaka wa fedha 2010/2011 na 2011/2012.**

- Mapitio ya taarifa za mkaguzi wa ndani katika baadhi ya halmashauri zimeonyesha matumizi yasiyo sahihi katika utumiaji wa rasilimali za mfuko wa afya. Kadhalika, tathmini ya mpango wa ukaguzi wa ndani ulibaini kuwa baadhi ya shughuli zilizotekelezwa za mfuko wa afya hazikuwekwa kwenye mpango wa ukaguzi na hazikukaguliwa.

- Mamlaka za serikali za mitaa haziandai vifungu vya matumizi vinavyojitegemea kwa kila programu ya mradi. Hii inasababisha ugumu katika kutofautisha fedha za kila mradi zinazoletwa na wahisani. Hata hivyo tatizo hili linaweza kutatuliwa kwa kutumia mfumo mpya wa maandalizi ya taarifa za fedha 'Epicor 9.5'

**(d) Ufuatiliaji na utoaji taarifa katika matumizi ya fedha za mfuko wa afya wa wilaya kwa ngazi ya kimkoa na kitaifa**

1. **Ilibainika kuwa kamati za utoaji huduma za afya hazikutekeleza majukumu yake ipasavyo kama ilivyoelekezwa katika mwongozo wa mpango wa kabambe wa afya**.

    - Mapitio yalibaini kuwa kamati hizi hazitekelezi majukumu yake ipasavyo.

    - Malengo ya kutumia mfumo wa tekinologia ya komputa hususani 'Epicor' hayakufanikiwa ipasavyo. Ukaguzi uligundua kuwa mfumo huu

hautumiwi kikamilifu katika maandalizi ya taarifa za hesabu kwani taarifa hizo zinaandaliwa nje ya mfumo. Mfano maandalizi ya mpango kabambe wa afya wa kila robo mwaka na ya mwaka mzima yalifanywa nje ya mfumo kwa miaka iliyokaguliwa. Pia mfumo wa maandalizi ya bajeti ambao ni nyenzo muhimu katika mamlaka ya serikali za mitaa, haukuunganishwa na mfumo wa maandalizi ya hesabu 'Epicor' na watumishi wa halmashauri hawapati mafunzo ya kutosha katika utumiaji wa mifumo hiyo.

2. **Jukumu la usimamizi wa Kamati za Afya za mikoa na TAMISEMI usioridhisha**

   TAMISEMI haikusimamia utekelezaji wa Mipango ya Afya katika ofisi za makatibu tawala wa wilaya na mamlaka za serikali za mitaa ili kutathmini utekelezaji wa mpango kabambe wa afya (CCHP) na mapendekezo yaliyotolewa katika ukaguzi wa mfuko wa afya. Vikao vya mwisho wa mwaka havikufanyika ambavyo vilipaswa kuwahusisha wakuu wa vitengo vya afya wa mikoa na wilaya ili kupanga mikakati madhubuti ya utekelezaji na kutoa dira katika mchakato wa kuboresha sekta ya afya.

## 7.2 Masuala yaliyojitokeza katika ukaguzi maalum wa miradi inayofadhiliwa na Shirika la Maendeleo la Denmark "PFM" na "SWMP"

### 7.2.1 Mradi Shirikishi wa Usimamizi wa Misitu

Muhtasari wa matokeo ya ukaguzi maalumu uliofanywa kwenye Mradi Shirikishi wa Usimamizi wa Misitu katika halmashauri kumi na moja (11), Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania na Wizara ya Maliasili na Utalii kitengo cha Misitu na Nyuki ni kama ilivyoonyeshwa hapa chini:

- **Manunuzi yaliyofanywa bila kushindanisha wazabuni Sh. 13,355,534**

  Ukaguzi ulibaini vifaa na mali vya kiasi cha Sh.13,355,534, vilivyonunuliwa na Halmashauri ya

Wilaya ya Kilosa Sh. 1,500,000 na Ofisi ya Katibu Tawala wa Mkoa wa Iringa Sh.11,855,534 kutoka kwa wazabuni mbalimbali bila ya kuwashindanisha kinyume na Kanuni Na.68 (4) ya Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2004 pamoja na Jedwali la kwanza la kanuni zinazoongoza taratibu za zabuni katika Serikaki za Mitaa za mwaka 2007.

- Kinyume na kanuni Na.68 (4) ya Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2004, halmashauri mbili zilinunua bidhaa, vifaa vya ujenzi na kupata huduma zisizokuwa za kiushauri zenye thamani ya Sh. 19,242,500 (Halmashauri ya Ileje Sh. 10,772,500 na Halmashauri ya Wilaya ya Iringa Sh.8,470,000) kutoka kwa wazabuni ambao hawakuidhinishwa na Bodi ya Zabuni pamoja na Wakala wa Serikali wa Manunuzi ya Umma.

- **Kukosekana kwa nyaraka za fedha zilizohamisha Sh.36,454,000**
  Katika kipindi cha mwaka 2012/13, kiasi cha Sh.36,454,000 kilihamishwa kutoka akaunti ya maendeleo ya Wilaya ya Chunya kwenda akaunti Na.6076600076 ya Mapogoro. Uongozi unaoshughulikia utekelezaji wa mradi haukuwasilisha nyaraka za fedha zilizohamishwa kinyume na kifungu Na. 5.7 cha Mwongozo wa Fedha na Utawala wa Mradi na Kanuni Na.138 ya Sheria ya Fedha za Umma ya mwaka 2001.

- **Fedha zilizotumiwa kwa kazi zisizohusiana na Mradi Sh.48,070,000**
  Kiasi cha Sh. 48,070,000 kilitumiwa na halmashauri mbili (Mbarali Sh.26,907,000 na Mbozi Sh.19,925,000) na Ofisi ya Katibu Tawala Mkoa wa Iringa Sh,1,238,000 kwa ajili ya kutekeleza shughuli zisizohusiana na mradi. Hivyo baadhi ya shughuli zilizopangwa kutekelezwa kwa mwaka husika hazikufanyika kama ilivyokusudiwa.

- **Kutoandaliwa kwa taarifa za usuluhishi wa kibenki**
  Taarifa za usuluhishi wa kibenki kwa mwezi Juni 2013 hazikuandaliwa na hivyo hazikuwasilishwa kwa ajili ya ukaguzi kinyume na Kanuni Na.162(1) ya Sheria ya Fedha za Umma ya 2001. Kutoandaliwa kwa taarifa za usuluhishi wa kibenki kunaweza kupelekea kutobainika kwa makosa na uwezekano wa kuwepo ubadhirifu wa fedha.

- **Malipo yenye nyaraka pungufu na masurufu yasiyorejeshwa Sh. 6,100,000**
  Malipo yaliyofanywa na Halmashauri ya Iringa ya kiasi cha Sh. 6,100,000 yalikuwa na nyaraka pungufu kinyume na Agizo Na. 8(2c) la Memoranda ya Fedha za Serikali za Mitaa ya mwaka 2009.

### 7.2.2 Programu ya Usimamizi endelevu wa Eneo Oevu (SWMP)

Muhtasari wa matokeo ya ukaguzi maalum uliofanywa katika halmashauri za wilaya tisa (9), Ofisi ya katibu Tawala Mkoa wa Iringa na TAMISEMI kwa mwaka wa fedha 2012/13 ni kama ilivyoonyeshwa hapa chini:

- **Malipo yenye nyaraka pungufu Sh.23,929,950**
  Malipo ya Sh.23,929,950 yaliyolipwa na halmashauri tano (5) (Mbarali Sh.10,924,500, Ngorongoro Sh.7,005,600, Ludewa Sh.2,659,850, Mbeya Sh.2,610,000 na Mufindi Sh.730,000) hayakuwa na nyaraka za kutosha kinyume na Kanuni Na.138 ya Sheria ya Fedha za Umma ya mwaka 2001

- **Matumizi yaliyofanywa pasipo kuwa na vifungu**
  Taarifa za matumizi katika Halmashauri ya Wilaya ya Iringa na Ofisi ya Katibu Tawala – Iringa hayakuwa na vifungu vinavyoonyesha kiasi na aina ya shughuli iliyopaswa kutekelezwa kwa mujibu wa bajeti katika mradi wa Usimamizi Endelevu wa Eneo Oevu. Hivyo haikuwa rahisi kujua aina ipi ya kifungu cha bajeti kilichopaswa kutumika kugharamia shughuli husika bila ya kupitia hati zote za malipo.

- **Matumizi yaliyofanywa nje ya bajeti iliyoidhinishwa Sh. 15,301,600**
  Bajeti ni nyenzo muhimu katika udhibiti na usimamizi wa matumizi, hivyo menejimenti inatakiwa kuhakikisha matumizi yote yanalipwa kulingana na bajeti iliyoidhinishwa, na endapo kutakuwa na malipo yatakayotokana na vifungu visivyohusika idhini lazima itolewe na mamlaka husika. Halmashauri tano zilitumia kiasi cha Sh. 15,301,600 (Iringa Sh. 720,000, Mbozi Sh.1,850,000, Katibu Tawala Mkoa wa Iringa Sh.1,500,000, Ludewa Sh.1,987,500 na Mbarali Sh.9,244,100) ambacho kilikuwa ni zaidi ya kiasi kilichoidhinishwa kwenye bajeti ya mradi kinyume na Agizo 23(1) la LAFM, 2009. Utumiaji wa fedha zaidi ya kiasi kilichoidhinishwa inaashiria udhaifu katika usimamizi wa matumizi ya fedha za mradi kulingana na bajeti.

# SURA YA NANE

# HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 8.0 Utangulizi

Matokeo ya ukaguzi yaliyomo kwa undani kwenye barua na ripoti za ukaguzi ambazo maswala yake yameelezwa kwa ufupi katika ripoti hii, yaliwasilishwa kwa maafisa masuuli kwa utekelezaji. Maafisa masuuli ambao ni wahusika katika utekelezaji wa miradi inayofadhiliwa na washirika wa maendeleleo wanawajibika kuandaa majibu yaliyo na mtiririko ulioandaliwa vyema wa maswala yaliyohojiwa pamoja na mapendekezo yaliyomo kwenye ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na kuwasilisha kwa Mlipaji Mkuu wa Serkali. Katika ripoti hii nimeainisha mapungufu kadhaa ya mfumo wa udhibiti wa ndani kwa mujibu wa Kanuni ya 28-35 ya Sheria ya Fedha za Umma ya mwaka 2001(iliyorekebishwa 2004). Maswala haya yanahitaji kushughulikiwa haraka na maafisa masuuli kwa kuwepo mfumo imara wa udhibiti wa ndani ambao utashughulikia mapungufu yaliyoainishwa katika ripoti hii kwa mujibu wa Kifungu Na. 11 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma ya mwaka 2008.

Nimetoa mapendekezo kadhaa ambayo iwapo yatatekelezwa yataimarisha usimamizi bora wa fedha zinazotolewa na Washirika wa maendeleo kwa Serikali.

## 8.1 Hitimisho la Jumla

- Ukaguzi wa ndani katika Wizara na Mamlaka za Serikali za Mitaa hauridhishi kutokana na kutokaguliwa maeneo muhimu kama ukaguzi wa taarifa za fedha na shughuli za miradi inayofadhiliwa na wahisani wa maendeleo katika eneo muhimu la uwajibikaji na tathmini ya utendaji wa miradi kwa mujibu wa mkataba wa maelewano (MoU).

- Kutokana na ukweli kwamba utekelezaji wa miradi inayofadhiliwa na washirika wa maendeleo hufanywa na watendaji wa ngazi za chini katika vijiji, maafisa masuuli katika Mamlaka za Serikali za Mitaa hawapati muda wa

kutosha wa kusimamia miradi inayofadhiliwa na washirika wa maendeleo.

- Maafisa masuuli hawatoi umuhimu wa kutosha wa kushughulikia mapendekezo na maswala yaliyohojiwa na wakaguzi. Hii inatokana na ushahidi kwamba, palikuwepo na mapendekezo yasiyojibiwa ya kipindi kilichopita ya Sh.129,329,551,647 kwa mwaka 2012/13, ukilinganisha na Sh. 20,289,040,011 kwa mwaka 2011/12 na Sh.106,797,796,940 kwa mwaka 2010/11.

- Kumekuwepo na tatizo kubwa la kutofuata mikataba ya makubaliano ambayo inasisitiza juu ya kuzingatia sheria za fedha na manunuzi Tanzania. Katika kipindi cha ukaguzi tuligundua mapungufu ya manunuzi ya kiasi cha Sh. 32,323,051,169 na Dola za Marekani 114,806. Kwa upande wa fedha kulionekana mapungufu ya kiasi cha Sh.18,775,777,298 na Dola za Marekani 3,391,816.

- Pamekuwepo na ucheleweshwaji wa fedha toka kwa washirika wa maendeleo na Hazina kwenda kwa watekelezaji wa miradi. Ucheleweshaji huu wa fedha umesababisha kuchelewa au kutokutekelezwa kwa miradi iliyokusudiwa na pia kuwepo na kiasi kikubwa cha fedha kisichotumika cha Sh. 346,284,115,450 na dola za Marekani 45,950,595 mpaka kufikia tarehe 30 Juni, 2013. Mtiriko unaonyesha kwa mwaka 2011/12 kulikuwa na Sh. 299,852,509,319, na Dola za Marekani 213,520,573 ambapo mwaka 2010/11 ilikuwa ni Sh. 221,997,432,753 na Dola za Marekani 51,356,184.

- Upungufu wa wafanyakazi wataalamu bado ni tatizo katika kutekeleza miradi ya wafadhili katika baadhi ya halmashauri. Kwa kipindi cha mwaka 2012/13 tumegundua upungufu wa wafanyakazi wataalamu 20,215 ukilinganisha na mahitaji ya wafanyakazi 41,043 wakati kwa mwaka 2011/12 kulikuwa na upungufu wa wafanyakazi 14,663 ukilinganisha na mahitaji ya 73,087.

- Tatizo la kutokuwepo kwa hati za malipo ni kithibitisho kuwa udhibiti wa ndani uko dhaifu. Hili limekuwa tatizo la

muda mrefu katika baadhi ya halmashauri, ningependa kukumbusha Tawala za Serikali za Mitaa juu ya wajibu wao katika kuhakikisha kuwa nyaraka za kifedha kama hati za malipo zinatunzwa vema.

## 8.2 Mambo muhimu ya kuzingatia kutokana na ukaguzi maalum uliofanyika

Jukumu la kuanzisha na kusimamia mfumo wa udhibiti wa ndani kutokana na viwango vya kimataifa vya ukaguzi 240 na Agizo 11 mpaka 14 ya LAFM, 2009, liko chini ya usimamizi wa baraza la halmashauri husika. Hata hivyo, imethibitika kuwa kuna udhaifu katika usimamizi wa mfumo wa udhibiti wa ndani. Hali hii imesababisha utawala kwa njia moja au nyingine kuvuruga mfumo wa udhibiti. Baadhi ya viashiria vya madhaifu yaliyoonekana ni:

- Kuna udhaifu upande wa Menejimenti ya Halmashauri katika kupata na kutunza nyaraka kwa ajili ya ukaguzi. Hii imekuwa na athari kwa kupunguza wigo wa ukaguzi.

- Uongozi wa Halmashauri haukuwa na ufanisi katika kutekeleza majukumu ya usimamizi na kuhakikisha uzingatiaji wa matumizi kwa kufuatana na bajeti. Kutokana na hali hii ya fedha za miradi zimetumika kwa matumizi yasiyokusudiwa, na yale yaliyokusudiwa kutotekelezwa ipasavyo.

## 8.3 Mapendekezo ya Jumla

- Vitengo vya ukaguzi wa ndani katika Wizara na Serikali za Mitaa ni lazima vijihusishe zaidi katika ukaguzi wa miradi inayofadhiliwa na wahisani kwa kuzingatia zaidi maeneo muhimu kama vile ukaguzi wa taarifa za robo mwaka, na utendaji wa miradi inayotekelezwa pamoja na utunzaji wa nyaraka sahihi kwa malipo ya miradi na kufuata mikataba wa makubaliano. Vitengo vya ukaguzi wa ndani vinapaswa kuhakikisha utekelezaji wa miradi ya wafadhili pamoja na usimamizi wa sekta ya fedha za umma unaimarishwa. Hii ni pamoja na kutembelea miradi husika kuona utekelezaji wake.

- Maafisa masuuli wanaohusika na udhibiti wa fedha za umma na usimamizi wa miradi ya wafadhili wanashauriwa kuweka juhudi zaidi katika kuhakikisha kwamba mapendekezo ya ukaguzi ya miaka ya nyuma yanashughulikiwa ipasavyo ili kuondoa uwezekano wa kujirudia kwa mambo hayo hayo katika kaguzi zijazo.

- Maafisa masuuli wanatakiwa kuzingatia udhibiti wa bajeti juu ya matumizi ili kuhakikisha kuwa rasilimali zinatumika katika ubora, ufanisi, kiuchumi na uwazi na matumizi yote yana kumbukumbu za kutosha ili kusaidia kutoa taarifa sahihi.

  Lazima kuwe na udhibiti sahihi na ukaguzi wa awali wa matumizi ili kuzuia, kutambua, kuripoti na kukabiliana na malipo yasiyoidhinishwa, yasiyokuwa na nyaraka, yenye nyaraka pungufu na matumizi yasiyostahili.

- Washirika wa maendeleo, Wizara ya Fedha na Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa wahakikishe utoaji wa fedha kwa wakati kuwezesha utekelezaji wa miradi iliyoainishwa kutekelezwa na kuepuka miradi kubakiwa na kiasi kikubwa cha fedha zisizotumika wakati wa kufunga mwaka.

- Serikali inapaswa kutathmini sifa za watumishi kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa kwani kuna ushahidi kwamba kuna uhaba mkubwa wa watumishi wenye sifa za kusimamia shughuli za Mamlaka za Serikali za Mitaa ikiwemo miradi inayofadhiliwa na Washirika wa maendeleo.

- Halmashauri kwa kushirikiana na Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani pamoja na Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ziweke mpango maalumu wa kusimamia mfumo wa udhibiti wa ndani na mfumo wa utawala bora ambao umekwisha pendekezwa. Mfumo huo ni lazima uwe na malengo na muda maalum wa kufikia malengo hayo.
- Maafisa masuuli wanapaswa kuhakikisha kwamba, matumizi ya fedha katika ununuzi wa kazi za ujenzi,

ununuzi wa bidhaa na huduma yanazingatia matakwa ya Sheria ya Manunuzi wa Umma ya mwaka 2004 pamoja na Kanuni zake za mwaka 2005 na Kifungu Na. 272 cha Memoranda ya Fedha ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa ya mwaka 1997 na Memoranda za makubaliano ili kuepuka manunuzi yasiyo ya lazima.

- Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ni lazima waimarishe au kuwezesha mafunzo ya kina kwa timu ya mkoa ya usimamizi wa afya, na timu ya halmashauri ya usimamizi wa afya juu ya mipango na ujuzi wa kuandika taarifa. Pia kuzingatia ugawaji wa rasilimali za kutosha katika huduma ya kuwafikia walengwa na kufanya usimamizi sahihi juu ya shughuli za kiafya katika Serikali za Mitaa.

- Serikali kuu inapaswa kuhakikisha kuwa inaongeza ufadhili wake katika huduma za afya kulingana na majukumu ya halmashauri katika utekelezaji wa sera ya afya ya taifa ya misamaha na uchangiaji wa gharama.

- Uongozi inapaswa kuhakikisha kuwa bajeti iliyopitishwa ndio inatumika katika kuendesha shughuli za miradi. Pia kabla matumizi hayajaingizwa kwenye rekodi ni lazima kupitiwa ili kuweza kuingiza matumizi kwenye kifungu husika. Hali kadhalika, ni lazima kuwe na kibali cha kulipa matumizi kupitia kifungu kisichohusika.

- Menejimenti lazima ihakikishe kuwa suluhisho za taarifa za kibenki zinaandaliwa vema, zinapitiwa na marekedisho yanafanyika kwa wakati.

- Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii ikishirikiana na TAMISEMI ihakikishe kwamba ugawaji wa fedha, usambazaji wa dawa na vifaa vya afya unazingatia mahitaji halisi kuepuka kugawa zaidi au pungufu ya mahitaji ya wilaya. Hii italeta usawa na kuepukana na tatizo la kuwepo na dawa na vifaa visivyohitajika kwenye wilaya.

- TAMISEMI iandae mfumo wa vifungu utakaowezesha kutambua na kutenganisha fedha za miradi mbalimbali ya maendeleo zilizokusanywa katika akaunti moja kwenye halmashauri. Mfumo huu utawezesha kuweka taarifa sahihi ya mradi ambazo zitarahisisha uandaaji wa taarifa za fedha za mradi ikiwemo salio la mwisho.

**Kiambatanisho Na.I**

**Mapendekezo ya masuala ya miaka iliyopita ambayo hayajatekelezwa - ASDP**

| Na. | Halmashauri | Kiasi (Sh) |
|---|---|---|
| 1 | Wilaya ya Sengerema | 2,343,687,360 |
| 2 | Wilaya ya Kwimba | 2,030,575,000 |
| 3 | Wilaya ya Muleba | 1,807,746,854 |
| 4 | Wilaya ya Mvomero | 1,795,314,299 |
| 5 | Wilaya ya Morogoro | 1,580,310,000 |
| 6 | Wilaya ya Masasi | 1,355,897,887 |
| 7 | Wilaya ya Mbulu | 1,284,487,660 |
| 8 | Wilaya ya Kishapu | 1,278,128,617 |
| 9 | Wilaya ya Biharamulo | 828,213,684 |
| 10 | Wilaya ya Chunya | 741,523,647 |
| 11 | Wilaya ya Kilombero | 695,855,314 |
| 12 | Wilaya ya Nachingwea | 672,732,000 |
| 13 | Wilaya ya Sikonge | 672,032,580 |
| 14 | Wilaya ya Chamwino | 658,943,978 |
| 15 | Wilaya ya Geita | 652,232,213 |
| 16 | Wilaya ya Rorya | 651,883,736 |
| 17 | Wilaya ya Chato | 643,854,248 |
| 18 | Wilaya ya Songea | 633,982,491 |
| 19 | Wilaya ya Ngara | 620,230,478 |
| 20 | Wilaya ya Nkasi | 607,229,406 |
| 21 | Wilaya ya Tarime | 583,208,343 |
| 22 | Wilaya ya Karagwe | 576,434,770 |
| 23 | Wilaya ya Lindi | 575,754,928 |
| 24 | Wilaya ya Liwale | 568,103,560 |
| 25 | Wilaya ya Mbinga | 555,408,570 |
| 26 | Wilaya ya Mtwara | 546,299,488 |
| 27 | Wilaya ya Mbeya | 544,534,630 |
| 28 | Wilaya ya Korogwe | 496,806,568 |
| 29 | Manispaa ya Iringa | 456,998,075 |
| 30 | Wilaya ya Arusha | 441,653,143 |
| 31 | Wilaya ya Kilosa | 384,000,000 |
| 32 | Wilaya ya Musoma | 338,429,000 |
| 33 | Wilaya ya Tabora | 328,084,835 |
| 34 | Mji wa Mpanda | 328,073,109 |

| | | |
|---|---|---|
| 35 | Jiji la Mwanza | 271,328,041 |
| 36 | Wilaya ya Kahama | 265,613,982 |
| 37 | Wilaya ya Kilwa | 264,700,805 |
| 38 | Wilaya ya Ileje | 247,473,679 |
| 39 | Wilaya ya Bariadi | 230,235,000 |
| 40 | Wilaya ya Misungwi | 208,642,697 |
| 41 | Wilaya ya Handeni | 201,798,689 |
| 42 | Wilaya ya Serengeti | 201,772,044 |
| 43 | Jiji la Mbeya | 181,891,824 |
| 44 | Wilaya ya Rufiji | 161,009,586 |
| 45 | Wilaya ya Mkuranga | 157,375,430 |
| 46 | Wilaya ya Hanang’ | 151,175,500 |
| 47 | Wilaya ya Monduli | 129,354,806 |
| 48 | Wilaya ya Karatu | 129,208,984 |
| 49 | Manispaa ya Morogoro | 110,349,715 |
| 50 | Wilaya ya Moshi | 103,065,960 |
| 51 | Wilaya ya Igunga | 98,937,000 |
| 52 | Wilaya ya Manyoni | 94,694,928 |
| 53 | Wilaya ya Maswa | 94,668,650 |
| 54 | Wilaya ya Longido | 93,838,099 |
| 55 | Wilaya ya Mufindi | 93,175,210 |
| 56 | Wilaya ya Misenyi | 90,779,916 |
| 57 | Manispaa ya Singida | 84,513,426 |
| 58 | Wilaya ya Kongwa | 80,000,000 |
| 59 | Manispaa ya Mtwara | 78,683,962 |
| 60 | Manispaa ya Sumbawanga | 77,098,489 |
| 61 | Wilaya ya Tandahimba | 71,693,690 |
| 62 | Wilaya ya Kilindi | 71,373,000 |
| 63 | Wilaya ya Kibaha | 69,433,000 |
| 64 | Wilaya ya Bukoba | 54,000,000 |
| 65 | Wilaya ya Siha | 53,151,660 |
| 66 | Wilaya ya Mafia | 50,707,620 |
| 67 | Wilaya ya Mwanga | 50,280,100 |
| 68 | Wilaya ya Magu | 45,489,850 |
| 69 | Wilaya ya Meatu | 45,485,900 |
| 70 | Wilaya ya Bunda | 39,955,000 |
| 71 | Manispaa ya Temeke | 35,615,000 |
| 72 | Manispaa ya Kigoma | 35,000,000 |
| 73 | Wilaya ya Iramba | 34,816,200 |

| | | |
|---|---|---|
| 74 | Wilaya ya Bukombe | 32,863,106 |
| 75 | Mji wa Babati | 31,943,203 |
| 76 | Wilaya ya Urambo | 29,785,610 |
| 77 | Wilaya ya Lushoto | 29,126,500 |
| 78 | Wilaya ya Bagamoyo | 26,642,865 |
| 79 | Wilaya ya Singida | 25,620,265 |
| 80 | Wilaya ya Bahi | 18,489,684 |
| 81 | Wilaya ya Simanjiro | 17,850,000 |
| 82 | Wilaya ya Mkinga | 16,909,879 |
| 83 | Manispaa ya Shinyanga | 14,377,580 |
| 84 | Manispaa ya Tabora | 13,509,155 |
| 85 | Manispaa ya Bukoba | 12,609,430 |
| 86 | Wilaya ya Nzega | 11,500,000 |
| 87 | Wilaya ya Kiteto | 10,000,000 |
| 88 | Wilaya ya Ruangwa | 9,805,132 |
| 89 | Wilaya ya Ukerewe | 9,127,964 |
| 90 | Manispaa ya Lindi | 8,954,000 |
| 91 | Wilaya ya Shinyanga | 8,715,616 |
| 92 | Wilaya ya Tunduru | 6,286,000 |
| 93 | Wilaya ya Mpwapwa | 5,222,007 |
| | **Jumla** | **33,176,375,908** |

**Kiambatanisho Na.II**

**Mapendekezo ya masuala ya miaka ya iliyopita ambayo hayajatekelezwa – Mfuko wa Maendeleo ya Afya**

| Na. | Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|
| 1 | Wilaya ya Igunda | 958,215,024 |
| 2 | Manispaa ya Dodoma | 817,332,240 |
| 3 | Wilaya ya Sengerema | 641,168,694 |
| 4 | Manispaa ya Tabora | 587,635,967 |
| 5 | Wilaya ya Kasulu | 477,853,545 |
| 6 | Jiji la Mwanza | 467,516,113 |
| 7 | Wilaya ya Kibondo | 422,223,895 |
| 8 | Manispaa ya Temeke | 399,499,850 |
| 9 | Wilaya ya Urambo | 353,616,412 |
| 10 | Wilaya ya Kilwa | 325,481,746 |
| 11 | Wilaya ya Kigoma | 293,950,874 |
| 12 | Wilaya ya Mpanda | 291,029,593 |
| 13 | Wilaya ya Moshi | 268,100,012 |
| 14 | Wilaya ya Chato | 236,694,175 |
| 15 | Wilaya ya Geita | 219,021,575 |
| 16 | Wilaya ya Lushoto | 218,084,200 |
| 17 | Wilaya ya Kwimba | 213,006,152 |
| 18 | Manispaa ya Lindi | 207,715,026 |
| 19 | Wilaya ya Rorya | 206,391,395 |
| 20 | Wilaya ya Korogwe | 192,139,950 |
| 21 | Wilaya ya Njombe | 163,988,753 |
| 22 | Wilaya ya Nkasi | 162,583,373 |
| 23 | Wilaya ya Babati | 156,414,372 |
| 24 | Wilaya ya Kishapu | 154,512,475 |
| 25 | Wilaya ya Sumbawanga | 153,493,964 |
| 26 | Wilaya ya Morogoro | 153,334,251 |
| 27 | Wilaya ya Tunduru | 145,917,000 |
| 28 | Manispaa ya Kigoma | 136,080,217 |
| 29 | Wilaya ya Masasi | 122,739,000 |
| 30 | Wilaya ya Kongwa | 120,820,961 |
| 31 | Wilaya ya Kahama | 119,023,875 |
| 32 | Wilaya ya Iringa | 108,466,803 |
| 33 | Wilaya ya Bagamoyo | 93,043,000 |

| | | |
|---|---|---|
| 34 | Wilaya ya Nachingwea | 88,483,435 |
| 35 | Wilaya ya Kisarawe | 85,379,050 |
| 36 | Wilaya ya Mbulu | 84,316,325 |
| 37 | Wilaya ya Ngara | 84,145,345 |
| 38 | Wilaya ya Lindi | 81,652,760 |
| 39 | Wilaya ya Ukerewe | 78,309,410 |
| 40 | Manispaa ya Sumbawanga | 74,270,765 |
| 41 | Wilaya ya Namtumbo | 73,545,000 |
| 42 | Wilaya ya Tandahimba | 66,882,000 |
| 43 | Mji wa Babati | 65,598,810 |
| 44 | Wilaya ya Hanang' | 63,454,151 |
| 45 | Wilaya ya Magu | 61,382,869 |
| 46 | Wilaya ya Karatu | 55,866,245 |
| 47 | Wilaya ya Missenyi | 50,742,569 |
| 48 | Wilaya ya Karagwe | 49,919,730 |
| 49 | Wilaya ya Bariadi | 47,997,506 |
| 50 | Jiji la Arusha | 47,570,500 |
| 51 | Wilaya ya Shinyanga | 47,335,808 |
| 52 | Wilaya ya Rufiji/Utete | 47,322,383 |
| 53 | Wilaya ya Maswa | 47,142,700 |
| 54 | Wilaya ya Meatu | 46,767,536 |
| 55 | Wilaya ya Monduli | 44,220,712 |
| 56 | Manispaa ya Moshi | 39,368,419 |
| 57 | Wilaya ya Manyoni | 38,895,100 |
| 58 | Wilaya ya Iramba | 38,236,300 |
| 59 | Wilaya ya Siha | 37,296,462 |
| 60 | Wilaya ya Sikonge | 36,158,046 |
| 61 | Wilaya ya Ileje | 35,632,359 |
| 62 | Wilaya ya Meru | 35,453,000 |
| 63 | Wilaya ya Mtwara | 31,548,385 |
| 64 | Mji wa Korogwe | 31,507,195 |
| 65 | Mji wa Mpanda | 26,897,900 |
| 66 | Wilaya ya Musoma | 23,996,559 |
| 67 | Manispaa ya Mtwara | 23,200,011 |
| 68 | Wilaya ya Mwanga | 22,752,550 |
| 69 | Wilaya ya Muheza | 22,192,950 |
| 70 | Wilaya ya Handeni | 21,755,000 |
| 71 | Wilaya ya Misungwi | 19,126,952 |
| 72 | Manispaa ya Iranga | 18,199,972 |

| | | |
|---|---|---|
| 73 | Wilaya ya Kibaha | 16,922,000 |
| 74 | Wilaya ya Ruangwa | 16,713,672 |
| 75 | Wilaya ya Mvomero | 16,041,500 |
| 76 | Jiji la Tanga | 15,113,700 |
| 77 | Wilaya ya Bukombe | 15,003,960 |
| 78 | Wilaya ya Ngorongoro | 14,912,000 |
| 79 | Manispaa ya Songea | 14,060,000 |
| 80 | Wilaya ya Chunya | 13,340,000 |
| 81 | Wilaya ya Mbeya | 13,117,500 |
| 82 | Wilaya ya Kondoa | 12,636,623 |
| 83 | Wilaya ya Rombo | 11,056,753 |
| 84 | Wilaya ya Chamwino | 10,000,000 |
| 85 | Wilaya ya Tarime | 7,550,000 |
| 86 | Manispaa ya Shinyanga | 7,311,566 |
| 87 | Wilaya ya Biharamulo | 7,310,000 |
| 88 | Manispaa ya Morogoro | 6,871,000 |
| 89 | Wilaya ya Mbinga | 6,705,425 |
| 90 | Wilaya ya Muleba | 6,310,240 |
| 91 | Wilaya ya Bukoba | 4,070,922 |
| 92 | Wilaya ya Arusha | 3,236,500 |
| 93 | Manispaa ya Singida | 2,173,500 |
| 94 | Wilaya ya Mkinga | 2,113,936 |
| 95 | Manispaa ya Bukoba | 2,045,000 |
| 96 | Wilaya ya Same | 1,572,000 |
| **Jumla** | | **11,707,805,048** |

**Kiambatanisho Na.III**

**Masuala ya miaka ya nyuma yasiyoshughulikiwa ya Mfuko wa Maendeleo ya Jamii**

| Na. | Halmashauri | Kiasi (Sh) |
|---|---|---|
| 1 | Wilaya ya Musoma | 652,367,864 |
| 2 | Wilaya ya Misungwi | 390,693,542 |
| 3 | Wilaya ya Meatu | 372,283,662 |
| 4 | Wilaya ya Masasi | 315,511,015 |
| 5 | Manispaa yaTabora | 297,994,024 |
| 6 | Manispaa Mtwara Mikindani | 279,886,439 |
| 7 | Wilaya ya Kishapu | 262,987,047 |
| 8 | Wilaya ya Geita | 209,148,871 |
| 9 | Wilaya ya Tarime | 208,005,127 |
| 10 | Wilaya ya Bunda | 182,257,132 |
| 11 | Wilaya ya Sengerema | 174,900,958 |
| 12 | Wilaya ya Mkuranga | 118,252,957 |
| 13 | Wilaya ya Lindi | 108,408,082 |
| 14 | Wilaya ya Bariadi | 108,240,069 |
| 15 | Wilaya ya Longido | 104,118,769 |
| 16 | Wilaya ya Handeni | 98,694,122 |
| 17 | jiji la Mwanza | 72,594,500 |
| 18 | Wilaya ya Rufiji | 67,302,421 |
| 19 | Wilaya ya Misenyi | 52,702,650 |
| 20 | Wilaya ya Pangani | 52,639,309 |
| 21 | Wilaya ya Kisarawe | 48,128,793 |
| 22 | Manispaa ya Moshi | 46,976,469 |
| 23 | Wilaya ya Igunga | 46,417,983 |
| 24 | Wilaya ya Sikonge | 41,999,350 |
| 25 | Wilaya ya Shinyanga | 34,165,312 |
| 26 | Wilaya ya Mvomero | 31,340,000 |
| 27 | Wilaya ya Mkinga | 27,249,055 |
| 28 | Wilaya ya Ruangwa | 23,894,318 |
